# TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR

# RIPOTI YA MAPITIO YA SHERIA YA ELIMU NAM. 6 YA MWAKA 1982 ZANZIBAR

**MWAKA, 2023**

**Inawasilishwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, (AR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Zanzibar**

**MHESHIMIWA HAROUN ALI SULEIMAN,**

**WAZIRI WA NCHI, AFISI YA RAIS- KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA,**

**ZANZIBAR.**

**MHESHIMIWA DKT. MWINYI TALIB HAJI,**
**MWANASHERIA MKUU WA ZANZIBAR,**
**ZANZIBAR.**

**MHESHIMIWA LELA MOHAMMED MUSSA**
**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI**
**ZANZIBAR.**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 14 cha Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar, Nam. 16 ya Mwaka 1986, kwa heshima, Tume inawasilisha Ripoti ya Mapitio ya Sheria ya Elimu Nam. 6 ya mwaka 1982 Zanzibar.

**…………..…………**

**KHADIJA SHAMTE MZEE**
**MWENYEKITI,**
**TUME YA KUREKEBISHA SHERIA,**
**ZANZIBAR**

**15 Mei, 2023.**

# MAKAMISHNA WA TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR



**MHE. KHADIJA SHAMTE MZEE**

**MWENYEKITI**



**DKT.YAHYA KHAMIS HAMAD**
**KAMISHNA**



**ND. SALIM MOHAMED ABDALLA**
**KAMISHNA**



**ND. JUMA MSAFIRI KARIBONA**
**KAMISHNA**



**DKT. SIKUJUA OMAR HAMDAN**
**KAMISHNA**



**MHE. JAJI Geoge Joseph Kazi**
**KAMISHNA**



**ND. MUSSA KOMBO BAKARI**
**KATIBU**

| | |
|---|---|
| Mhe. Khadija Shamte Mzee | Mwenyekiti |
| Mhe. Jaji Geoge Joseph Kazi | Kamishna |
| Dkt. Yahya Khamis Hamad | Kamishna |
| Dkt. Sikujuwa Omar Hamdan | Kamishna |
| Nd. Salum Mohammed Abdalla | Kamishna |
| Nd. Juma Msafiri Karibona | Kamishna |
| Nd. Mussa Kombo Bakari | Katibu |

**WATAFITI**

| | |
|---|---|
| Mhe. Khadija Shamte Mzee | Mwenyekiti wa Tume |
| Nd. Mussa Kombo Bakari | Katibu wa Tume |
| Dkt. Mahfoudha Masoud Ali | Mkurugenzi wa Mapitio ya Sheria |
| Nd. Khamis Ali Jaku | Mkurugenzi wa Mipango, Utumishi Na rasilimali Watu |


Tume ya Kurekebisha Sheria

Vuga, Zanzibar-

P.O BOX 2539,

Simu +255 24 2231143,

Nukushi +255 24 2231137,

barua pepe info@lrcz.go.tz,

tovuti www.lrcz.go.tz

## VIFUNGU VYA UTANGULIZI

**Sheria zilizotumika……………………………………………………………………viii**

**Shukrani……………………………………………………………………………………x**

**Vifupisho vya Maneno……………………………………………………………….xii**

**Muhtasari……………………………………………………………………………….xiv**

**SURA YA KWANZA**

1.0 **UTANGULIZI**…………………………………………………………………………………1

1.1 Mamlaka ya Tume……………………………………………………………………………1

1.2 Chimbuko la Utafiti…………………………………………………………………………..1

1.3 Maelezo ya Tatizo……………………………………………………………………………..2

1.4 Historia ya Elimu Zanzibar………………………………………………………………...3

1.5 Hadidu Rejea…………………………………………………………………………………….5

1.6 Malengo ya Utafiti…………………………………………………………………………….6

1.7 Umuhimu wa Utafiti…………………………………………………………………………..6

1.8 Njia za Utafiti…………………………………………………………………………………..7

**SURA YA PILI**

**2.0 DHANA NA MISINGI YA SHERIA YA ELIMU……………………………………8**

2.1 **Dhana ya Elimu**……………………………………………………………………………8

2.2 Jukumu la kuelimisha ……………………………………………………………………9

2.3 Umuhimu wa elimu…………………………………………………………………………10

2.4 Haki ya kupata elimu………………………………………………………………………10

2.5 Ukuaji wa elimu………………………………………………………………………………11

2.6 Suala la nidhamu katika maskuli…………………………………………………………11

2.7 Viongozi na Kamati za Skuli………………………………………………………………..13

2.8 Ustawi wa walimu……………………………………………………………………………14

2.9 Sera za elimu…………………………………………………………………………………14

2.10 Mfumo wa elimu…………………………………………………………………………….16

2.11 Watoto wenye mahitaji maalum /elimu mjumuisho……………………………………..17

2.12 Tabia za kitaaluma za mwalimu…………………………………………………………19

**SURA YA TATU**

**3.0 SERA, MIPANGO YA KITAIFA NA SHERIA MBALI MBALI……………………………..20**

**3.1 Utangulizi…………………………………………………………………………………..20**

**3.2** Mipango Mikuu…………………………………………………………………………..20

3.2.1 ILANI ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025 ……………………………………….20

3.2.2 Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050……………………………………………..22

**3.3** Sera zinazohusiana na masuala ya elimu…………………………………………..24

3.3.1 Sera ya Elimu ya Mwaka 2006………………………………………………………..24

3.3.2 Sera ya Afya na Usalama Kazini Zanzibar ya Mwaka 2016…………………………..27

3.3.3 Sera ya Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2018 ………………………………………...27

3.3.4 Sera ya Uhakika wa Chakula na Lishe Zanzibar ya Mwaka 2008……………………28

**3.4** Sheria zinazohusiana na Elimu……………………………………………………….29

3.4.1 Katiba ya Zanzibar ya 1984…………………………………………………………....29

3.4.2 Sheria ya Elimu Nam. 6 ya 1982……………………………………………………..30

3.4.3 Sheria ya Kuwalinda Wari na Watoto wa Mzazi Mmoja Nam 4 ya 2005………..34

3.4.4 Sheria ya Mtoto Nam. 6 ya mwaka 2011………………………………………………..36

3.4.5 Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu Zanzibar Nam. 3 ya mwaka 2011....38

3.4.6 Sheria ya Baraza la Mitihani Zanzibar Nam. 6 ya Mwaka 2012……………………...40

3.4.7 Sheria ya Bodi ya Huduma za Maktaba Zanzibar Nam. 7 ya Mwaka 1993……..41

3.4.8 Sheria ya Taasisi ya Elimu Nam. 14 ya mwaka 2016…………………………………42

3.4.9 Sheria ya Vyuo vya Amali Nambari 8 ya mwaka 2006………………………………43

3.4.10 Sheria ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu Nam. 10 ya mwaka 2018…………..44

**SURA YA NNE**

**4.0 MAONI YA WADAU…………………………………………………………………………46**

**4.1 Utangulizi:…………………………………………………………………………………...46**

4.2 Maoni ya Kisera…………………………………………………………………………………..46

4.3 Maoni ya Kisheria……………………………………………………………………………….47

4.4 Masuala ya Kanuni…………………………………………………………………………….....55

4.5 Maoni ya Kiutendaji ……………………………………………………………………………...56

**SURA YA TANO**


**5.0 MIKATABA YA KIMATAIFA, KIKANDA NA UZOEFU WA NCHI NYENGINE………59**

**5.1 Utangulizi…………………………………………………………………………………….59**

**5.2 Mikataba ya Kimataifa..........................................................................................59**

5.2.1 Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu (1948).....................................................59

5.2.2 Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni wa Mwaka 1966...............................................................................................................59

5.2.3 Mkataba wa Haki za Mtoto wa mwaka 1989……………………………………………..61

5.2.4 Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW) wa mwaka 1979…………………………………………………………………….63

5.2.5 Mkataba wa Haki za Watu wenye Ulemavu wa mwaka 2006……………………….64

5.2.6 Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa mwaka 1966…………….65

5.2.7 Mkataba wa UNESCO dhidi ya Ubaguzi katika Elimu wa mwaka 1960…………….65

5.3 Mikataba ya Kikanda…………………………………………………………………………..66

5.3.1 Mkataba wa Afrika wa Haki za binadamu na Watu wa mwaka 1981……………….67

5.3.2 Mkataba wa Afrika wa haki na Ustawi wa Mtoto wa mwaka 1990………………….67

5.3.3 Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa haki za Binadamu na Watu kuhusu Haki za Wanawake katika Afrika ya mwaka 2003……………………………………………...68

5.3.4 Mkataba wa Vijana wa Kiafrika wa mwaka 2006…………………………………………..69

5.3.5 Dira ya Umoja wanchi za Afrika mashariki 2050……………………………………………69

5.3.6 Sera ya Elimu ya Umoja wa Nchi za Afrika Mashariki (EAC) 2016…………………….70

5.4 Uzoefu wa nchi mbali mbali.............................................................................................71

5.4.1 Sheria ya Elimu ya Shelisheli (Seychelles) Nam. 13 Ya Mwaka 2004……………….71

5.4.2 Jamhuri ya Singapore………………………………………………………………………….76

5.4.2.1 Sheria ya Elimu ya Jamhuri ya Singapore ya Mwaka 1957……………………………..76

5.4.2.2 Sheria ya Elimu ya Lazima ya Jamhuri ya Siingapore ya Mwaka 2000………………81

5.4.3 Sheria ya Elimu ya Kenya Sura ya 211…………………………………………………………83

5.4.4 Sheria ya elimu ya Msingi ya Finland Nam. 628 ya mwaka 1998……………………..86

5.4.5 Sheria ya Elimu Nam. 21 ya 2002 ya Grenada, Sura ya 86…………………………………92

5.4.6 Sheria ya Elimu ya Tanzania Nam. 25 ya mwaka 1978……………………………………100

5.4.7 Sheria ya Elimu ya Ghana Nam.778 ya Mwaka 2008……………………………………..105

**SURA YA SITA**

**6.0 MATOKEO YA UTAFITI……………………………………………………………………….107**

**6.1 Utangulizi…………………………………………………………………………………….107**

**6.2** Njia zilizotumika katika Utafiti………………………………………………………………107

**6.3** Makundi ya Wadau (Sampuli ya utafiti) na Uchambuzi wa Takwimu……………107

**6.4** Matokeo ya Utafiti……………………………………………………………………………...114

6.4.1 Matokeo ya Kisera……………………………………………………………………………...114

6.4.2 Matokeo ya Kisheria…………………………………………………………………………...116

6.5 Matokeo ya Kiutendaji……………………………………………………………………….124

**SURA YA SABA**

**7.0 MAPENDEKEZO YA TUME NA HITIMISHO……………………………………………...126**

7.1 **Utangulizi……………………………………………………………………………………….126**

7.2 Mapendekezo ya Kisera……………………………………………………………………….126

7.3 Mapendekezo ya Kisheria……………………………………………………………………...127

7.4 **Hitimisho……………………………………………………………………………………….**141

7.5 **Rejea…………………………………………………………………………………………...143**

## ORODHA YA KATIBA NA SHERIA NA SERA ZILIZOTUMIKA

Sheria ya Elimu ya Shelisheli (Seychelles) Nam. 13 Ya Mwaka 2004

Sheria ya Elimu ya Singapore ya Mwaka 1957

Sheria ya Elimu ya Lazima ya Mwaka 2000 Singapore

Sheria ya Elimu ya Kenya Sura 211.

Sheria ya elimu ya Msingi ya Finland Nam. 628 ya mwaka 1998

Sheria ya Elimu Nam. 21 ya 2002 ya Grenada, Sura ya 86

Sheria ya Tanzania Nam. 25 ya mwaka 1978

Sheria ya Elimu ya Ghana Nam.778 ya Mwaka 2008

### Mipango Mikuu na Sera

ILANI ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025

Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050

Sera ya Elimu ya mwaka 2006

Sera ya Afya na Usalama Kazini Zanzibar ya Mwaka 2016

Sera ya Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2018

Sera ya Uhakiki wa Chakula na Lishe Zanzibar ya Mwaka 2008

### Sheria za Zanzibar

Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984

Sheria ya Elimu, Sura ya 9 ya mwaka 1959 (The Education Decree, 9/1959).

Sheria ya Mfuko wa Elimu ya Juu Zanzibar ya Nam.6 ya mwaka 2001

Sheria ya Elimu Nam. 6 ya 1982

Sheria ya Kuwalinda Wari na Watoto wa Mzazi Mmoja Nam. 4 ya mwaka 2005

Sheria ya Mtoto Nam. 4 ya mwaka 2005

Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu Zanzibar Nam. 3 ya mwaka 2011.

Sheria ya Baraza la Mitihani Zanzibar Nam. 6 ya Mwaka 2012.

Sheria ya Bodi ya Huduma za Maktaba Zanzibar Nam. 7 ya Mwaka 1993

Sheria ya Taasisi ya Elimu Nam. 14 ya mwaka 2016

Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyuo vya Amali Nambari 8 ya mwaka 2006

Sheria ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu Nam. 10 ya mwaka 2018

Sheria ya Tume ya Kurekebisha sheria Zanzibar Nam. 16 ya mwaka 1986

Sheria ya Elimu Nam. 6 ya mwaka 1982

Sheria ya Marekebisho Nam. 4 ya mwaka 2020

**SHUKRANI**

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar imefanikiwa kukamilisha utafiti wa Sheria ya Elimu Nam. 6 ya mwaka 1982 kwa lengo kupata ufanisi wa usimamizi na uendeshaji wa Sekta ya elimu Zanzibar. Kukamilika kwa Utafiti huu kumetokana na juhudi na ushirikiano mkubwa ambao Tume iliopata kutoka ndani nan je ya Tume.

Tume inatoa Shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendeleza Sekta ya elimu na kutaka kufanyiwa mapitio Sheria hii ili iweze kukidhi haja kwa malengo yaliowekwa katika Dira ya 2050 na kuweka utaratibu wa kusimamia sekta hii ambayo ni muhimu zaidi katika maendeleo ya Kiuchumi ya Zanzibar.

Aidha shukrani za dhati ziende kwa Mheshimiwa Mwalim Haroun Ali Suleiman, Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa juhudi zake katika kusimamia sekta ya Sheria ikiwemo miongozo yake kwa Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar. Aidha, Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar inapenda kutoa shukrani kwa Mheshmiwa Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi pamoja na Viongozi wengine wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kwa ushirikiano na msaada mkubwa katika kufanikisha utafiti na mapitio ya Sheria ya Elimu.

Aidha, Tume inatoa shukrani kwa taasisi za Serikali, Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), asasi za kiraia zinazoshughulikia masuala ya elimu, Vyama vya Waalimu, Skuli za kibinasi, Wastaafu katika Sekta ya elimu, na taasisi nyenginezo zilizosaidia kupata maoni, michango na mapendekezo yaliyowasilishwa wakati wa mapitio ya Sheria hii ya Elimu. Vile vile shukrani

za dhati zinatolewa kwa wadau wote waliochangia katika kufanikisha utafiti huu.

Shukrani pia zinatolewa kwa wataalam mbali mbali wa masuala ya elimu kutoka taasisi za Serikali na taasisi binafsi pamoja na watu mashuhuri waliojitolea kutoa maoni yao ya kizalendo kwa manufaa ya Taifa kutokana na uzoefu wao katika sekta hii ya elimu. Maoni na utaalamu wao umeisaidia sana Tume katika kufanikisha ripoti hii.

Aidha, shukrani za dhati ziende kwa Katibu wa Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar Ndg. Mussa Kombo Bakari na wataalam wa Sheria, Utafiti na Mipango, walioongoza zoezi la utafiti na kufanya uchambuzi yakinifu wa taarifa na uandishi wa ripoti hii.

Katika kukamilisha Utafiti huu, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Makamishna wote wa Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar kwa michango yao iliyosaidia katika utafiti huu na utayarishaji wa Ripoti hii.

**VIFUPISHO VYA MANENO:**

| | |
|---|---|
| CEDAW | Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake |
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| EAC | Jumuiya ya Umoja wa Nchi za Afrika Mashariki |
| FAWE | Jukwaa la Wanawake wa Wasomi wa Kiafrika |
| ICT | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| MKUZA | Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar |
| S.O.S | Kituo cha Kulelea Watoto Yatima |
| SUZA | Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| UNESCO | Shirika la Kimataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni |
| ZAFELA | Chama cha Wanasheria Wanawake Zanzibar |

| | |
|---|---|
| ZATU | Chama Cha Walimu Zanzibar |
| ZATUC | Chama Cha Wafanyakazi Zanzibar |

**MUHTASARI**

Sekta ya elimu Zanzibar ina historia refu tokea wakati wa ukoloni. Elimu ya kikoloni haikulenga kutoa fursa sawa za elimu kwa wote na upatikanaji wa elimu haukuwa ni haki ya kila mtu. Utoaji wake ulizingatia matabaka ya kijamii na ubaguzi wa rangi. Kwa sasa mfumo wa Elimu unasimamiwa na Sheria ya Elimu ya Zanzibar ya mwaka 1982 ya Zanzibar, na kufanyiwa marekebisho makubwa mwaka 1993, pamoja na kutunga Sera ya Elimu kwa Zanzibar ya mwaka 2006.

Katika kufanya utafiti huu, njia mbalimbali zimetumika ikiwemo kupitia rejea mbali mbali za ndani na nje ya nchi, kuangalia miongozo ya kimataifa na Sheria za elimu za nchi nyengine, kupitia Katiba ya Zanzibar, Sera na Sheria mbali mbali za ndani ya nchi, pamoja na kukusanya maoni ya wadau na wataalamu wa sekta ya elimu Zanzibar.

Aidha, baada ya kukamilika kwa ukusanyaji wa maoni na taarifa nyenginezo, Tume imebaini mapungufu na changamoto mbali mbali za Kisheria na utekelezaji ambazo zimechangia Sheria hii kufanyiwa mapitio ikiwemo, kutokuzingatiwa mipango iliyoelezwa katika Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020 na vipaumbele vya uchumi vilivyowekwa katika Mipango ya Maendeleo Zanzibar. Aidha, kubadilika kwa mfumo wa elimu utakaowawezesha vijana kujiajiri wenyewe zaidi kuliko kutegemea ajira za Serikali pamoja na kuwepo kwa baadhi ya maeneo ambayo tayari yametungiwa Sheria nyengine kama Sheria ya Vyuo vya Amali, Ukaguzi wa elimu na nyenginezo, kujumishwa kwa masuala mengine katika masuala ya

Muungano kama Suala la Elimu ya Juu kumeifanya Sheria hii kuhitaji mapitio ya kina.

Maeneo mengine yanayokwaza utekelezaji wa Sheria hii ya Elimu iliyopo kwa sasa ni kutokuwekwa mazingira ya kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa shughuli za elimu kupitia vyombo mbali mbali vilivyopewa kazi ya usimamizi wa sekta hii. Aidha, kutokuwekwa mgawanyo ulio wazi baina ya majukumu ya Serikali, Waziri, Tawala za Mikoa, Bodi ya Elimu na vyombo vyengine vya usimamizi, pamoja na kutokubainishwa majukumu ya wadau muhimu kama walezi, wazee na jamii katika kusimamia masuala ya elimu, yameonekana kukwaza sekta ya elimu.

Utafiti umebaini Sheria iliyopo haikuweka wazi masuala ya usajili kwa skuli za Serikali na binafsi, masharti na vigezo vya usajili na taratibu nyenginezo, taratibu za usajili wa walimu, kutokuwepo utaratibu wa uwasilishaji wa malalamiko, pamoja na changamoto nyenginezo katika maeneo mbali mbali ya utekelezaji wa sheria hii.

Mapitio ya Sheria ya Elimu Zanzibar yatasaidia kuweka vyema misingi mizuri ya usimamizi wa elimu, kuiendeleza sekta ya elimu ili iweze kwenda na wakati uliopo na kuifanya elimu iwe chachu ya mabadiliko ya teknolojia, maendeleo endelevu, na kuimarisha upatikanaji wa huduma za kijamii hapa nchini.

Utafiti umependekeza mambo mbali mbali ya kufanywa wakati wa utekelezaji wa Sheria ya elimu itakayokuja. Hivyo mambo hayo ni muhimu kuzingatiwa katika sheria inayokusudiwa kutungwa, ikiwemo kuweka wazi malengo ya

kuwepo kwa Sheria ya Elimu, kuimarisha misingi katika masuala ya elimu, kutambua vyombo vya usimamizi wa masuala ya elimu na kazi zake, kutambua na kuweka Jukumu la mamlaka za Serikali za Mitaa katika sekta ya elimu, kuweka utaratibu mzuri wa masuala ya nidhamu na adhabu, kuwa na mitaala iliyo bora zaidi kwa manufaa ya nchi na kuwa na mfumo mzuri wa uteuzi wa wajumbe wa kamati za Skuli na vyombo vyengine vya usimamizi wa sekta ya elimu.

Mapendekezo mengine ni kutambua Idara na taasisi za usimamizi wa elimu ndani ya Wizara husika, kuweka utaratibu bora zaidi katika upimaji wa viwango vya elimu, uanzishwaji wa Jukwaa la Elimu, suala la uzingatiaji wa teknolojia katika elimu, uchunguzi wa afya za wanafunzi na mazingira, uanzishwaji wa Mfuko wa elimu, majukumu ya wazazi na wanafunzi, Walimu Wakuu, Kamati za Skuli na Jamii kwa ujumla, mfumo bora wa Usajili wa skuli, mfumo wa uendeshaji na muundo wa skuli za binafsi na Serikali pamoja na usimamizi wa walimu na usajili wa walimu.

Tume inaamini matokeo na mapendekezo ya utafiti huu iwapo yatafanyiwa kazi ipasavyo, yatasaidia kuweka usimamizi mzuri katika sekta ya elimu na huduma ya elimu inayotolewa na kuleta mabadiliko ya upatikanaji wa elimu na matarajio ya Serikali katika masuala yote yanayohusiana na elimu hapa nchini.

**SURA YA KWANZA**

## 2.0 UTANGULIZI

### 1.9 Mamlaka ya Tume

Tume ya Kurekebisha Sheria ya Zanzibar imeanzishwa chini ya Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria.[1] Sheria hiyo inaipa uwezo Tume kuzifanyia mapitio sheria zote za Zanzibar kwa nia ya kuzirekebisha ili ziende sambamba na maendeleo na mabadiliko ya kimfumo.[2]

Tume ya Kurekebisha Sheria katika kufanya mapitio ya sheria inaweza kufanya mapitio kwa kutumia njia tatu zilizoainishwa katika sheria. Njia ya kwanza, inataka Tume kuangalia haja ya Mapitio ya Sheria ikiona ipo haja ya kufanya hivyo,[3] njia ya pili ni kwa maelekezo ya Waziri anayehusika na mambo ya sheria,[4] na njia ya tatu ni kwa maelekezo ya Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar.[5]

Kutokana na uwezo iliyopewa kwa mujibu wa Sheria, na katika kutekeleza majukumu yake ya msingi, Tume imefanyia mapitio ya Sheria ya Elimu[6] kwa ajili ya kuainisha mapungufu ya sheria hiyo na kupendekeza Serikalini marekebisho yake.

### 1.10 Chimbuko la Utafiti

[1] Sheria Nam. 16 ya mwaka 1986
[2] Kifungu cha 4(1) cha sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar Nam. 16 ya mwaka1986
[3] Ibid kifungu 4(2)
[4] Ibid Kifungu cha 7
[5] Ibid kifungu cha 8
[6] Sheria ya Elimu Nam. 06 ya mwaka 1982

Mabadiliko ya Kisera katika sekta ya elimu, pamoja na Mipango ya nchi ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020-2050 na ILANI ya Uchaguzi ya CCM ya 2020, mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia, pamoja na mwelekeo wa Uchumi yamepelekea haja ya kufanyiwa mapitio kwa Sheria ya Elimu Nam. 6 ya mwaka 1982.

Mabadiliko hayo yameifanya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuitaka Tume ya Kurekebisha Sheria kuifanyia mapitio Sheria hiyo kulingana na mabadiliko mbalimbali ndani ya Serikali na mabadiliko katika ngazi ya kimataifa yaliyojitokeza na ikibidi kupendekeza mabadiliko katika mfumo wa Kisheria na utendaji na utekelezaji wa malengo ya Serikali.

### 1.11 Maelezo ya Tatizo

Sekta ya elimu ni eneo ambalo linabadilika kutokana na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, Kisayansi na teknolojia na hivyo linahitaji kufanyiwa mapitio mara kwa mara ili liendane na mahitaji na wakati uliopo. Mbali ya kuwepo kwa mabadiliko mbalimbali ya kiuchumi, mabadiliko ya Sera za nchi, Dira ya Maendeleo ya 2050 na malengo ya millennia, bado Sheria ya Elimu Nam. 6 ya mwaka 1982 haijafanyiwa mabadiliko ili kujumuisha malengo yaliyoainishwa katika mipango hiyo. Sheria hii imefanyiwa marekebisho mwaka 1993 na mwaka 2020 katika maeneo ya ugatuzi.

Kutokana na umuhimu wa kuibadilisha sekta hii ya elimu, ili isaidie zaidi jamii na iendane na mipango ya nchi iliyopo, Serikali imeona umuhimu wa kufanyiwa mapitio Sheria ya Elimu Nam. 6 ya mwaka 1982.

## 1.12 Historia ya Elimu Zanzibar

Zanzibar iliwahi kuwa sehemu ya Oman katika karne ya 19 chini ya Seyyid Said, ambaye alihamisha mji mkuu wake kutoka Oman hadi Zanzibar. Kuanzia 1890 hadi 1963, Zanzibar ilikuwa chini ya himaya ya ulinzi wa Uingereza, na Sultan kama mkuu wa nchi.[7]

Sekta ya elimu Zanzibar ina historia refu tokea wakati wa ukoloni. Kipindi cha 1905-1920 suala la elimu lilisimamiwa na Mkurugenzi wa Elimu Rivers Smith na Resident Pearce ambao walijaribu kuainisha sera ya elimu na kuingiza athari za Skuli za Serikali katika taasisi za dini[8], ingawa walikumbana na vikwazo kwa viongozi wa kidini ambao hawakuwa wamejitayarisha kupokea mchanganyiko huo.[9]

Katika mwaka 1923, Ofisi ya kikoloni iliunda Kamati ya ushauri katika masuala ya elimu kwa nchi zilizo katika Tropiki ya Afrika (Tropical Africa), ingawa elimu hiyo ilikuwa haisaidii wananchi kutokana na mahitaji na kufanikiwa kielimu kulikuwa kunategemea Gavana aliyepo, na elimu iliyotolewa haikuwa na maslahi kwa wananchi.[10]

---

[7] Lofchie, M. F. (2015). Zanzibar: Background to revolution. United States of America: Princeton University Press.

[8] ibid

[9] Zehlia Babaci- (2015) "Zanzibar's Curriculum Reform: Implications for Children's Educational Rights," part of comparative and International Education book series, Q*uarterly Review of Comparative Education*, v45 n2 p181-195 Jun 2015, ukurasa wa 198

[10] W. Hendry Some Aspects of Education in Zanzibar, Journal of the Royal African Society, Vol. 27, No. 108 (Jumai 1928), pp. 342-352 (11 pages) Published By: Oxford University Press)

Elimu ya kikoloni haikulenga kutoa fursa sawa za elimu kwa wote na Watawala wa Uingereza wa Zanzibar hawakuona elimu kama haki ya binadamu, hivyo utoaji wake ulizingatia matabaka ya kijamii na ubaguzi wa rangi, huku Waafrika wakiwa ndio kundi la watu wasiojiweza.[11]

Katika mwaka 1940-1963, utawala wa Kingereza ulikubali kujumuisha wataalam wa Alawy katika sera za kikoloni na mafunzo ya Quran ambayo yalijumuishwa kwa mara ya kwanza katika mwaka 1952 na kupelekea kuanzishwa kwa Chuo cha Kiislamu (Muslim Academy).[12] Katika kipindi hicho, elimu rasmi ilizingatiwa katika vyuo na taasisi za mafunzo ya dini ya kiislam, skuli ya Wahindi na skuli za misheni hadi mwaka 1964 wakati Zanzibar ilipopata uhuru wake kupitia Mapinduzi ya tarehe 12 Januari, 1964.[13]

Hali ya kielimu baada ya uhuru wa mwaka 1964 ilibadilika na kutangazwa Elimu bure kwa Wazanzibari wote, kwa ngazi ya elimu ya awali na skuli ya msingi bila kujali tofauti za rangi na jinsia.[14] Tokea wakati huo mfumo wa elimu umekuwa ukipitia mabadiliko tofauti katika Maendeleo ya elimu na marekebisho ya sera yaliyofanywa ili kuendana na matamko ya kimataifa ya maendeleo ya elimu.[15]

---

[11] Mapuri, O. R. (1996). Zanzibar, the 1964 revolution: Achievements and prospects. Dar es Salaam: Tema.

[12] R.P.L Loimeier, Between Social Skills and Marketable Skills, Chapter Five. The Politics Of Education In The Colonial Period I: Schools, Pages: 1500–1573 DOI: https://doi.org/10.1163/ej.9789004175426.i-1929.30

[13] ibid

[14] Abdalla. S.M. (2014) Education statistical Abstract, Ministry of Education and vocational training Zanzibar.

[15] Anangisye, W. A., & Fussy, D. (2014). Tanzania: Revisiting eastern and central African education systems. In C. Wolhuter (Ed.), Education in East and Central Africa, (pp. 373—398). London: Bloomsbury.

Mwaka 1982, Zanzibar ilitunga Sheria ya Elimu Nam. 6 ya 1982, ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 1993. Aidha Sera ya Elimu ya Zanzibar ilitungwa mwaka 1991 na kufanyiwa marekebisho mwaka 1995.[16] Kufuatia kutamkwa kwa mikataba na matamko ya kimataifa, Sera ya mwaka 1991 ilieleza malengo na shabaha muhimu za kisekta ambazo kama Taifa linatarajia kufikia. Aidha, katika mwaka 1996, Serikali ilitoa mpango mkuu wa elimu Zanzibar (ZEMAP) ambao uliainisha malengo ya elimu ya Zanzibar kwa miaka kumi ijayo.[17] Mwaka 2006 Sera ya Elimu ya mwaka 1991 ilifutwa na badala yake, Sera ya Elimu ya mwaka 2006 ilitungwa. Sera hii ililenga kuleta mabadiliko zaidi katika sekata ya elimu nchini.

Mabadiliko kwenye sekta ya elimu yalifanyika katika mwaka 2020 kwa kuzipa Serikali za Mitaa mamlaka ya kusimamia masuala ya elimu katika skuli za maandalizi na msingi kwa utaratibu wa ugatuzi na hivyo, masuala ya uandikishwaji, ufundishwaji na uajiri ukawekwa chini ya Serikali za Mitaa.[18]

Kutokana na changamoto za kiutendaji zilizojitokeza baada ya marekebisho ya Sheria ya Elimu yaliyofanywa mwaka 2020, Serikali ilifanyia marekebisho sekta ya elimu kwa kurudisha mamlaka ya usimamizi wa elimu chini ya Wizara ya Elimu (kuondoa ugatuzi katika eneo hilo) kupitia Sheria Nam. 5 ya mwaka 2021.

[16] Revolutionary Government of Zanzibar Ministry of Education and Vocational Training, Zanzibar Education Development Programme (ZEDP) 2008/09 – 2015/16 DRAFT 3 February 6, 2007, https://www.globalpartnership.org/sites/default/files/2008-02-Tanzania-Zanzibar-Sector-Plan.pdf , katika 1.4.1 ukurasa wa 8

[17] ibid

[18] Marekebisho ya kifungu cha 26 cha Sheria ya Elimu, Nam. 6 ya Mwaka 1982 pamoja na kuingizwa vifungu vipya vya 26 A na 26 B vya Sheria ya Marekebisho Nam.4 ya mwaka 2020

## 1.13 Hadidu Rejea

Katika kufanya utafiti huu Hadidu Rejea zifuatazo zilizingatiwa:

(a) Kupitia mabadiliko yaliyopo katika miongozo ya Elimu Zanzibar, pamoja na mipango ya elimu iliyowekwa na Serikali na kulinganisha na sheria iliyopo.

(b) Kuangalia uzoefu wa Sheria za nchi mbalimbali kuhusiana na masuala ya elimu na kuangalia, namna uzoefu huo unavyoweza kutumika kwa mazingira ya Zanzibar;

(c) Kukusanya maoni ya wadau mbalimbali wanaohusika na sekta ya elimu ili kuimarisha mfumo na sekta nzima ya elimu.

(d) Kutoa mapendekezo yanayofaa ya kisheria na kisera kwa ajili ya kutatua changamoto zinazokwaza sekta ya elimu na namna ya kuweka mfumo wa kisheria utakaoimarisha masuala ya Elimu Zanzibar.

## 1.14 Malengo ya Utafiti

Lengo la kufanya utafiti huu ni kuangalia mapungufu yaliyopo katika Sheria ya Elimu Nam. 6 ya mwaka 1982 kwa kuzingatia Sera ya Elimu na marekebisho yake na mipango ya nchi katika usimamizi wa sekta ya elimu na kupendekeza marekebisho yake Serikalini.

## 1.15 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu wa mapitio ya Sheria ya Elimu Zanzibar utasaidia kuweka misingi mizuri ya usimamizi wa sekta nzima ya elimu, kuiendeleza sekta ya elimu kwa kuiwekea misingi inayokwenda na wakati uliopo na mabadiliko ya teknolojia, kuleta maendeleo endelevu katika sekta na taasisi mbalimbali zinazosimamia masuala ya elimu; na kuimarisha upatikanaji wa huduma za elimu Zanzibar.

### 1.16 Njia za Utafiti

Katika kufanya utafiti huu, njia mbalimbali zimetumika ikiwemo kupitia rejea mbali mbali za ndani na nje ya nchi, na kuangalia miongozo ya kimataifa na sheria za nchi nyengine, Katiba, Sera na Sheria mbali mbali, pamoja na kukusanya maoni ya wadau na wataalamu wa sekta ya elimu Zanzibar.

## SURA YA PILI

## 3.0 DHANA NA MISINGI YA SHERIA YA ELIMU

### 2.1 Dhana ya Elimu

Elimu ina maana ya mabadiliko katika mwenendo wa maisha ya mwanadamu, na uwezo wa kuchagua kilicho bora zaidi katika hali ambayo mtu anakabiliana nayo.[19] Elimu inatafsiriwa pia kama maendeleo ya kumtayarisha mtu kupitia njia bora ya kutatua shida wakati wowote au uwezo wa kurekebisha hali kulingana na mazingira.[20]

Elimu ni zaidi ya uwekezaji wa kiuchumi na ni nyanja muhimu ambayo maisha, maendeleo na uhai wa mwanadamu hutegemea.[21] Elimu ni haki ya binadamu na njia muhimu ya kufikia haki nyengine za binadamu ambayo imeelezwa katika sheria na Katiba za nchi mbalimbali. Kwa maana pana, elimu haimalizii darasani au skuli pekee, bali ni mchakato mrefu wa maisha unaojumuisha uzoefu wote, maarifa na hekima ambayo mtu amepata katika hatua tofauti za maisha yake kupitia njia tofauti (yaani, njia rasmi, au njia isiyo rasmi).[22]

---

[19] Bogonko, S. N(2000). Reflections on education in East Africa. Nairobi Kenya: Oxford University Press

[20] Nyerere, J.K (1967). Education for Self Reliance. Arusha United Republic of Tanzania

[21] World Bank (1996). Tanzania: The Challenge of Reforms: Growth, Incomes and Welfare.Volume 1, World Bank

[22] Kuleana (1999). The State of Education in Tanzania: Crisis and Opportunity. Mwanza, Kuleana in Tanzania: Debate and Action. Dar es Salaam, University of Dar es Salaam Convocation

Mtazamo mwengine huchukulia elimu kama kitendo kinachohusiana na malezi au athari ya ziada kwa utu wa mtu binafsi. Inaaminika kuwa elimu sio tu chombo cha mabadiliko ya kijamii, lakini pia uwekezaji katika maendeleo ya taifa.[23] Mtazamo kama huo wa elimu unajumuisha uzoefu wote wa maisha, kwani kuna mabadiliko kutoka maendeleo ya mtu binafsi hadi maendeleo ya taifa.[24]

## 2.2 Jukumu la kuelimisha

Kawaida jukumu la kutoa elimu ni jukumu la kila mtu katika nchi ikiwemo; wazazi, watu wazima, au walimu, katika sekta ya umma au binafsi, ili kusaidia kutoa fursa kwa watu wote kujiendeleza kikamilifu kadri iwezekanavyo.[25]

Elimu inapaswa kuwa njia ya kuwawezesha watoto na watu wazima kuwa washiriki hai katika mabadiliko ya jamii zao na kujifunza na kuzingatia maadili, mitazamo na tabia zinazowezesha watu binafsi kujifunza kuishi pamoja katika maeneo tofauti.[26] Kwa hiyo elimu ina nafasi muhimu katika kukuza utaalamu na uelewa wa haki za binadamu, msingi wa maadili na utaalamu unaohitajika ili kuimarisha utamaduni na kidemokrasia.[27]

Elimu huzalisha kizazi kipya kinachowezesha kutatua matatizo halisi katika jamii na hivyo watu wengi hawaridhiki na elimu yao ya msingi na wanajaribu

---

[23] Fisher, R. 1990. Teaching children to think. Nelson Thornes, Cheltenham.

[24] Kumar, S. & Ahmad, S. (2008): Meaning, aims and process of education. In: School of Open Learning. Newark: Science and Education Publishing.

[25] MEoC(2001).Education sector development programme: Primary Education Development Plan, 2002–2006.Dar es Salaam: United Republic of Tanzania Mkuki Press

[26] Abagi, O. and Odipo, G (2000). Implementing the Report of the Commission of Inquiry into the Education System Dar es salaam Data star

[27] Abdalla. S.M. (2014) Education statistical Abstract Ministry of Education and vocational training Zanzibar

kupata elimu ya juu zaidi ili kukidhi matakwa ya jamii ya kisasa.[28] Watu hujitolea kwa kutumia pesa kuinua kiwango cha elimu kwa sababu wanatambua kuwa elimu kwao ni muhimu hasa katika siku zijazo.

Jukumu la elimu ni kutoa uelewa kamili katika utambulisho wa mtu au kitu, kutoa huduma kwa jamii, kukuza elimu ya uraia, na kufanya matendo mazuri yanayokubalika. Kwa hivyo, ni muhimu kwa elimu kusisitiza hisia ya uraia, ambapo wanafunzi hujifunza umuhimu wa kusaidia na kuchangia katika familia, jamii taifa kwa jumla.[29]

## 2.3 Umuhimu wa elimu

Elimu ni muhimu kwa maendeleo ya maarifa na uelewa na ukuzaji wa haki za binadamu na demokrasia, na kulinda mazingira.[30] Elimu inasaidia katika ukuaji wa mtu na kuinua hali za watu au kuwatoa katika umasikini; inawapa watu maana ya kushiriki kikamilifu katika jumuiya zao; inawawezesha wanawake; na inawalinda watoto dhidi ya unyanyasaji na udhalilishaji. Elimu pia inatambulika kama moja ya uwekezaji bora wa kifedha ambao Serikali inaweza kufanya.[31]

## 2.4 Haki ya kupata elimu

Haki ya kupata elimu inategemea mwelekeo wa kijamii na mwelekeo wa uhuru. Hivyo, haki hii inaifanya Serikali kuchukua hatua mbalimbali ili elimu ipatikane

[28] Hija, I. M. (2010) Zanzibar. International Encyclopedia of Education (Third Edition), 896-903
[29] Cohen, L., Manion, L., & Morrison, K. (2018). *Research methods in education* (8th ed.). Routledge.
[30] Abdulghani Al-Shuaibi (2014) The Importance of Education, Salalah College of Technology, https://www.researchgate.net/publication/260075970_The_Importance_of_Education
[31] Committee on Economic, Social and Cultural Rights, *General Comment 13, the Right to Education,* Twenty FirstSession, 1999, para. 1

kwa urahisi kwa watu wote na kuanzisha hatua na taratibu za huduma ya elimu bila malipo.[32]

Kipimo cha uhuru kinamaanisha uhuru wa watu binafsi au uhuru wa wazazi na walezi ambao huchagua taasisi za elimu zinazokidhi viwango vyao vya elimu au imani zao za kidini au maadili.[33] Haki ya kupata elimu inahitaji Serikali kuwajibika katika kuhakikisha upatikanaji, ufikiaji, na kubadilika kwa elimu.[34]

## 2.5 Ukuaji wa elimu

Ukuaji wa elimu unakuza maarifa na hivyo shughuli za skuli lazima zibuniwe kwa njia ambayo inakuza maendeleo binafsi ya wanafunzi.[35] Ukuaji wa elimu unalenga kutoa motisha katika kufikia malengo ya mwanafunzi kujifunza.

Katika ukuaji wa elimu inasisitizwa umuhimu wa kukuza maendeleo binafsi ya kila mwanafunzi ili kuwa na mabadiliko kutoka kwa mtazamo wa kibinadamu na kuongeza maarifa katika masomo, maendeleo ya wanafunzi, na mambo yanayoathiri wanafunzi nje ya maeneo ya skuli.[36]

## 2.6 Suala la nidhamu katika maskuli

---

[32] Bryk, A. S., Gomez, L. M., Grunow, A., & LeMahieu, P. G. (2015). *Learning to improve. How America's schools can get better in getting better*. Harvard Education Press.

[33] Dewey, John (2016). Democracy and Education. New YorkThe Free Press Education

[34] Boyd, W. L., & Crowson, R. L. (2002). The quest for a new hierarchy in education: From loose coupling back to tight? *Journal of Educational Administration*, *40*(6), 521–533. https://doi.org/10.1108/09578230210446018

[35] Joanna Giota & Ingemar Emanuelsson (2018) Individualized teaching practices in the Swedish comprehensive school from 1980 to 2014 in relation to education reforms and curricula goals, Nordic Journal of Studies in Educational Policy, 4:3, 144-155, https://doi.org/10.1080/20020317.2018.1541397

[36] Ninni Wahlstrom, Daniel Sundberg (ed) (2018) Transnational Curriculum Standards and Classroom Practices The New Meaning of Teaching, 1st Edition, Routledge, ukurasa wa 68

Nidhamu ya skuli ni eneo jengine muhimu katika usimamizi wa elimu. Hii ni kwa sababu nidhamu ni mfumo wa maisha kwa mujibu wa kanuni zilizowekwa na jamii ambazo wanajamii wote wanapaswa kuzingatia na ukiukwaji wake unamuweka mtu katika sehemu nyengine kimaadili.[37]

Kwa hiyo, lengo la nidhamu ni kumsaidia mtu binafsi kurekebishwa na kuwa mwenye manufaa kwa jamii yake. Mafundisho ya nidhamu katika skuli kulingana na Nakpodia (2009), yanatokana na dhana ya kutoa mamlaka ya skuli na wajibu kamili wa malezi ya watoto, haki ya nidhamu na udhibiti.[38]

Jukumu la kuweka nidhamu katika skuli limeachwa pia kwa walimu ambao wana haki ya kuwaadabisha wanafunzi wanaokiuka sheria za skuli. Hivyo, mazingira hayo ya kuchunga nidhamu za wanafunzi kuwapelekea wazazi kukubali kukabidhi watoto wao kwa maofisa wa skuli na kuhamisha kwa maafisa hao, mamlaka ya mzazi ya kudhibiti mwenendo wa watoto wao kwa namna ambayo itakuwa ya manufaa kwa mtoto.[39]

Nidhamu ya skuli inatumia "dhima ya urithi" ambayo hutumika kumfanya mtu mmoja kuwajibishwa kwa matendo ya mwengine anaposhiriki katika aina fulani ya shughuli iliyoshirikisha watu kwa pamoja au humfanya mwanafunzi kuwajibika kwa madhara yanayosababishwa na mwengine, kwa sababu ya uhusiano fulani unaofaa kisheria kati ya hao wawili.[40] Katika eneo hili la

[37] Imaguezor, M. V. (1997). *Analysis of Cases of Violation of Students Rights in Secondary Schools in Edo State*. M.Ed Thesis, University of Benin, Nigeria.
[38] Nakpodia, E.D. (2009). Perceptions of Principals' Responsibilities in in-loco-parentis in Nigerian Secondary Schools. *Journal of Education Administration and Policy Studies*, 1 (1), 1-7.
[39] Everard, K.B. Geoffrey, M. & Wilson, J. (2004). *Effective school management.* Fourth Edition. London: Paul Chapman Publishing
[40] John, B. & Earl, M. (2003). Key *issues in secondary education: Introductory readings.* New York: Continuum

nidhamu inashauriwa, mwalimu mkuu kuwahusisha wazazi na walimu inapobidi katika kufanya maamuzi.[41]

## 2.7 Viongozi na Kamati za Skuli

Vyombo vya usimamizi ndani ya skuli vinasaidia skuli kujitathmini katika kuanzisha, kuongoza, na kusimamia mabadiliko ya skuli husika na kupelekea mabadiliko na ufanisi. Viongozi wa elimu pia wanajukumu katika kuweka tathmini ya skuli kwa kuzingatia muundo wa usimamizi wa skuli.[42] Mambo ambayo yanasaidia katika usimamizi wa skuli ni ubunifu, matokeo ya mitihani, rasilimali na maendeleo ya walimu na wanafunzi.

Ili kuwezesha mabadiliko katika skuli, wasimamizi wanapaswa kuimarisha uongozi utakaotimiza malengo ya skuli na kukuza usimamizi wa maadili kwa wadau wote, kuzingatia na kuchagua kwa uangalifu shabaha za skuli na kudhibiti rasilimali, pamoja na kujenga ari ya wafanyakazi.[43]

Viongozi wenye ufanisi ni wale wanaoweza kupitisha na kusimamia mbinu za kubadilika kwa urahisi katika kukabiliana na changamoto zinazotokana na mabadiliko ya mazingira ya nje na katika kuongoza skuli zao ili ziwe bora.[44] Viongozi wa skuli wanapaswa kuwa kitu kimoja, kati yao na wazazi, kupanga

---

[41] John, B. & Earl, M. (2003). Key *issues in secondary education: Introductory readings.* New York: Continuum.

[42] Education and Manpower Bureau (2003): Enhancing school development and accountability through school self-evaluation and external school review. EMB Circular No. 23/2003.

[43] Berjaoui, R. R. & Karami-Akkary, R. (2019): Distributed leadership as a path to organisational commitment: the case of a Lebanese school. Leadership and Policy in Schools, 19(4), 610-624.

[44] Scottish Office (2002): How good is our school? Self-evaluation using performance indicators. Edinburgh: the Scottish Office of Education and Industry Department.

mikakati au kujadili mafanikio na changamoto zinazoikabili skuli na kuimarisha uhusiano baina yao.[45]

## 2.8 Ustawi wa walimu

Hali duni kwa walimu inaweza kuwa na madhara makubwa kwa taaluma ya ualimu ikiwa haitashughulikiwa. Kwa mfano, hali hiyo inaweza kusababisha walimu kuacha taaluma, kukosa ari ya kufundisha jambo ambalo linaweza kugharimu skuli na mfumo wa elimu.[46]

Watafiti wanakiri kwamba walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu ambayo yanaweza kuathiri vibaya ustawi wao, wanakabiliwa na mahitaji ya ushindani hata katika hali ya kawaida, ambayo inaweza kusababisha dhiki na wasiwasi, na kuongeza migogoro. Changamoto zinazowakabili walimu zisiposhughulikiwa kwa awamu zitaathiri mifumo yao ya ufundishaji. [47] Kuendelea kwa ufundishaji na ufunzaji kunategemea jinsi walimu wanavyosaidiwa na kukuza hali ya kujiamini kwao nyakati za migogoro na huhitaji maamuzi magumu ili walimu watekeleze wajibu wao.[48]

## 2.9 Sera za elimu

[45] Martin, A. J., Nejad, H., Colmar, S. & Liem, G. A. D. (2012): Adaptability: Conceptual and empirical perspectives on responses to change, novelty and uncertainty. Journal of Psychologists and Counsellors in Schools, 22(1), 58-81.

[46] Randall, L. & Coakley, L. (2007): Applying adaptive leadership to successful change initiatives in academia. Leadership & Organization Development Journal, 28(4), 325- 335

[47] Sokal, L., Trudel, L. E. & Babb, J. (2020): Canadian teachers' attitudes toward change, efficacy, and burnout during the COVID-19 pandemic. International Journal of Educational Research Open, 1, 1-8.

[48] Spilt, J. L., Koomen, H. M. & Thijs, J. T. (2011): Teacher wellbeing: The importance of teacher-student relationships. Educational Psychology Review, 23(4), 457-477.

Elimu ni moja ya vipengele muhimu katika maisha ya watu walio wengi katika taifa na hivyo misingi mizuri ya sera inahitajika.[49] Maeneo yanayoweka misingi mizuri katika sera ni pamoja na mitaala ya kufundishia, walimu, na maeneo yanayoleta mabadiliko katika sekta ya elimu. Ni muhimu kutambua kwamba elimu ya umma kupitia skuli za Serikali inajumuisha idadi ya wanafunzi wengi hivyo, sera na mikakati inaweza kuwekwa ili kuhakikisha kuwa kuna uimarishaji wa elimu katika nchi.

Serikali ina jukumu kubwa la kutekeleza na kuhakikisha kuwa uimarishaji wa elimu unafanyika katika mtazamo juu ya elimu, kuinua matarajio ya elimu, na kuimarisha dhamira ya Serikali katika utoaji wa elimu.

Eneo jengine la Kisera ni ugatuzi ikimaanisha ushirikishwaji wa ngazi za Wilaya na mikoa kushiriki kwa kiasi fulani katika usimamizi na uendelezaji wa elimu, kama vile viongozi wa kitaifa na wilaya kufanya kazi kwa pamoja na kamati zinazosimamia skuli, katika utoaji wa ruzuku na huduma nyengine ili kuhakikisha maendeleo ya elimu katika ngazi hizo.

Aidha, suala jengine muhimu la kisera ni upatikanaji wa rasilimali ili kuimarisha maendeleo ya skuli. Skuli nyingi katika taasisi za elimu ya umma, zinafanya vibaya katika mitihani kwa sababu ya upungufu wa rasilimali, uhaba wa madarasa na nyenzo za kufundishia ambazo ni muhimu katika kuhakikisha wanafunzi wanafanya vizuri.[50]

---

[49] Opper, I. (2019): Teachers Matter: Understanding Teachers' Impact on Student Learning. Santa Monica, CA: Rand Corporation.

[50] Prodhan, M. (2016): The educational system in Bangladesh and scope for improvement. Journal of International Social Issues, 4(1), 11-23

Pia, sera za elimu zinahitaji kuakisi Mipango ya Serikali na Maendeleo ya Elimu ya Msingi ambayo ni muhimu ili kuhakikisha watoto wengi wanajiunga na skuli. Mahudhurio bora ya wanafunzi katika skuli, ni njia mojawapo ya kuboresha elimu na hivyo kuhalalisha uwekezaji wa fedha katika programu za elimu.[51] Utekelezaji wa sera hii huongeza kiwango cha kujua kusoma na kuandika, kulazimisha watoto wote kuhudhuria skuli na kuongeza elimu katika taifa.

## 2.10 Mfumo wa elimu

Elimu ya sasa ina tofauti kubwa na elimu iliyokuwa ikitolewa zamani; jukumu kubwa la kufundisha na kukuza vijana ulimwenguni linabadilika.[52] Lengo kuu la elimu ya kisasa ni kukuza ustadi na maarifa ya kupata fedha. Wamiliki wa skuli mara nyingi hupima mafanikio kwenye ukuaji wa mapato au fedha badala ya thamani kwa wanafunzi.[53]

Aidha, mfumo wa elimu wa kufundishia na kujifunza uliopo Zanzibar unaonesha kuwa hautoshelezi na hausaidii kwa mahitaji ya kujifunza kwa karne ya 21.[54] Mamlaka za Serikali lazima ziwajibike na kuchukua hatua za kufanya mabadiliko muhimu katika mfumo wa elimu ili kuendana na wakati.[55]

---

[51] Letseka, M. M. (2013): Understanding of African Philosophy through Philosophy for Children (P4C). Mediterranean Journal of Social Sciences, 4(14), 745-753

[52] Carneiro, R. (2007): The big picture: understanding learning and meta-learning challenges. European Journal of Education, 42(2), 151-172.

[53] Sun, J., Anderson, R., Lin, T. & Morris, J. (2015): Social and cognitive development during collaborative reasoning. In C. S. Asterhan, S. N. Clarke & L. B. Resnick (Eds.) Socializing intelligence through academic talk and dialogue (pp. 63-76). Washington, DC: American Educational Research Association.

[54] Mulford, B., Kendall, D., Ewington, J., Edmunds, B., Kendall, L. & Silins, H. (2008): Successful principalship of high-performance schools in high-poverty communities. Journal of Educational Administration, 46(4), 461-480.

[55] UNESCO (2015): Rethinking Education: Towards a global common good? Paris: UNESCO. Witherspoon,

Mabadiliko hayo yanaweza kujumuisha suala la mitaala inayotayarishwa kuhakikisha kuwa inawapa wanafunzi maarifa sahihi na utaalamu.[56]

## 2.11 Watoto wenye mahitaji maalum /elimu mjumuisho

Watoto wenye ulemavu (CWDs) ni mojawapo ya makundi yaliyo hatarini zaidi katika jamii na maendeleo ya elimu. Asilimia kubwa ya watoto wenye ulemavu duniani wanaishi katika nchi zinazoendelea.[57]
Utafiti wa Benki ya Dunia wa 2017 ulibaini kuwa pengo la kusoma na kuandika kati ya CWDs na wenzao wasio na ulemavu imekuwa ikiongezeka zaidi ya miongo mitatu iliyopita. Hii ni kutokana na sababu kadhaa ikiwa ni pamoja na kutengwa, kubaguliwa, pamoja na mtazamo hasi wa kitamaduni uliopo kuhusu ulemavu.[58]

Watoto wenye ulemavu wanakabiliwa na ubaguzi hata ndani ya familia na wakati mwengine hutengwa na mwingiliano wa familia na huwekwa mbali kwa sababu ya kuogopa unyanyapaa unaofanywa na jamii.[59]

Taasisi nyingi za elimu ya umma hazijaweka mazingira ya kuwasaidia watoto wenye mahitaji maalum na majengo mengi ya skuli yanajengwa kwa namna

[56] Serdyukov, P. (2017): Innovation in education: what works, what doesn't, and what to do about it? Journal of Research in Innovative Teaching & Learning, 10(1), 4-33.
[57] Obraori Nmabunwa Peters Adiela & Chinuru Achinewhu Safeguarding the Future and Right to Education of Children with Disabilities in Nigeria, in New Challenges to Education: Lessons from Around the World BCES Conference Books, 2021, Volume 19. Sofia: Bulgarian Comparative Education Society ISSN 2534-8426 (online), ISBN 978-619-7326-11-6 (online), p. 231-237
[58] UNICEF (2007): Promoting the Rights of Children with Disabilities. Innocenti Digest No 13. Florence, Italy: UNICEF Innocenti Research Centre.
[59] Boezaart, T. (2012): A Constitutional Perspective on the Rights of Children with Disabilities in an Educational Context. South African Journal of Public Law, 27, 465-472.

ambayo watoto wenye ulemavu wa kimwili wanakuwa tegemezi kwa wengine.[60]

Lengo la kuelimisha watoto wenye ulemavu ni sawa na lile la kuelimisha watoto wasio na ulemavu: kusaidia watoto kufikia uwezo wao kamili na kuishi maisha yenye tija kama wanajamii hai.[61] Watoto wenye ulemavu mara nyingi huhitaji huduma maalum na usaidizi ili kufahamu maudhui yanayofundishwa.[62]

Elimu mjumuisho inaweza kuwepo tu kwa msaada mkubwa kutoka kwa Serikali na sheria mahsusi. Kwa bahati nzuri, uelewa wa jumla kwamba watoto wenye ulemavu wana haki ya kupata elimu unakua.[63] Nchi nyingi kwa sasa zina sheria au kanuni mahsusi ili kuhakikisha kuwa watoto wenye ulemavu wana fursa sawa za kupata elimu.[64]

Suala jengine ni ukosefu wa walimu waliofunzwa kufanya kazi na CWDs. Kuna upungufu wa walimu wa watoto wenye mahitaji maalum na hivyo walimu wasio na utaalamu wa kufundisha watoto hao wanashindwa jinsi ya kuwashughulikia watoto hao.[65]

---

[60] Giangreco, M. F., Broer, S. M., & Edelman, S. W. (2001). Teacher engagement with students with disabilities: Differences between paraprofessional service delivery models. Research and Practice for Persons with Severe Disabilities, 26(2), 75–86.

[61] Moberg, G. (2000). *Development of teacher perceptions of inclusive education in Finland*. Paper presented at the 11th International Association for Scientific Study of Intellectual Deficiency, World Congress, Seattle, WA.

[62] International Disability and Development Consortium. (2013). *Teachers for all: Inclusive education for children with disabilities.*,

[63] Falvey, M. A. (2004). Toward realizing the influence of "Toward realization of the least restrictive educational environments for severely handicapped students.". Research and Practice for Persons with Severe Disabilities, 29(1), 9–10.

[64] Labon, D. (1999). Inclusion education at work: Students with disabilities in mainstream schools. Washington, DC: Organisation for Economic Co-operation and Development

[65] Giangreco, M. F., Broer, S. M., & Edelman, S. W. (2001). Teacher engagement with students with disabilities: Differences between paraprofessional service delivery models. Research and Practice for Persons with Severe Disabilities, 26(2), 75–86.

## 2.12 Tabia za kitaaluma za mwalimu

Sifa za mwalimu zinaweza kuzuia maendeleo ya wanafunzi au kuwakuza wanafunzi wanaofundishwa. Mara nyingi, mwalimu ambaye hana sifa zinazotakiwa anaweza kuwa na changamoto za ufundishaji.

Mwalimu anahitaji kupata taaluma zaidi ili kumuwezesha kuwa na ufanisi zaidi katika utekelezaji wa kazi yake. Mwalimu lazima awe na utaalamu mkubwa katika mada yoyote anayotaka kufundisha na anapaswa kusoma kwa upana juu ya mada ili kuhakikisha ana uelewa mzuri.[66]

Eneo la taaluma kwa walimu likisimamiwa vyema litaongeza thamani katika mfumo wa elimu na kuleta tija kwa wadau wote; wanafunzi, walimu, wazazi, wasimamizi na wengine. Walimu watakaposimamiwa watasaidia wanafunzi kushiriki ipasavyo katika mitaala ili kutambua uwezo na vipaji vyao na kuwasaidia wanafunzi kuondoa vikwazo vinavyoweza kuzuia kujifunza.[67]

# SURA YA TATU

## 4.0 SERA, MIPANGO YA KITAIFA NA SHERIA MBALI MBALI

## 4.1 Utangulizi

[66] Russell, T. & Munby, H. (1992). Teachers and Teaching from Classroom to Reflection. London: Falmer Press.
[67] Bigge, M.L. & Shermis, S.S. (1992). Learning Theories for Teachers. (5th ed.). New York: Harper Collins Publishers.

Sura hii inaeleza kuhusu mfumo wa sera, sheria na mipango mikuu ya nchi inayohusiana na eneo la elimu ambalo linafanyiwa utafiti. Sera mbali mbali zimefafanuliwa katika Sura, hii ikiwemo Sera ya Elimu. Aidha, Sheria mbali mbali zenye mnasaba na masuala ya elimu pamoja na baadhi ya mipango mikuu ya nchi inayoakisi suala la elimu nayo inafafanuliwa katika Sura hii. Maeneo hayo yanafafanuliwa  kama ifuatavyo:

## 4.2 Mipango Mikuu

### 3.2.1 ILANI ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025

Ilani ya CCM imeeleza azma ya kuisimamia Serikali katika sekta ya elimu nchini kwa kuweka mikakati mbali mbali ya kuleta maendeleo katika sekta hiyo muhimu kwa ajili ya maendeleo ya nchi. Miongoni mwa mambo ya msingi ya kusaidia katika maendeleo ya sekta ya elimu ni pamoja na kupitia upya mfumo wa elimu ya ufundi na amali ili uweze kusajili vijana wengi zaidi na kuzalisha wataalam mahiri wa ngazi ya msingi na ya kati wenye ujuzi katika fani zao na uwezo wa kujiajiri na kuajirika mahali popote duniani.[68]

Aidha, Ilani hii imebainisha mkakati wa usimamiaji na utekelezaji Sera ya Elimu juu ya makuzi na malezi kwa watoto ambao wamefika umri wa kuanza skuli kwa ajili ya maandalizi. Ilani pia inahamasisha wananchi kushiriki katika maendeleo ya elimu ya maandalizi kwa skuli za ndani na za nje ya nchi katika kuwajenga wanafunzi ili kupata elimu bora.[69]

[68] Ibara ya 136D ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025 iliyojumuisha suala la mfumo wa elimu ya ufundi kama sehemu ya vipaumbele vilivyowekwa katika Ilani hiyo katika kipindi cha miaka mitano ijayo ya utekelezaji wa Ilani.

[69] Ilani ya chama cha Mapinduzi 2020-2025 ibara ya 182

Kwa upande mwengine, Ilani imeitaka Serikali kuweka mkakati wa kuimarisha programu za mafunzo ya amali zinazoendana na mahitaji ya soko la ajira ili kupunguza tatizo la ajira na umasikini kwa ujumla.[70] Masharti haya yanatokana na kutambua umuhimu uliopo katika sekta ya elimu hasa katika elimu ya mafunzo ya amali itakayowatayarisha vizuri wanafunzi hao.

Ilani kwa upande wa skuli za msingi, imeeleza kuwa Serikali itaimarisha ubora wa elimu kwa kufanya mageuzi kwenye mitaala ya elimu pamoja na utekelezaji wake katika kuinua kiwango cha ufundishaji.[71] Ilani imetambua umuhimu wa kufanya mapitio ya mitaala ya elimu katika ngazi mbali mbali ikiwemo ngazi ya elimu ya mafunzo ya amali.

Kwa upande wa skuli za Sekondari, ilani imeelekeza Serikali kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika masomo kwa vitendo, kushirikiana na sekta binafsi katika kutoa huduma bora za elimu kwa madarasa yote, pamoja na kuimarisha matumizi ya Teknojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kujifunza na kusomeshea masomo mbalimbali kwa njia ya kielektroniki.[72]

### 3.2.2 Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050

Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050 imezingatia sekta mbali mbali za maendeleo ikiwemo sekta ya elimu katika kuweka mipango itakayowezesha Zanzibar kupiga hatua kubwa za maendeleo ifikapo mwaka 2050. Mipango hiyo inajumuisha mikakati ya kuhakikisha kuwa Zanzibar inapiga hatua za

[70] Ibid, Ibara ya 182
[71] Ibara ya 182(e)
[72] Ibid

kimaendeleo katika kipindi hicho cha Dira. Sehemu hii inafafanua maeneo yaliyobainishwa katika Dira hiyo ya Maendeleo yanayohusiana na sekta ya elimu kama ifuatavyo:

**(a) Mchango wa Sekta ya Elimu katika Maendeleo ya nchi**

Dira ya Maendeleo ya 2050 imetambua mchango wa sekta ya elimu katika kipindi cha miaka 20 iliyopita, wakati ikichambua utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2020. Maendeleo hayo yanagusa sehemu mbali mbali ikiwa ni pamoja na mafunzo ya walimu, ujenzi wa skuli za kisasa, uboreshaji wa uandikishaji wa wanafunzi wapya, hasa katika ngazi ya maandalizi, msingi na sekondari na kuanzishwa kwa taasisi mpya za elimu ya juu.[73]

**(b) Changamoto za mfumo wa Elimu**

Dira ya Maendeleo ya 2050 pia imetambua changamoto mbali mbali katika mfumo wa elimu ambazo zinaathiri ufikiwaji wa maendeleo. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na elimu ya maandalizi na msingi kutowezesha upatikanaji wa maarifa ya kielimu kwa wanafunzi wa ngazi hizo.[74]

Aidha, Dira imeeleza kuwa kwa upande wa ngazi ya sekondari, elimu inayotolewa haitoi stadi zinazowezesha wanafunzi kuwa na uwezo wa uchambuzi wa fikra (critical thinking), ubunifu (creativity and innovations) na stadi zinazohitajika katika soko la ajira.[75]

[73] 29 Ukurasa wa Dira ya 2050
[74] Dira ya Maendeleo ya 2050, sehemu ya Usuli (Background) iliyopo ukurasa wa 29.
[75] Ibid.

Dira pia imeeleza changamoto nyengine ikiwemo ya elimu inayotolewa katika vituo vya amali kulenga zaidi wanafunzi walioshindwa kuendelea na masomo na hivyo kupoteza mwelekeo wa Serikali wa kuwa na nguvu kazi yenye uwezo mkubwa pamoja na changamoto ya kukosa miundombinu bora kama maabara, maktaba, vifaa vya TEHAMA na madarasa ya kutosha.[76]

**(c ) Matarajio ya Dira katika Sekta ya Elimu**

Katika kuimarisha sekta ya elimu ili ichangie kikamilifu katika maendeleo ya nchi, Dira imeweka matarajio yafuatayo:

(a) Kuwa na mfumo imara wa upatikanaji wa walimu ili kuimarisha ubora wa elimu;[77]

(b) Kuwa na mitaala ya elimu itakayotoa stadi zinazowezesha wanafunzi kuwa na uwezo wa uchambuzi wa fikra (critical thinking), ubunifu (creativity and innovations) na stadi zinazohitajika katika soko la ajira;[78]

(c) Kuwa na mfumo wa elimu utakaojumuisha elimu ya dini na kujumuisha madrasa;[79]

(d) Kuwa na mitaala ya elimu itakayojumuisha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika ngazi zote za elimu ili wanafunzi wajifunze toka ngazi za awali;[80]

---

[76] Ibid.
[77] Dira ya Maendeleo ya 2050 katika Ibara ya 2.1.2
[78] Dira ya Maendeleo ya 2050 katika Ibara ya 2.1.3
[79] Ibara ya 2.1.4
[80] Ibara ya 1.6.5

(e) Utoaji wa elimu katika fani mbali mbali ili kusaidia maendeleo ya fani hizo, zikiwemo fani za utalii[81] na viwanda.[82]

## 4.3 Sera zinazohusiana na masuala ya elimu

Sehemu hii inafafanua na sera mbali mbali zenye mnasaba ya elimu nchini. Sera hizo zinafafanuliwa kama ifuatavyo:

### 3.3.1 Sera ya Elimu ya Mwaka 2006

Sera inayosimamia masuala ya elimu Zanzibar ilitungwa mwaka 2006 na inajulikana kama Sera ya Elimu Zanzibar ya mwaka 2006. Sera hii ina lengo la kuweka mazingira bora ya elimu ambayo yatakidhi haja ya kuwa na mfumo shirikishi utakaowaunganisha wadau wote wa sekta ya elimu kuwa kitu kimoja na hivyo kupelekea jitihada za maendeleo ya elimu kuratibiwa ili kuhakikisha mafanikio ya malengo na maazimio katika elimu yanafikiwa. Sera hii imeanisha maeneo mbali mbali yanayolenga kuimarisha sekta ya elimu nchini kama yanavyofafanuliwa kama ifuatavyo:

#### (a) Malengo ya Elimu

Sera ya Elimu imeweka malengo mbali mbali yanayoazimiwa kufikiwa katika sekta ya elimu nchini. Malengo hayo yanajumuisha upanuzi wa fursa ya elimu ya lazima kwa miaka kumi na mbili kwa wanafunzi wote kuanzia elimu ya maandalizi mpaka kufikia kiwango cha kidato cha nne.[83]

[81] Ibara ya 1.3.4
[82] Dira ya Maendeleo ya 2050 katika Ibara ya 1.2.5
[83] Sera ya Elimu Zanzibar ya mwaka 2006, Ibara ya 2.3

Aidha, ibara hiyo ya Sera pia imefafanua malengo mengine ya elimu kama kurahisisha upatikanaji wa elimu endelevu kupitia mfumo wa elimu ya jadi au kwa njia ya mafunzo ya stadi za kazi; kutoa fursa sawa ya elimu kwa makundi maalumu kama vile watu wenye mahitaji maalumu; na kukuza ubora na ufanisi wa mfumo wa elimu. Malengo mengine ni  kuongeza ubora wa elimu kwa wanafunzi ili waweze kukuza ujuzi wao wenyewe na kutambua uwezo wao kama raia; kuboresha elimu na mafunzo kwa walimu ili ujuzi na maarifa yaendane na mabadiliko na matarajio ya jamii na kukidhi mahitaji ya wanafunzi; kuwapatia wanafunzi ujuzi unaohitajika kwa ajili ya maisha yao. kuhakikisha upatikanaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa walimu, wanafunzi na wafanyakazi wa elimu; kuimarisha elimu ya juu; na kuimarisha ushirikiano wa sekta za umma na sekta binafsi.

Kiujumla malengo haya yote yanakusudia kuimarisha mfumo wa elimu nchini kwa kuweka misingi imara ya elimu na kuifanya elimu inayotolewa Zanzibar kushirikisha wananchi wote na kuifanya elimu hiyo kuleta matokeo na hivyo kusaidia katika maendeleo ya nchi.

### (b) Upatikanaji wa Elimu kwa Usawa

Sera hii ya Elimu ya mwaka 2006 imeweka Sura mahsusi inayozungumzia upatikanaji wa elimu katika ngazi ya maandalizi, msingi, sekondari, elimu ya juu, elimu kwa watu wenye mahitaji maalum, elimu mbadala, elimu ya watu wazima, elimu ya ufundi stadi na maeneo mengine ya elimu kwa usawa, na kubainisha mikakati ya kufikia azma hiyo.[84] Miongoni mwa mikakati ya kufanikisha azma hiyo ya kuleta ufanisi katika ngazi hizo za elimu ni kuimarisha

[84] Sura ya Nne ya Sera ya Elimu yam waka 2006, ukurasa wa 8-25.

ushirikiano baina ya taasisi za umma, jumuiya zisizo za kiserikali, kamati za skuli, taasisi binafsi na jamii kwa ujumla, kuhamisha uwekezaji wa skuli binafsi, na utoaji wa mafunzo kwa walimu. Mikakati mengine ni kuimarisha bajeti ya masuala ya elimu, kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano na kutambua na kuimarisha huduma za elimu kwa watu wenye ulemavu.

### (c) Ubora wa Elimu

Sera pia imeainisha Sura inayohusu masuala ya ubora wa Elimu nchini kwa kuweka mikakati mbali mbali ya kufikia ubora wa elimu katika skuli za Serikali na skuli binafsi.[85] Mikakati kadhaa imewekwa katika kuhakikisha ubora wa elimu na mikakati hiyo inajumuisha uimarishaji wa maabara na maktaba katika skuli mbali mbali, uendelezaji na upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na matumizi ya Teknolojia ya habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika sekta ya elimu.

### (d) Walimu na kazi ya ualimu

Sura ya sita ya Sera ya Elimu ya mwaka 2006 inaeleza kuwa walimu wanastahili kupewa hadhi na kipaumbele zaidi katika kunyanyua ubora wa elimu katika skuli au katika programu mbalimbali zinazohusiana na jamii.[86] Pia Sera inatilia mkazo kuheshimiwa kwa walimu katika Nyanja zote, kupewa stahiki za kutosha, kupewa fursa za mafunzo, vituo vya mafuzo vya walimu ili kuwezesha kupatikana walimu wenye sifa na kupelekea kupatikana kwa mafaniko ya elimu.[87]

---

[85] Sera ya Elimu ya mwaka 2006, Sura ya Tano, ukurasa wa 26-38
[86] Ibid Ukurasa 39
[87] Ibid.

### 3.3.2 Sera ya Afya na Usalama Kazini Zanzibar ya Mwaka 2016

Sera ya Usalama na Afya Kazini Zanzibar ya mwaka 2016 nayo imegusa maeneo yenye mnasaba na suala la sekta ya elimu nchini. Sera hiyo inajumuisha mikakati ya utekelezaji inayoweka uhusiano na Sera ya Elimu ya mwaka 2006. Miongoni mwa mikakati hiyo iliyofafanuliwa katika Sera hiyo ya Afya na Usalama Kazini ni pamoja na uundaji wa mitaala ya elimu ya usalama na afya kazini ambayo itatumika kukuza usalama na utamaduni wa kiafya katika maeneo ya kazi zikiwemo skuli na katika utoaji wa mafunzo kwenye vyuo vikuu viliopo nchini.[88]

### 3.3.3 Sera ya Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2018

Sera ya Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2018 nayo imetambua umuhimu wa suala la elimu na hivyo kujumuisha maeneo yanayohusu sekta hiyo ya elimu kwenye Sera hiyo. Sera ya Watu wenye Ulemavu imesisitiza kuwa elimu itolewe pamoja na mafunzo ya kiufundi na amali kwa watu wenye ulemavu kwa ajili ya kuhakikisha wanajiajiri wenyewe na wanajitegemea.[89] Pia, Sera hiyo imeeleza tatizo kuu katika elimu na maendeleo ya kiujuzi kwa watu wenye ulemavu ni uhaba wa skuli za elimu mjumuisho, hali inayopelekea watoto wenye ulemavu hasa wale wasioona na wenye uziwi kukosa mazingira bora ya kujifunzia.[90]

Suala jengine muhimu lililoelezwa katika Sera hiyo ni uwepo wa elimu mjumuisho ambayo haijafikia viwango vinavyokubalika katika skuli nyingi

[88] Sera ya Afya na Usalama Kazini, ukurasa 5
[89] Sera ya watu wenye ulemavu, ukurasa wa 11
[90] ibid

ambazo zina huduma hizi, hasa kwa watoto wenye ulemavu wa viungo.[91] Kwa mantiki hiyo, Sera imetambua kuwa skuli hizo zenye huduma za elimu mjumuisho, hazitoi elimu hiyo mjumuisho kama inavyohitajika na hivyo kuathiri taaluma hiyo kwa watu wenye ulemavu.

### 3.3.4 Sera ya Uhakika wa Chakula na Lishe Zanzibar ya Mwaka 2008

Sera hii imeelaza baadhi ya vyanzo vinavyopelekea kutokuwepo kwa Usalama wa chakula na utapiamlo kwa wananchi katika ngazi ya familia na kutambua suala la viwango vidogo vya elimu kama miongoni mwa vyanzo hivyo. Pamoja na Sera kutoeleza aina ya elimu iliyokusudiwa, elimu hiyo inaweza kujumuisha elimu ya kilimo katika ngazi mbali mbali na hivyo wananchi kushindwa kulima kitaalamu ili kupata tija katika kilimo na kuzalisha kwa wingi na kuimarisha usalama wa chakula.

Elimu imetambuliwa kuwa na mchango mkubwa katika kufikia hali ya usalama wa chakula kwa kuweka miongozo ya utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya amali itakayosaidia kuondoa tatizo la ukosefu wa usalama wa chakula nchini pamoja na ukosefu wa lishe.

Aidha, Sera hiyo imeweka mkakati ya kisera (*Policy Strategies*) mbali mbali ili kufikia malengo ya sera na miongoni mwa mikakati hiyo ni pamoja na kuhakikisha kunakuwepo na utoaji thabiti wa elimu ya afya na elimu ya lishe. Ibara ya 3.2 ya sera hii imeweka jukumu kwa Wizara zilizotambuliwa kuwa na mchango mkubwa katika kufikia lengo hilo ni Wizara ya elimu.[92]

[91] Ibid Ukurusa wa 12

[92] Sehemu ya tano ya Sera imejumuisha mazingira mazuri ya utekelezaji wa Sera kuanzia ukurasa wa 36 mpaka ukurasa wa 40 .

## 4.4 Sheria zinazohusiana na Elimu

### 3.4.1 Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984

Katiba ni nyenzo muhimu inayoongoza sheria za nchi husika na imekuwa ikitambuliwa kama sheria mama inayotoa misingi na miongozo ya nchi. Katiba ya Zanzibar ya 1984 katika kuweka malengo ya kisiasa ya nchi, imeweka wajibu kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha kuwa kunakuwepo na fursa sawa katika kupata elimu kwa viwango vyote vya elimu. [93] Msingi huu uliowekwa na kifungu hicho cha 10 cha Katiba, unatoa uhakika wa kila mtu ndani ya Zanzibar kupata fursa ya elimu katika ngazi yoyote, bila ya kubaguliwa kwa namna yoyote.

Aidha, kifungu hicho cha Katiba kinasisitiza Serikali kuhakikisha kuwa kunakuwa na fursa za kutosha na hivyo kuwawezesha watu wote kupata nafasi ya kupata elimu. Misingi ya kisheria inahitaji utungaji wa sheria, kanuni au miongozo yoyote itakayotungwa au kutolewa katika eneo hilo la elimu, kuzingatia masharti ya kifungu hicho cha 10 cha Katiba.

### 3.4.2 Sheria ya Elimu Nam. 6 ya Mwaka 1982

Sheria ya Elimu Nam. 6 ya mwaka 1982 ambayo ilifanyiwa marekebisho makubwa mwaka 1993 kupitia Sheria Nam. 4 ya mwaka 1993, ilitungwa kwa lengo la kuweka utaratibu mzuri wa usimamizi wa elimu kwa ajili ya maendeleo ya sekta hiyo ya elimu nchini. Sheria hii ya Elimu iliifuta Sheria iliyokuwepo awali iliyotambulika kama Sheria ya Elimu, Sura ya 9 ya mwaka 1959 (The Education Decree, 9/1959). Katika kufikia lengo la kuleta maendeleo ya sekta ya elimu nchini, Sheria hii ya Elimu imeweka masharti mbali mbali ya kisheria

[93] Katiba ya Zanzibar kifungu cha 10(f)

katika maeneo mbali mbali. Baadhi ya masharti hayo yanafafanuliwa kama ifuatavyo:

**(a) Uanzishwaji wa skuli**

Sheria imeweka wazi kwamba Waziri kupitia Baraza la Elimu atathibitisha uanzishwaji wa skuli kwa masharti kwamba skuli inayotaka kuanzishwa ni skuli ya umma; skuli ya binafsi ambayo wamiliki wake wamemridhisha Waziri kwamba wao ndio wamiliki halali wa skuli hiyo na kwamba hawataendesha skuli kwa misingi ya rangi, dini, hadhi ya kijamii, kipato, ulemavu au misingi yoyote ya kibaguzi; au Skuli inayopata msaada wa umma.[94] Aidha Sheria hii imeanzisha masomo ya ziada kwa lengo la kukuza elimu na elimu hiyo ya ziada itasimamiwa chini ya programu ya elimu ya watu wazima.[95]

**(b) Usajili wa skuli**

Sheria ya Elimu imeweka masharti kuhusu taratibu za kuzisajili skuli mbali mbali za Zanzibar. Kwa mujibu wa Sheria hii, Skuli zote zitasajiliwa na Baraza la Elimu kwa mfumo ambao Baraza hilo litaona unafaa na kuweka rejista ya skuli zote na usajili huo utaambatana na cheti ambacho kitaonesha umiliki wa skuli hiyo.[96] Aidha, kifungu cha 14 cha Sheria hii kimeweka wazi kwamba ni kosa kuanzisha skuli bila ya kuwa na cheti cha usajili kilichotolewa na Baraza la Elimu na mtu yeyote atakayeshindwa kutimiza masharti ya kusajili skuli kama iliyoelezwa kwa mujibu wa kifungu cha 13, atakua amefanya makosa na akitiwa hatiani atalazimika kulipa faini isiyopungua Shilingi Elfu hamsini au kupelekwa chuo cha mafunzo.

[94] Sheria ya Elimu Nam. 6 ya Mwaka 1982, kifungu cha 10 na cha 11
[95] Ibid, kifungu cha 12
[96] Ibid kifungu cha 13

### (c) Usimamizi wa skuli

Sheria hii kwa upande wa usimamizi wa skuli za umma, imeweka mamlaka kwa Waziri anayehusika na masuala ya elimu, kuweka utaratibu wa kutambua aina mbalimbali za skuli kulingana na asili au namna au viwango vya elimu vinavyotolewa; na madarasa, viwango au mifumo tofauti ndani ya skuli kulingana na asili ya elimu inayotolewa katika skuli hizo.[97] Sheria imempa jukumu Katibu Mkuu wa wizara inayohusika na elimu la usimamizi wa skuli za Serikali. Kwa upande wa skuli binafsi skuli za Kidini na Skuli zinazopokea msaada wa Serikali, Mratibu Mkuu ambae atateuliwa na Waziri, ataratibu na kufuatilia shughuli za skuli hizo.[98]

### (d) Uandikishwaji wa wanafunzi

Sheria imeweka wazi kuwa ni lazima watoto wote waliotimiza umri wa miaka saba na ambao bado hajapindukia umri wa miaka kumi na tatu, waandikishwe skuli ya msingi wakitimiza umri wa miaka saba[99] Aidha, Sheria hii imewapa jukumu wazazi na walezi kuhakikisha mtoto huyo anahudhuria skuli mpaka atakapokamilisha elimu ya lazima ambayo kwa mujibu wa Sera ni kidato cha nne au kutimiza umri wa miaka kumi na nane.[100]

Sheria hii katika kifungu cha 22 imewataka wazazi kutoa taarifa kwa Afisa Elimu wa Mkoa pindi watoto wao wanapofikia umri wa kwenda skuli pamoja

[97] Ibid kifungu cha 17
[98] Ibid kifungu cha 18 na cha 18A
[99] Ibid,kifungu cha 19
[100] Ibid, kifungu cha 20

na kuwasilisha majina kamili ya watoto; tarehe ya kuzaliwa na utaifa wa mtoto; na jina la skuli ya karibu na maazi yake anayotaka mtoto wake aandikishwe.

### (e) Uanzishwaji wa kamati

Sheria hii pia imeanzisha kamati katika kila skuli ya umma ambazo zitaundwa na Mwenyekiti ambaye atachaguliwa na Mkuu wa Wilaya.[101] Aidha, Sheria imeweka Mjumbe mmoja kutoka kila Serikali ya Mitaa, ambayo skuli ipo atakayeteuliwa na Serikali ya mtaa husika.[102]

Pia, sheria imempa nafasi Sheha kuchagua mjumbe mmoja kutoka katika shehia ambapo skuli ipo, na wajumbe wengine wasiozidi wawili ambao watachaguliwa na Afisa Elimu Wilaya.[103] Sheria chini ya kifungu cha 24 (1) (e) imemtaja Mwalimu Mkuu wa skuli husika kuwa katibu wa kamati. Kamati hiyo pia itakuwa na watu wengine wasiozidi watatu ambao watachaguliwa na wazazi, na mkuu wa serikali ya wanafunzi ikiwa atakua ameshafika elimu ya sekondari.[104]

### (f) Bodi ya skuli ya Wilaya

Sheria imeanzisha bodi za skuli za Wilaya ambazo zitaundwa na mwenyekiti ambaye atakua ni mtu anayekubalika na ambaye si mfanyakazi wa wizara ya elimu au taasisi zilizo chini ya Wizara hii ambaye anateuliwa na Waziri.

---

[101] Ibid, kifungu cha 24
[102] Ibid
[103] ibid
[104] Ibid, kifungu cha 24

Pia, Sheria imetambua nafasi ya Katibu wa Bodi ambaye ni Afisa Elimu wa Wilaya. Bodi pia inajumuisha mjumbe aliyeteuliwa na Mkuu wa Wilaya kutoka afisi ya mkuu wa wilaya; wajumbe wasiozidi watano kutoka katika vikundi mbalimbali kama vile wazazi, vijana; wanawake na wanafunzi kama Mkuu wa Wilaya anavyoona inafaa ambao wanateuliwa na Mkuu wa Wilaya; Maafisa wasiozidi watatu kutoka Wizara inayohusika na elimu watakaoteuliwa na Waziri; wazee wasiozidi watatu ambao wanakubalika na kuheshimika na wananchi katika Wilaya na ambao watateuliwa na Waziri kwa kushauriana na Bodi ya Elimu.

Kazi za Bodi hii zimeelezwa katika Vifungu vya 25 na 27 vya Sheria hii na kujumuisha kusimamia skuli zote katika Wilaya hiyo na kufanya kazi kama bodi ya rufaa kwa malalamiko kutoka kwa bodi za skuli za umma na za binafsi zilizo ndani ya mamlaka yake kwa masuala yanayohusiana na elimu.

**(g) Bodi ya Skuli ya Mkoa**

Sheria imeanzisha bodi za skuli za mkoa katika kila mkoa. Bodi hizo zinaundwa na Mwenyekiti ambaye atakua ni mtu anayeheshimika katika eneo hilo na hatokuwa mjumbe kutoka wizara ya elimu au kutoka taasisi nyegine zilizo chini ya Wizara ya za elimu. Aidha, Kifungu hicho kimetambua nafasi ya Katibu wa bodi ambaye atakua ni Afisa elimu wa Mkoa.[105]

Vile vile, Sheria imeweka mjumbe mmoja atakayetuliwa na Mkuu wa Mkoa kutoka katika Ofisi yake na wajumbe wasiozidi watano kutoka katika makundi

[105] Ibid, kifungu cha 26

yenye maslahi kama vile wazazi, vijana, wanawake na wanafunzi kama Mkuu wa Mkoa atakavyoona inafaa ambao pia watateuliwa na Mkuu wa Mkoa; watumishi wasiozidi watatu kutoka Wizara inayohusika na elimu watakaoteuliwa na Waziri wa Elimu; Wazee wasiozidi watatu wanaoheshimika na wananchi katika Mkoa huo na ambao watateuliwa na Waziri anayehusikana elimu kwa kushauriana na Bodi ya Elimu.[106]

Aidha, Sheria imeainisha kazi mbali mbali za bodi ya skuli ya Mkoa kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 29 ikiwemo Bodi ya rufaa kwa malalamiko kutoka Bodi ya skuli ya Wilaya ndani ya eneo hilo.

### 3.4.3 Sheria ya Kuwalinda Wari na Watoto wa Mzazi Mmoja Nam.4 ya Mwaka 2005.

Sheria hii ilitungwa kwa lengo la kufuta sheria ya kuwalinda wari, vizuka na wajane walioachwa ya mwaka 1985 na kutoa ulinzi kwa wari na watoto wa mzazi mmoja. Sheria imetoa tafsiri ya neno mwari ambaye ni mwanamke ambaye hajaolewa mwenye umri wa miaka baina ya miaka 18 na 21 na ambae hajawahi kuzaa. Vile vile imemtafsiri mwanafunzi kama mtu yeyote ikiwa mwanamke au mwanamme wa umri wowote ambae bado anasoma elimu yake ya msingi kama ilivyotafsiriwa katika sheria ya Elimu.[107] Sheria imetoa ulinzi na haki katika maeneo mbalimbali yakiwemo:

**(a) Kulindwa kwa haki ya kupata elimu**.

[106] Ibid, kifungu cha 28
[107] Ibid, kifungu cha 2

Sheria katika kifungu cha 4 inaeleza kwamba ikiwa mtoto wa kike atapata ujauzito akiwa bado anasoma, anatakiwa kusimamishwa masomo. Mtoto huyo atarejeshwa skuli mwaka unaofuata wa masomo baada ya kujifungua au muda wowote mamlaka za elimu zitakapoona inafaa.

Vilevile, Sheria imetoa fursa ya mwari kurejeshwa masomoni mwaka unaofuata baada ya kumaliza kutumikia adhabu yake ya kutumikia jamii au muda wowote mamlaka za elimu zitakapoona inafaa.[108] Sheria hii imefafanua wazi kwamba mwari atakaepata ujauzito kwa hiari yake atatakiwa kutumikia jamii kwa muda wa miezi sita baada ya kutimiza miezi mitatu ya kujifungua.

Aidha, Sheria imempa haki mwanafunzi wa kiume aliyekua chini ya umri wa miaka kumi na nane ambaye atasababisha ujauzito[109] kurudi skuli mwaka unaofata mara tu baada ya kutumikia adhabu yake na si zaidi ya miaka miwili.

### (b) Jukumu la kuhudumia mtoto

Sheria imeeleza kwamba aliyebainika au anayedaiwa kuwa ni baba wa mtoto ndiye mwenye jukumu la kumpatia mtoto huyo mahitaji yote ya msingi ikiwemo mavazi, chakula, afya, malazi na elimu kwa kutegemea uwezo wa baba huyo.[110] Sheria imeendelea kutoa maelezo juu ya elimu iliyokusudiwa kuwa ni elimu ya msingi iliyoelezwa kwenye sheria ya Elimu ya mwaka 1982 na vilevile kama uwezo wa baba unaruhusu, itajumuisha elimu ya juu.[111]

---

[108] Ibid, kifungu cha 4 (3)
[109] Ibid, kifungu cha 3(5)
[110] Ibid, kifungu cha 8(1)
[111] Ibid, kifungu cha 8(2)

### 3.4.4 Sheria ya Watoto Nam. 6 ya Mwaka 2011

Sheria hii imetungwa pamoja na mambo mengine, kuweka haki muhimu za watoto zinazotokana na mikataba ya kimataifa na kikanda iliyozingatia maslahi bora ya mtoto. Sheria katika kuzingatia maslahi bora ya mtoto imemuwekea mtoto mahitaji maalum ambayo kupatikana kwake kutapelekea kumkuza mtoto katika mazingira mazuri. Sheria katika kifungu cha 10 imetaja mahitaji muhimu kwa watoto ambapo miongoni mwa mahitaji hayo ni kupata elimu. Jukumu la kutoa mahitaji hayo muhimu limebakishwa kwa mzazi au mlezi wa mtoto au mtu mwengine anayeishi na mtoto kumhudumia mtoto huyo kulingana na uwezo wake.

Vile vile, sheria imewataja watoto wenye ulemavu kuwa wanastahili kupata kinga na fursa sawa na watoto wengine. Watoto hao wanatakiwa wapate mafunzo, elimu mjumuisho, huduma za afya, ajira na fursa za michezo.[112]Baadhi ya mambo muhimu yaliyomo katika sheria hii ni :

**(a) Dhamana na majukumu ya mzazi**

Kifungu cha 12 cha sheria hii pia kinaeleza kuwa wazazi wanatakiwa kuhakikisha watoto wao wanapata haki ya kuishi, heshima, uhuru, elimu na mengineyo yote ambayo ni muhimu kwa ukuaji wa mtoto kimwili, kiroho na kiakili**.** Sheria imeweka wazi kwamba ikiwa wazazi wa mtoto watatengana au kuachana, mtoto wao miongoni mwa haki zake ni kupata matunzo na elimu ya kiwango sawa na alichokuwa anapata kabla ya wazazi wake kutengana au kuachana.[113]

[112] Ibid, kifungu cha 11
[113] Ibid, kifungu cha 70

**(b) Kafala na kuasili**

Sheria hii imeruhusu kafalah (kumlea mtoto) ikizingatia kwamba majukumu yote ya mzazi yatahamishiwa kwa mtu aliyeomba ulezi wa mtoto husika. Sheria imeeleza kwamba mtu ambaye atakua ni mlezi katika kafalah atabeba majukumu yote ambayo mzazi anayo kwa mtoto wake. Majukumu hayo yakijumuisha malezi, matunzo ya mtoto, makaazi na kumpatia elimu mtoto huyo.[114]

Aidha, kwa upande wa kuasili, Sheria imeweka wazi kwamba miongoni mwa athari za kuasili mtoto ni kuwa mtu ambaye amemuasili mtoto atabeba dhima na majukumu yote ambayo mzazi halisi wa mtoto huyo alikua nayo. Majukumu na dhima ambazo atakuwa nazo mtu aliyemuasili mtoto chini ya Sheria hii zitajumuisha mtoto kupata huduma, malezi na kumpatia elimu kama kwamba mtoto huyo amezaliwa na mtu aliemuasili.[115]

**(c) Nyumba salama kwa watoto**

Sheria hii kwa madhumuni ya kulinda maslahi bora ya mtoto, imeanzisha makaazi salama kwa watoto. Aidha, Sheria imeweka masharti kwamba uanzishwaji wa makaazi hayo salama kwa watoto yataanzishwa pale tu Waziri atakapojiridhisha kwamba makaazi hayo yanaweza kusimamiwa vizuri na wapo wafanyakazi wa kutosha ambao wataweza kuwahudumia watoto kwa kuzingatia ukuaji mzuri wa watoto, furaha yao na maendeleo kwa ujumla hasa ya kielimu na kiafya.[116]

[114] Ibid, kifungu cha 75(2)(b)
[115] Ibid, kifungu cha 85(1)(b)
[116] Ibid, kifungu cha 123(5)

Pia, Sheria kwa kuzingatia ukuaji mzuri wa watoto katika nyumba hizo salama zilizoanzishwa, inaelekezwa kuanzishwa kamati itakayoundwa na wajumbe wasiopungua wanne.

**(d) Ajira kwa Watoto**

Kwa ujumla Sheria hii inakataza ajira kwa watoto ambazo zitawapelekea madhara ya kiafya, kielimu, kiakili au ukuaji.[117] Aidha Sheria imebainisha wazi kuwa mtoto mwenye umri wa kuanzia miaka kumi na tano anayo haki ya kufanya kazi kwa kuzingatia maslahi yake. Pia kazi hizo ziwe ni nyepesi (kazi ambazo hazimuathiri mtoto huyo kuhudhuria skuli, kushiriki katika mafunzo ya amali, kufanya kazi zake za skuli, kuzingatia maendeleo yake ya afya).[118]

### 3.4.5 Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar Nam. 3 ya Mwaka 2011.

Sheria hii imefuta Sheria ya Mfuko wa Elimu ya Juu Zanzibar Nam.6 ya mwaka 2001 na kuanzisha Sheria mpya ya bodi ya mikopo ya elimu ya juu Zanzibar ya Nam. 3 ya mwaka 2011 itakayosimamia masuala ya mikopo ya elimu ya juu Zanzibar. Katika kuhakikisha ustawi wa elimu kwa wazanzibari, Sheria hii imeanzisha Mfuko wa mikopo ya elimu ya juu,[119] na kuanzisha bodi maalum iitwayo Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar[120] ambayo itasimamia mfuko huo. Aidha, sheria pia imeanzisha Kamati ya Elimu ya Juu ambayo itaisaidia Bodi katika kutekeleza majukumu yake.[121]

---

[117] Ibid, kifungu cha 97
[118] Ibid, kifungu cha 98
[119] Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar, kifungu cha 17
[120] Ibid, kifungu cha 3
[121] Ibid, kifungu cha 11

Bodi hiyo imepewa majukumu ya kutoa mikopo kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wa kizanzibari kuweza kulipia ada za elimu ya juu kwa kiwango maalum na kwa kuzingatia utaratibu maalum ambao bodi utaona unafaa, na kuweka idadi ya wanafunzi wenye sifa ambao watapatiwa mkopo kwa kila mwaka, kuweka rejista na kuhifadhi kumbukumbu za mikopo ya wanafunzi na majina ya wanafunzi waliopewa mikopo.

Aidha, majukumu mengine ya Bodi hiyo ya mikopo ni kufuatilia wanafunzi waliopewa mikopo katika taasisi za elimu ya juu, kupokea zawadi na misaada ya kuwezesha Mfuko wa Bodi, kuhakikisha kuwa Mfuko unatumika kwa matumizi yaliyokusudiwa pamoja na kufanya tafiti, kutoa zawadi na kuwezesha udhamini wa nje na ndani ya Zanzibar kwa wanafunzi wa kizanzibari,[122]kwa kuzingatia sifa zilizowekwa.[123]

### 3.4.6 Sheria ya Baraza la Mitihani Zanzibar Nam. 6 ya Mwaka 2012.

Sheria hii ya Baraza la Mitihani Zanzibar, katika kuhakikisha ustawi wa elimu kwa wazanzibari, imeanzisha vyanzo maalum vya mapato kwa lengo la kutekeleza majukumu ya Baraza. Miongoni mwa vyanzo hivyo ni kiasi cha fedha kitakachopitishwa na Baraza la Wawakilishi, fedha au mali yoyote itakayotokana na vyanzo vyengine kama vile, zawadi, ruzuku, tozo au ada zinazokusanywa na Baraza katika kutekeleza majukumu yake pamoja na mali yoyote itakayopatikana kwa kuuzwa au kukodishwa kwa mali inayomilikiwa

[122] Ibid, kifungu cha 5
[123] Ibid, kifungu cha 20

na Baraza.[124] Aidha, sheria pia imeanzisha kamati ya baraza la mitihani ambayo itaisaidia Baraza katika kutekeleza majukumu yake.[125]

Baraza la mitihani limepewa majukumu ya kuweka taratibu na viwango vitakavyotumika kwa skuli za msingi, sekondari na vyuo vya walimu, kusaidia katika kufikia mafanikio ya skuli ili kufikia malengo ya elimu na kuandaa miongozo ya tathmini kwa skuli na vyuo vya ualimu.[126]

Aidha, Baraza limepewa majukumu ya kutoa matokeo na kuzawadia vyeti wanafunzi waliofaulu, kuandaa ripoti ya kiwango cha matokeo ya ufaulu wa wanafunzi kwa mwaka na kupelekwa kwa wadau wote wa elimu, kufanya utafiti kwa lengo la kuboresha mitihani pamoja na majaribio ya wanafunzi, kuunga ushirikiano na mabaraza ya ndani na nje ya Zanzibar juu ya kupata uzoefu wa usimamizi na uendeshaji wa mabaraza hayo.[127]

### 3.4.7 Sheria ya Bodi ya Huduma za Maktaba Zanzibar Nam. 7 ya Mwaka 1993

Sheria hii imeanzisha Bodi ya Huduma za Maktaba kwa ajili ya kusimamia na kutoa huduma za maktaba Zanzibar.[128] Katika kuhakikisha ustawi wa elimu ya chini Zanzibar, sheria hii imeipa Bodi ya Huduma za Maktaba Zanzibar jukumu la kukuza, kuanzisha, kusimamia na kuendeleza maktaba na matumizi ya maktaba, kukuza na kuhamasisha matumizi ya maktaba kwa wazanzibari, kuanzisha na kuimarisha vituo vya nyaraka pamoja na kusaidia katika utoaji wa

---

[124] Sheria ya Baraza la Mitihani Zanzibar Nam. 6 ya Mwaka 2012, kifungu cha 19
[125] Ibid, kifungu cha 14
[126] Ibid, kifungu cha 5 (a), (b), (c), (d), (e)
[127] Ibid, kifungu cha 5(f), (g), (h), (i), (j)
[128] Sheria ya Bodi ya Huduma za Maktaba Zanzibar Nam. 7 ya Mwaka 1993, kifungu cha 3

vifaa pamoja na mafunzo ya taaluma za maktaba katika kila taaluma muhimu ambayo Bodi itaona inafaa.[129]

Aidha, majukumu mengine ya Bodi ya Hudumu za Maktaba ni kudhamini pamoja na kupanga semina na vikao mbali mbali vinavyohusiana na maktaba, kupanga majukumu pamoja na program za mafunzo kwa wafanyakazi wa maktaba kwa ajili ya kuboresha huduma za maktaba, kuhakikisha huduma bora za maktaba kwa maeneo ya mjini na shamba, kuhamasisha uzalishaji na ugawaji wa vitabu pamoja na huduma nyengine za maktaba pamoja na kufanya tafiti juu ya masuala yote yatakayosaidia kukuza huduma za maktaba.[130]

Katika kuimarisha ustawi wa elimu Zanzibar, Sheria hii imeweka utaratibu wa kisheria wa vyanzo vya mapato kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Bodi.[131]

### 3.4.8 Sheria ya Taasisi ya Elimu Nam. 4 ya Mwaka 2016

Sheria hii inatumika kwa Skuli Binafsi na za Serikali sambamba na Vyuo vya mafunzo ya Ualimu vya Serikali na Binafsi.[132] Sheria imezitaja kazi za Taasisi ikiwemo kubuni, kukuza, kufanya mapitio, kurekebisha na kutathmini mitaala kwa ajili ya skuli na vyuo.[133]

Taasisi ina jukumu la kuishauri Serikali kuhusiana na mambo yanayohusiana na ukuzaji na uendelezaji wa mitaala sambamba na kuandaa, kutathmini vitabu

---

[129] Ibid, kifungu cha 17(1) (a), (b), (c), (d)
[130] Ibid. kifungu cha 17(1) (e), (f), (g), (h), (m)
[131] Ibid, kifungu cha 24
[132] Sheria ya Taasisi za Elimu ya Zanzibar Nam. 4 ya Mwaka 2016, kifungu cha 2.
[133] Ibid,kifungu cha 5 (a).

na rejea, miongozo kwa walimu, ufundishaji na miongozo mengine ya kufundishia na ya watu wenye mahitaji maalum.[134]

Taasisi imepewa jukumu la kusaidia katika uendelezaji wa malengo ya elimu, sera na vipaumbele vya utaratibu bora wa uendelezaji wa elimu na usimamizi wa taaluma sambamba na kuandaa mipango ya kufundisha na kusaidia ufundishaji kwa walimu,[135] na kuanisha matatizo ya kielimu ndani ya Zanzibar ambayo yanahitaji kufanyiwa utafiti na kupatiwa ufumbuzi na kukuza mitaala ili kuinua kiwango cha ubora wa elimu.[136]

Katika kuhakikisha ustawi wa Elimu Zanzibar, Sheria hii imeunda Kamati ya Taaluma.[137] Miongoni mwa kazi za Kamati ni kufanya mapitio ya mitaala ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia kuanzia elimu ya maandalizi hadi vyuo vya ualimu sambamba na kuhakikisha ubora wa program za kielimu zinazotayarishwa na Taasisi;[138] kupitia masuala yote yanayohusiana na mitaala ya sera ya elimu na kutoa mapendekezo ya programu za elimu na mitaala iliyotayarishwa au kuthibitishwa kwa Bodi.[139]

### 3.4.9 Sheria ya Vyuo vya Amali Nam. 8 ya Mwaka 2006

Sheria hii ya Vyuo vya Amali itatumika kwa wale wote wanaoanzisha na kuendesha vituo vya mafunzo ya ufundi vya Zanzibar sambamba na

---

[134] Ibid, kifungu cha 5 (b) na (d)
[135] Ibid, kifungu cha 5 (g) na (i)
[136] Ibid, kifungu cha 5 (o) na (q)
[137] Ibid, kifungu cha 12 (1).
[138] Ibid, kifungu cha 13 (a) na (b)
[139] Ibid,kifungu cha 13(d) na ( e).

wanaohitaji mafunzo na ujuzi wa mafunzo ya ufundi husして wanawake, vijana, watoto, watu weye ulemavu na wanajamii.[140]

Sheria imeanzisha Mamlaka ya Mafunzo ya Amali,[141] ambayo itasimamia mafunzo ya ufundi kwa kutathmini viwango vya mafunzo, vituo, usajili, na kuidhinisha uwezo na ujuzi wa wakufunzi. Pia, kazi za Mamlaka zimefafanuliwa kuwa ni kuratibu mafunzo ya Amali kwa kufanya utafiti katika soko la ajira, kutayarisha mitaala ya mafunzo ya muda mfupi na mafunzo ya muda mrefu .[142]

Sheria hii imempa majukumu Mkurugenzi Mtendaji kuhakikisha kuwa mwongozo na mafunzo yanaelekezwa katika kutambua na kukuza vipaji kwa ajili ya uzalishaji, kuimarisha kiwango cha elimu ili kuwa na ufanisi zaidi,[143] kuandaa utaratibu na miongozo inayohusu mitihani, vyeti, mitaala, wakufunzi, upatikanaji wa wakufunzi pamoja na kufanya utafiti kuhusiana na soko la ajira.[144]

Sheria imetaja makosa pamoja na adhabu kwa mtu yeyote atakayeanzisha kituo cha mafunzo ya Amali bila ya idhini ya Bodi au bila ya kusajiliwa au baada ya kukataliwa kuanzisha kituo hicho na mamlaka husika, atakuwa ameenda kinyume na Sheria na atapewa adhabu ya kulipa faini isiyopungua Shilingi Laki Moja za Kitanzania au kifungo kisichozidi miezi sita au vyote.[145]

---

[140] Sheria ya Vyuo vya Amali Nam. 8 ya Mwaka 2006, kifungu cha 2 (i) na (ii)
[141] Ibid, kifungu cha 5 (1)
[142] Ibid, kifungu cha 6 (a) (b)
[143] Ibid, kifungu cha 8 (a)
[144] Ibid, kifungu cha 8(b) (d)
[145] Ibid, kifungu cha 29

**3.4.10 Sheria ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu Nam. 10 ya Mwaka 2018**

Sheria hii inatumika kwa Skuli zote za Maandalizi, Msingi na Sekondari, Taasisi zinazotoa mafunzo ya Ualimu, Vituo vya Elimu Mbadala na Watu wazima pamoja na Taasisi za Elimu zilizosajiliwa nje ya mfumo rasmi wa elimu.[146] Aidha, Sheria imeeleza malengo ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu na miongoni mwa malengo hayo ni kuhakikisha elimu inatolewa kwa mujibu wa Sera, Sheria na miongozo ya Serikali, kuhakikisha Taasisi zote zinafundisha kwa mujibu wa mitaala iliyoidhinishwa, kushauri juu ya viwango bora vya ufundishaji na ujifunzaji sambamba na kuhakikisha kuwa viwango vya elimu na udhibiti ubora vinafuatwa kwa ngazi zote za skuli na kwa mujibu wa miongozo ya Wizara.[147]

Vile vile Sheria hii imeanzisha mfumo wa Ukaguzi wa Elimu utakaothibitishwa na Bodi na ukaguzi utafanywa kwa kila skuli kwa kuangalia viwango vya ufundishaji na ufunzaji, ukaguzi wa masomo kwa kumkagua mwalimu wa somo kwa kila skuli sambamba na ukaguzi wa kushtukiza,[148] ili kuhakikisha mtaala uliokubalika ndio unatumika.[149]

Kazi za Mkaguzi mkuu wa Elimu ni pamoja na kusimamia upatikanaji wa mafanikio ya kiwango cha juu na ubora wa elimu katika skuli, kushirikiana na Idara za Serikali, wadau wengine na washirika wa maendeleo katika ukaguzi wa elimu.[150]

---

[146] Sheria ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu Nam.10 ya Mwaka 2018, kifungu cha 2
[147] Ibid, kifungu 6 (a) (b) (d) na (e )
[148] Ibid, kifungu cha 7 (1) a (I), (iii), na (iv).
[149] Ibid, kifungu cha 9 (a) (b) na (d)
[150] Ibid, kifungu cha 14 (b) (g)

Sheria imeweka makosa pamoja na adhabu kwa mtu yeyote ambaye kwa makusudi atakataa, atazuia au kukwamisha mkaguzi yoyote wa elimu kutekeleza majukumu yake atakuwa ametenda kosa na atatakiwa kulipa faini isiyopungua Shilingi Laki Tano na isiyozidi Shilingi Milioni Tano za Kitanzania au kifungo cha muda usiozidi mwaka mmoja au adhabu zote.[151] Aidha Sheria hii imezungumzia suala la kuwepo adhabu kwa mwalimu ambaye atashindwa kutekeleza majukumu yake ya usimamizi wa skuli ambaye atalazimika ndani ya miezi mitatu, kuchukuiwa hatua za kinidhamu.[152]

# SURA YA NNE

## 4.6 MAONI YA WADAU

## 4.7 Utangulizi:

Tume ya Kurekebisha Sheria katika kukamilisha utafiti huu, ilikutana na makundi thalathini na tano ya wadau yaliojumuisha Wizara inayosimamia masuala ya Elimu, Walimu wastaafu, Mamlaka za Elimu ikiwemo Baraza la Elimu Zanzibar, walimu wa sekta mbalimbali, wazazi na wanafunzi, na umoja wa skuli binafsi. Pia Tume ilikutana na wadau wengine mbali mbali zikiwemo Asasi za kiraia, vyama vya wafanyakazi kama vileChama cha Walimu (ZATU) na (ZATUC). Lengo la vikao hivyo lilikuwa ni kupata maoni na mapendekezo ya Shirikisho la Wafanyakazi Zanzibar, wadau wa sekta ya Elimu. Tume

[151] Ibid, kifungu cha 31.
[152] Ibid, kifungu cha 32.

imeyagawa maoni katika maeneo ya Kisera, Kisheria na Kiutendaji kama inavyoainishwa hapa chini.

### 4.8 Maoni ya Kisera

#### (a) Kuwepo na Sera Mpya ya Elimu

Wadau wamependekeza kuangaliwa tena Sera ya Elimu ya mwaka 2006 ili ijumuishe mipango na malengo ya Serikali yaliyoelezwa katika Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 na MKUZA pamoja na mabadiliko ya sekta ya elimu Kikanda na kidunia.

Aidha, wadau wamependekeza kuwa Sera ielekeze mifumo ya ufundishaji kwa kutumia teknolojia ya Mawasiliano ya Habari (ICT) na mifumo itakayohakikisha ushirikishaji zaidi wanafunzi katika suala la upatikanaji wa elimu. Imependekezwa Sera ibainishe matumizi mazuri ya lugha ya kufundishia pamoja na kuelekeza njia au mifumo ya kupima ufahamu wa wanafunzi.

#### (b) Kuwepo na Usimamizi mzuri wa Sera

Wadau wamependekeza Sera ianzishe mifumo ya usimamizi na ielekeze kwa walimu, wanafunzi, Wizara, wazazi, Serikali za Mitaa na taasisi binafsi juu ya nafasi yao katika mifumo ya kusimamia skuli zinazoanzishwa za Serikali na taasisi binafsi. Wadau hao pia wamependekeza Sera iweke wazi mfumo wa elimu na kuondoa changamoto iliyopo hivi sasa ambayo imempa uwezo Mh. Waziri kufanya mabadiliko ya mfumo kila baada ya muda.

### (c) Mapitio ya mfumo wa elimu

Wadau wamependekeza Sera ielekeze utaratibu na muda wa kufanyiwa mapitio mifumo ya elimu na mitaala iliopo ili kuweza kupima kiwango cha utekelezaji kila baada ya muda. Wadau hao walieleza kuwa Sera katika eneo hili ielekeze masomo, vitabu na silabasi za kutumika kulingana na mazingira na mabadiliko yaliopo. Aidha, wadau waliitaka Sera itoe maelekezo ya mitaala kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, walimu, na maeneo ya skuli ambayo yatakuwa rafiki kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

## 4.9 Maoni ya Kisheria

### (a) Marekebisho ya Sheria ya Elimu

Wadau wameeleza kwamba Sheria ya Elimu ya mwaka 1982 ina mapungufu ambayo yanakwaza ukuaji wa sekta ya elimu nchini.

Aidha, wadau hao walipendekeza Sheria hii kufanyiwa mapitio kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2020 na mipango ya muda mrefu ya nchi ambayo maudhui yake bado hayajazingatiwa katika Sheria ya Elimu.

Maeneo mengine yaliyobainishwa na wadau kuwa yanahitaji kufanyiwa mapitio katika Sheria ni pamoja na masuala ya mitaala, matumizi ya TEHAMA, udhibiti wa skuli binafsi, masharti kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu, majukumu ya walimu, wazazi na jamii katika usimamizi wa elimu nchini.

### (b) Kuboreshwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Elimu

Wadau wamependekeza kuwa Mfuko wa Maendeleo ya Elimu uliowekwa kwenye Sheria ya Elimu, uwekewe misingi ya kikanuni ya usimamizi na

utaratibu wa upatikanaji wa fedha za Mfuko huo ili kuleta maendeleo katika sekta ya elimu kama ilivyoelekezwa katika Sheria. Aidha, imependekezwa Mfuko huu pia uainishe upatikanaji wa fedha zake, matumizi yake pamoja na shughuli zake ikiwemo kuendeleza elimu, ununuzi wa baadhi ya vifaa vya skuli na masuala ya utafiti na tathmini juu ya masuala mbalimbali yanayohusu elimu.

**(c) Msajili wa Elimu**

Wadau wamependekeza kuimarishwa majukumu ya Kitengo cha Msajili wa Elimu ili kiweze kusajili masuala mbali mbali ya elimu ikiwemo usajili wa skuli binafsi na za Serikali, usajili wa walimu, kutoa vyeti vya usajili wa walimu na shughuli nyengine zitakazowekwa kwa mujibu wa Sheria. Aidha, wadau hao walipendekeza Msajili apewe jukumu la kufanya tathmini ya walimu na skuli zilizopo, kufuta usajili iwapo masharti ya Sheria hayatazingatiwa na kutoa ripoti za utendaji na mapendekezo ya kuimarisha usimamizi wa walimu na skuli ziliopo.

**(d) Baraza la Elimu**

Wadau wameeleza kwamba Baraza la Elimu halijafanya kazi inavyotakiwa na kwamba kuna haja kuzingatia sifa za wajumbe, idadi ya wajumbe, kazi za wajumbe pamoja na majukumu ya kumshauri Waziri katika usimamizi wa sekta ya elimu nchini. Wadau pia walishauri Baraza hili liwekewe muundo, muda wa kufanya kazi, na masharti ya kuanzishwa kwake ili liweze kusimamia vyema na kuvishauri vyombo na taasisi zinazosimamia elimu Zanzibar.

**(e) Kuanzishwa kwa Tume ya Utumishi ya Walimu**

Wadau wamependekeza kuanzishwa kwa Tume ya Utumishi ya Walimu ambayo itashughulikia masuala na mahitaji yote ya walimu ili kuweza kuwadhibiti walimu wote, maslahi yao, kuwapandisha madaraja, kupatiwa mafunzo ya nadharia na vitendo. Imependekezwa Tume hii iwe na mamlaka kama zilivyopewa Tume nyengine za Utumishi. Pendekezo hili la wadau limetokana na ukweli kuwa kada hii imekuwa na watumishi wengi na kuhitaji usimamizi na uangalizi wa walimu kwa karibu zaidi, utakaoweza kufanywa kwa ufanisi kupitia Tume ya Utumishi wa Walimu.

**(f) Kamati za Elimu katika ngazi ya Wilaya na Mkoa**

Wadau wamependekeza kuangaliwa muundo wa Kamati za Elimu katika ngazi ya Wilaya na Mkoa kama ilivyoelezwa katika vifungu vya 26 na 28 vya Sheria ya Elimu pamoja na kuweka wazi majukumu ya Kamati hizo. Wadau Walipendekeza kuwa Kamati hizi ziwekewe utaratibu wa kusaidia zaidi masuala ya elimu katika maeneo yao na kuainisha umuhimu wa vyombo hivyo, matumizi ya vyombo hivyo, uratibu wake na uwajibikaji wake katika ngazi za Mikoa na Wizara ya Elimu.

**(g) Ukaguzi wa Elimu**

Mbali ya kuwepo kwa Sheria maalum inayosimamia masuala ya ukaguzi, wadau wamependekeza Sheria ya Elimu ijumuishe vifungu vya msingi wa ukaguzi imara wa elimu ili kuratibu utaratibu mzuri wa kuwasilisha ripoti na utekelezaji wa matokeo ya ripoti za ukaguzi.

Aidha, imependekezwa na wadau kuwa Sheria iweke wazi ukaguzi wa elimu ujumuishe uwajibikaji wa walimu, ubora wa elimu inayotolewa, tathmini ya

wanafunzi na vitendea kazi. Wadau wamependekeza pia eneo la ukaguzi libainishe wazi sifa za wakaguzi, uweledi, uadilifu na uzoefu wao ili kuwasaidia kuchanganua kasoro zilizopo katika meneo wanayoyakagua na kutoa mapendekezo.

Kwa upande mweninge, wadau walipendekeza kuwekwa mfumo imara utakaohakikisha taarifa za ukaguzi wa elimu zinafanyiwa kazi ipasavyo na kunakuwa na utaratibu wa kueleza namna taarifa hizo zilivyofanyiwa kazi.

**(h) Sifa za mwalimu**

Wadau wamependekeza eneo la sifa za walimu liwekewe masharti zaidi kwa lengo la kuwa na walimu wenye uweledi, maadili, nidhamu na taaluma ya kutosha katika ufundishaji. Aidha, imependekezwa walimu wapangiwe masomo kwa mujibu wa sifa walizonazo na waendelezwe kwa kupatiwa mafunzo katika maeneo ambayo watakuwa wanayafundisha. Vile vile walimu wawekewe muda maalum wa kufundisha na isifike muda wa kustaafu wakiwa bado wanafundisha kwa vyenginevyo wapangiwe kazi nyengine katika taasisi za elimu.

**(i) Maadili ya ualimu**

Wadau wamependekeza kuanzishwa kanuni za maadili ya walimu pamoja na utaratibu wa kuripoti masuala ya nidhamu yanayotokana na walimu ili kuhakikisha nidhamu inaongezeka na walimu wanakua mfano bora kwa wanafunzi na kwa jamii kwa ujumla. Aidha, katika kuitolea ufafanuzi hoja hii, Wadau wamependekeza Sheria iweke utaratibu wa kuwasilisha malalamiko yanayohusu maadili ya walimu, jinsi ya kushughulikia malalamiko hayo, na

hatua za kuchukuliwa kwa walimu wanaokiuka maadili kwa mujibu wa Kanuni za Maadili za walimu na kutokana na mtizamo wa jamii na heshima wanayopewa walimu katika maeneo ya skuli na maeneo wanayoishi.

**(j) Sheria itambuwe kuanzishwa na majukumu ya Idara mbalimbali**

Wadau wamependekeza Sheria ya Elimu itambue idara au taasisi ambazo zipo chini ya Wizara na majukumu yake hayajawekwa vizuri katika Sheria. Wadau hao walibainisha Idara zinazotakiwa kuzingatiwa ni pamoja na Idara ya masuala ya teknolojia ya Mawasiliano na majukumu yake, ukuzaji mitaala, masuala ya mitihani Zanzibar, ofisi ya Mrajis wa elimu, ukaguzi wa Elimu, usimamizi wa skuli binafsi ambapo kazi zao zitaelezwa na sheria husika.

**(k) Majukumu ya wazazi/walezi na jamii**

Wadau wamependekeza Sheria ya Elimu ibainishe wazi majukumu ya wazazi/walezi na jamii katika kusimamia masuala ya elimu kwa watoto wao. Imeelezwa kwamba kutokana na mabadiliko ya teknolojia na utandawazi, ni vigumu jukumu la kuwaelimisha wanafunzi kuachiwa walimu pekee na kuna haja ya kuwa na mashirikiano ya karibu baina ya wazazi/walezi na walimu na suala hilo la ushirikiano liwekwe Kisheria.

**(l) Ushiriki wa wadau mbali mbali katika sekta ya elimu**

Wadau wamependekeza kuwekwa mazingira mazuri ya ushirikiano baina ya Wizara, wawekezaji, wanasiasa, wahisani na washirika wa maendeleo na taasisi za serikali na wadau wengine wakiwemo asasi za kiraia ili mashirikiano yanayofanywa na taasisi hizo yaratibiwe vizuri, yawekewe misingi imara, yafuate masharti ya sheria iliopo na yasaidie kunufaisha sekta nzima ya elimu.

Imeelezwa kwamba hatua hii itasaidia kujua matumizi na usimamizi wa michango, fedha na misaada mbali mbali inayopelekwa katika skuli mbali mbali na thamani halisi ya michango au misaada inayotolewa na matarajio ya wadau wanaosaidia katika sekta hii.

**(m) Mitaala ya Elimu Mbadala**

Wadau wamependekeza Sheria ibainishe kuwa mitaala ya elimu iwekewe utaratibu katika kupitishwa kwake na jinsi ya kuzingatia mahitaji ya nchi na malengo ya Serikali ili kutoa fursa kwa wanafunzi wanaomaliza elimu ya Sekondari kujiendeleza katika mfumo wa elimu mbadala na vyuo vya amali.

Wadau hao wamependekeza kuwe na muendelezo wa elimu ya sekondari hadi elimu ya vitendo kwa kuhakikisha kwamba kunawekwa utaratibu wa wanafunzi wanaomaliza sekondari kupangiwa vyuo vya amali na fani za kusomea kulingana na utaalamu unaohitajika. Aidha, walipendekeza kuwa wakati wanafunzi wanamaliza masomo ya Sekondari wapewe fursa ya kuchagua masomo na fani wanazopendelea kusoma katika hatua zinazofuata za masomo yao katika vyuo vya amali na kuondokana na dhana ya mafunzo ya amali kuwa kwa waliofeli masomo yao..

**(n) Adhabu**

Wadau wamependekeza Sheria irekebishwe katika eneo la adhabu kwa makosa mbali mbali iwapo masharti ya Sheria hii yatakiukwa ikiwemo kuanzisha skuli bila ya kusajiliwa, vibali vya kufundishia, kufundisha kwa kutumia mitaala isiyoruhusiwa, kukiuka maadili, kutokutekeleza wajibu kwa wazazi, walimu n.k.

Aidha, imependekezwa adhabu zitakazoainishwa katika Sheria zilingane na makosa yanayofanywa, na baadhi ya makosa yanayohusisha jinai au masuala ya watoto yawekewe utaratibu kulingana na Sheria zinazosimamia masuala haya.

**(o) Eneo la utafiti wa elimu**

Wadau wamependekeza kuwekwa mamlaka na malengo ya kufanya utafiti wa maeneo mbali mbali yanayogusa sekta ya elimu na usimamizi wake kwa Zanzibar. Imependekezwa tafiti hizo zilenge kuweka sera bora za elimu kila baada ya muda, katika maeneo ya usimamizi wa walimu, usimamizi wa wanafunzi, tathmini ya ufaulu wa wanafunzi, mitaala na usimamizi wa mitihani kwa ujumla. Pia, walishauri matokeo ya utafiti yalenge kuishauri Bodi na Serikali kuchukua maamuzi kuhusu maendeleo ya elimu Zanzibar.

**(p) Elimu iakisi vipaumbele vya nchi**

Wadau wamependekeza mifumo ya elimu izingatie mazingira na kujumuisha maeneo ya vipaumbele katika kukuza uchumi wa Zanzibar. Hivyo, imependekezwa wanafunzi wafundishwe misingi ya uchumi wa buluu kwa kuwa Zanzibar imezungukwa na bahari, masuala ya utalii na uwekezaji, kilimo na uvuvi ambayo yanachangia asilimia kubwa katika uchumi wa Zanzibar na wananchi wengi wanajikita katika maeneo hayo. Wadau hao wameeleza kuwa mapendekezo hayo yanatokana na haja ya elimu tokea ngazi za chini kuwatayarisha wazanzibari kuwa na stadi zitakazowawezesha kuingia katika soko la ajira.

### (q) Uanzishwaji wa Skuli

Wadau wamependekeza Sheria iweke wazi sifa za kuanzisha skuli hasa za binafsi kama vile mazingira ya majengo, upatikanaji wa vitabu, uwezo wa walimu na sifa zao, mazingira ya wanafunzi, uwezo wa kifedha wa skuli ili kuhakikisha skuli zinazoanzishwa zinadumu kwa muda mrefu, zinajiendeleza na zina vyanzo vya kifedha vya uhakika.

Wadau hawa walieleza kuwa sheria iweke masharti hayo kwa kuwa kuna baadhi ya skuli zinazoanzishwa ni za kibiashara zaidi na za kimsimu ambazo hufanya kazi kwa muda mfupi, hazina uwezo wa kutoa elimu inayostahiki kwa wanafunzi na baadhi hufungwa ndani ya muda mfupi. Wadau hao pia wameeleza kwamba mazingira ya baadhi ya skuli hayaridhishi na skuli nyingi hazina vyombo vya usimamizi vya kufuatilia maendeleo ya wanafunzi kwa jumla.

### (r) Uteuzi wa walimu wakuu

Wadau wamependekeza sheria ibainishe sifa maalum kwa walimu wakuu wa skuli kwa kuzingatia uzoefu wao na uwezo waliokuwa nao wa kiuongozi. Imependekezwa walimu hao wapatiwe mafunzo ya uongozi na usimamizi wa walimu walio chini yao pamoja na wanafunzi. Wadau pia wamependekeza Sheria iweke wazi majukumu ya walimu wakuu wa skuli, mamlaka yao, uwezo wao na hatua za kuchukua katika masuala yanayojitokeza katika shughuli zao.

## 4.10 Masuala ya Kanuni

Wadau walieleza kwamba maeneo kadhaa ambayo yameelezwa katika Sheria ya Elimu yana changamoto kutokana na kutokutungwa Kanuni na miongozo kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 60 (1) cha Sheria hiyo. Kanuni hizo zilikusudiwa zisaidie utekelezaji mzuri wa Sheria hiyo na hivyo kutokutungwa kwake kunaathiri utekelezaji mzuri wa Sheria hii ya Elimu. Miongoni mwa maeneo ambayo Wadau walieleza kuwa yameshindwa kutekelezwa kutokana na kutotungwa Kanuni ni pamoja na uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Elimu ambao utekelezaji wake umeelezwa kuhitaji kufafanuliwa katika Kanuni. Wadau walieleza kuwa utekelezaji wa baadhi ya mambo katika sekta ya elimu yanahitaji hatua za utendaji ili kuimarisha sekta ya elimu hivyo, wadau hao walitoa maoni mbali mbali ya kiutendaji kama yanavyofafanuliwa hapa chini. Hivyo, wadau hao wamependekeza kutungwa kwa kanuni hizo ili kusaidia ufanisi wake.

### 4.11 Maoni ya Kiutendaji

#### (a) Utoaji wa huduma kielektorniki

Wadau wamependekeza kuwa baadhi ya huduma muhimu kama vile leseni za walimu zitolewe kwa njia ya kielektroniki ili kupunguza urasimu na gharama kwa wizara na watumiaji. Aidha, kwa upande wa leseni za walimu wamependekeza kuwepo na usimamizi mzuri tofauti na hali iliyopo sasa ambapo leseni za walimu hazitolewi kwa mujibu wa sheria na kanuni.

#### (b) Watoto wenye ulemavu

Wadau wamependekeza skuli ziweke mazingira ya kujifunzia kwa Watoto wenye mahitaji maalum Pamoja na kuwapa ushauri nasaha mara kwa mara ili

wajione ni sehemu ya jamii na kukuza ufahamu na ufaulu wao. Mazingira yaliyoelezwa na wadau ni pamoja na miundombinu itakayowawezesha watoto wenye mahitaji maalum kuyafikia maeneo ya kujifunzia kwa urahisi pamoja na vifaa maalum vinavyohitajika kwa ajili ya watoto hao. Wadau pia walipendekeza kuanzishwa skuli maalum za watoto wenye ulemavu kwa lengo la kumudu kuwapatia elimu kwa pamoja.

### (c) Uvamizi wa maeneo ya skuli

Wadau wamependekeza suala la umiliki wa maeneo ya skuli na mipaka yake liwekwe wazi na kupatikana hati miliki ili kuzuia watu binafsi wasivamie na kujenga katika maeneo ya skuli. Aidha, wadau wamependekeza kuwa inapotokea kuna uvamizi wa maeneo ya skuli, hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya mtu alievamia eneo hilo, jambo ambalo litapunguza uvamizi wa maeneo ya skuli kwa kiasi kikubwa.

### (d) Mafunzo endelevu kwa walimu

Kwa upande mwengine, wadau wamependekeza Wizara inayohusika na elimu iandae program bora zaidi na zitakazokua endelevu, za kutoa mafunzo kwa walimu wa ngazi mbali mbali. Wadau hao walipendekeza kuwepo kwa programu hizo za mafunzo endelevu kutokana na kuwepo kwa changamoto ya uwezo wa kufundisha kwa baadhi ya walimu na hivyo kuathiri viwango vya elimu kwa wanafunzi. Aidha, walipendekeza kuwa mafunzo hayo kwa walimu yazingatie mageuzi ya mfumo wa elimu unaopendekezwa.

### (e) Kuimarisha maslahi ya walimu

Wadau pia walipendekeza kuchukuliwa jitihada mahsusi kuimarisha maslahi ya walimu ili kazi ya ualimu iwe na hadhi ya hali ya juu na vijana wengi wenye uwezo mkubwa kitaaluma wawe na hamu kusomea fani ya ualimu na kufundisha. Wadau hao walieleza kuwa kwa sasa kozi ya ualimu husomwa na vijana waliokosa fursa ya kujiunga na baadhi ya kozi zinazoonekana kuwa na hadhi zaidi kama udaktari, uhandisi, uhasibu, sheria na kozi nyengine kama hizo. Hivyo, wadau hao walishauri juhudi mahsusi zichukuliwe ili kubadili mtazamo huo katika jamii na fani ya ualimu ipate vijana wenye ufahamu mkubwa kielimu ili kukuza sekta ya elimu.

**(f) Kuimarishwa kwa Miundombinu ya Skuli**

Wadau wamebainisha kuwa maendeleo ya sekta ya elimu kwa kiasi kikubwa yanategemea upatikanaji wa miondombinu bora katika skuli ikiwemo madarasa bora yenye nafasi za kutosha, viti vya kukalia wanafunzi, maabara na maktaba za kisasa na zenye vifaa bora vya kijifunzia pamoja na nyumba za walimu za kisasa. Hivyo, wadau hao wamependekeza jitihada mahsusi zichukuliwe kuimarisha miundombinu hiyo ya skuli ili wanafunzi wapate mazingira mazuri ya kujifunzia.

# SURA YA TANO

## 6.0 MIKATABA YA KIMATAIFA, KIKANDA NA UZOEFU WA NCHI NYENGINE

## 6.1 UTANGULIZI

Mikataba ya Kimataifa pamoja na Mikataba ya Kikanda imeweka misingi ya upatikanaji wa haki ya elimu kwa kuifanya haki hiyo kuwa ni ya lazima kwa kila binadamu na kuzitaka nchi wanachama kuwapatia wananchi wake elimu bila ya malipo. Vile vile, Mikataba hii imweka usimamizi wa kulinda upatikanaji wa haki ya elimu.

## 5.2 Mikataba ya Kimataifa

### 5.2.1 Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu (1948)

Azimio la Kimataifa la Haki za binadamu limepitishwa mwaka 1948 na Umoja wa Mataifa.[153] Azimio hili linajumuisha aina zote za haki za binadamu yaani haki za kiraia na kisiasa pamoja na haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni.[154]

Azimio hili limetoa haki ya kila mtu kupata elimu na kusoma kadri apendavyo bila ya kujali kabila, rangi au uraia.[155] Azimio hili limezitaka nchi wanachama kuwapatia wananchi wake elimu bila ya malipo angalau katika ngazi ya elimu ya awali pamoja na elimu ya msingi.[156]

Aidha, Azimio hili limetamka kuwa elimu ya msingi ni ya lazima kwa kila binadamu, elimu za kitaalamu ziwe zinapatikana kwa kila mtu anayehitaji kujifunza. Pamoja na hayo, elimu ya juu itolewe kwa misingi ya usawa ambayo itazingatia sifa za ufaulu.[157]

Azimio hili limetamka kuwa elimu inayotolewa na nchi wanachama ielekezwe katika maendeleo ya misingi ya tabia za kibinadamu, kuimarisha misingi ya haki za binadamu na misingi ya uhuru.[158] Mkataba huu umetoa haki kwa wazazi kuchagua aina ya elimu ambayo watapewa watoto wao.[159]

### 5.2.2 Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni wa Mwaka 1966.

---

[153] Mkataba wa haki za Binadamu wa Mwaka 1948 ambao unapatikana Universal Declaration of Human Rights | United Nations
[154] Azimio la Haki za Binadamu 1549287176-Mkataba wa Kimataifa wa Kutokomeza aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake.pdf (parliament.go.tz) ukurasasa wa 1.
[155] Kifungu cha 26 cha Tamko la Haki za Binadamu Duniani la Mwaka 1948.
[156] Kifungu cha 26 (1) cha Tamko la Haki za Binadamu Duniani la Mwaka 1948
[157] ibid
[158] Ibid, kifungu cha 26 (2)
[159] Ibid, kifungu cha 26 (3)

Mkataba huu ulipitishwa na Umoja wa Mataifa mnamo mwaka 1966 na kuanza kutumika tarehe 3 Januari, 1976.[160] Mkataba huu ulianzishwa kwa lengo la kuhakikisha nchi wanachama wanasimamia upatikanaji wa haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni kwa wananchi wao.[161]

Mkataba huu unazitaka nchi wanachama kutambua haki ya kila mtu katika elimu ambayo itaelekezwa katika maendeleo ya misingi ya utu pamoja na kuimarisha misingi ya haki za binadamu na uhuru.[162] Vile vile, nchi wanachama zihakikishe kuwa elimu itakayotolewa inampelekea mtu kuweza kushiriki katika masuala ya kijamii na ilenge kuimarisha uelewa, uvumilivu pamoja na kujenga urafiki kati ya mataifa yote, rangi au vikundi vya kidini pamoja na kuendeleza shughuli za Umoja wa Mataifa kwa ajili ya kudumisha Amani.[163]

Aidha, katika utekelezaji wa upatikanaji wa haki ya elimu kwa kila mtu, mkataba huu umezitaka nchi wanachama kuhakikisha kuwa:[164]

(a) Elimu ya msingi ni ya lazima na inatolewa bure kwa kila binadamu.

(b) Elimu ya sekondari, elimu ya ufundi na elimu ya amali zipatikane kwa watu wote ikiwa ni muendelezo wa elimu bila ya malipo.

(c) Elimu ya juu itolewe kwa usawa.

(d) Elimu ya muendelezo itolewe kwa wote ambao hawakubahatika kupata elimu ya msingi.

---

160 Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni wa mwaka 1966 unapatikana UN General Assembly, *International Covenant on Economic, Social and Cultural Rights*, 16 December 1966, United Nations, Treaty Series, vol. 993, p. 3, https://www.refworld.org/docid/3ae6b36c0.html [accessed 24 March 2023]

161 ibid, Refworld | International Covenant on Economic, Social and Cultural Rights

162 Kifungu cha 13 cha Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni wa mwaka 1966. Refworld | International Covenant on Economic, Social and Cultural Rights

163 Ibid

164 Ibid kifungu cha 13 (2)

(e) Kufuatilia kwa kikamilifu mfumo mzima wa skuli katika ngazi zote za elimu na kuhakikisha maslahi bora yanapatikana kwa walimu.

### 5.2.3 Mkataba wa Haki za Mtoto wa mwaka 1989

Mkataba huu wa Haki za Mtoto ulipitishwa na Umoja wa Mataifa mnamo mwaka 1989 na kuanza kutumika Septemba 1990. Mkataba huu ndio uliokubalika zaidi duniani katika mikataba ya haki za binadamu.[165] Mkataba huu unajumuisha haki kamili za watoto zikiwemo haki za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni katika mkataba mmoja.[166]

Aidha, katika kusimamia haki za kijamii, Mkataba huu unatambua haki ya mtoto kupata fursa sawa ya elimu.[167] Mkataba huu unazitaka nchi wanachama kuhakikisha kuwa elimu ya msingi ni ya lazima na inatolewa bila ya malipo kwa watu wote.[168] Pia, nchi wanachama zinatakiwa kuimarisha elimu ya sekondari pamoja na elimu ya mafunzo ya amali na ufundi na iweze kupatikana kwa kila mtoto pamoja na kuchukua hatua zinazofaa kuhakikisha elimu hizo zinatolewa bila ya malipo na kama itahitajika, basi msaada wa kifedha utolewe kwa watoto.[169] Vile vile, nchi wanachama zinatakiwa kusimamia upatikanaji wa elimu ya juu kwa misingi ya usawa kwa wote, na taarifa na miongozo ya upatikanaji wa elimu na mafunzo ya amali iwe inapatikana kwa watoto wote.[170]

---

[165] Compass: Manual for Human Rights Education with Young people, Council of Europe inapatikana Compass: Manual for Human Rights Education with Young People - Manual for Human Rights Education with Young people (coe.int)

[166] ibid

[167] Kifungu cha 28 cha Mkataba wa Haki ya Mtoto wa mwaka 1989

[168] Ibid

[169] ibid

[170] ibid

Aidha, mkataba huu unazitaka nchi wanachama kuchukua juhudi za kumarisha mahudhurio katika maskuli pamoja na kupunguza utoro maskulini.[171] Katika uchukuaji wa hatua za kinidhamu kwa watoto, Mkataba huu unazitaka nchi wanachama kuhakikisha kuwa hatua za kinidhamu zinazotolewa maskulini zinalinda utu wa mtoto.[172]

Pamoja na hayo, Mkataba huu unazitaka nchi wanachama kuhakikisha kuwa elimu ya mtoto inaelekezwa katika kukuza utu wa mtoto, kipaji chake na uwezo wake wa kiakili na kimwili.[173] Vile vile, elimu hiyo ielekezwe katika kukuza heshima kwa wazazi wa watoto, utambulisho wao wa kiutamaduni, asili yao, lugha na maadili ya nchi wanayoishi au maadili ya nchi waliyotoka.[174]

### 5.2.4 Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW) wa mwaka 1979.

Umoja wa Mataifa ulipitisha Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW) tarehe 18 Disemba 1979 na kuanza kutumika tarehe 3 Septemba 1981. Mkataba huu unajulikana ulimwenguni kama mkataba wa kimataifa wa haki za wanawake.[175] Tanzania ilisaini Mkataba huu tarehe 7 Julai, 1980 na kuuridhia Mkataba huu tarehe 20 Agosti,1985.

---

[171] ibid
[172] Ibid, kifungu cha 28 (2)
[173] Ibidi kifungu cha 29 (1) (a)
[174] Ibidi, kifungu cha 29 (1)(c)
[175] Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW) wa Mwaka 1979 unapatikana Convention on the Elimination of All Forms of Discrimination against Women (un.org)

Mkataba huu unazingatia maeneo matatu muhimu ambayo ni haki za Kiraia na hali ya kisheria za wanawake, haki za uzazi na mambo ya kiutamaduni yanayoathiri mahusiano ya jinsia.[176] Katika utekelezaji wa upatikanaji wa haki za kiraia, Nchi wanachama zinatakiwa kuchukua hatua zote zinazofaa kuondoa ubaguzi dhidi ya wanawake na kuwahakikishia haki sawa baina ya wanawake na wanaume katika nyanja ya elimu pamoja na kuhakikisha kuwapo kwa usawa wa elimu kati ya wanawake na wanaume.[177] Vile vile, Mkataba huu unazitaka nchi wanachama kuhakikisha elimu inapatikana katika makundi yote ya vijijini na mijini na kuhakikisha maeneo yote kunakuwepo skuli za awali, msingi, sekondari, ufundi, elimu ya juu, na mafunzo ya amali.[178]

Aidha, Mkataba huu unazitaka nchi wanachama kupunguza idadi ya wanafunzi wa kike wanaoacha skuli na kuandaa programu maalum kwa watoto wa kike na wanawake walioacha skuli mapema.[179]

### 5.2.5 Mkataba wa Haki za Watu wenye Ulemavu wa mwaka 2006.

Mkataba wa Haki za Watu wenye Ulemavu unalenga kulinda haki za binadamu na utu wa watu wenye ulemavu.[180] Mkataba huu ulipitishwa na Umoja wa Mataifa mnamo mwaka 2006 na kuanza kutumika Mwezi Mei, 2008.

---

[176] Eferrit Unachopaswa kujua kuhusu Mkataba wa Haki za Binadamu wa CEDAW inapatikana Unachopaswa kujua kuhusu Mkataba wa Haki za Binadamu wa CEDAW (eferrit.com)

[177] Kifungu cha 10 cha Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW) wa Mawaka 1979

[178] ibid

[179] ibid

[180] Convention on the Rights of Persons with Disabilities - Physiopedia (physio-pedia.com)

Mkataba huu unazitaka nchi wanachama kutambua haki ya elimu kwa watu wenye ulemavu.[181] Katika kusimamia upatikanaji wa haki hii, nchi wanachama zimetakiwa kutambua hali hii bila ya ubaguzi na kwa misingi ya usawa na kuhakikisha kuwa nchi wanachama zinakuwa na mfumo wa elimu jumuishi katika ngazi zote za elimu.[182]

Aidha, katika utoaji wa elimu, nchi wanachama wanatakiwa kuhakikisha elimu inayotolewa inaelekezwa katika ukuzaji wa watu wenye ulemavu na utu wao, vipaji na ubunifu wao pamoja na uwezo wao wa kiakili na kimwili.[183]

### 5.2.6 Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa mwaka 1966.

Mkataba huu ni miongoni mwa mikataba muhimu ya haki za binadamu ambao unatoa ulinzi mbali mbali kwa haki za kiraia na kisiasa.[184] Mkataba huu ulipitishwa na Umoja wa Mataifa mnamo mwaka 1966 na kuanza kutumika mwaka 1976.

Aidha, katika Ibara ya 18 ya Mkataba huu unazitaka nchi wanachama kuhakikisha kuwa kila mtu ana haki ya kuwa na uhuru wa mawazo, fikra (*conscience)* na uhuru wa dini. Haki hii inajumuisha uhuru wa kuchagua dini au imani mtu aitakayo, uhuru wa kushiriki katika masuala ya kidini, uhuru wa

---

[181] Kifungu cha 24 cha Mkataba wa Haki za Watu wenye Ulemavu.
[182] ibid
[183] ibid
[184] FAQ: The International Covenant on Civil & Political Rights (ICCPR) | American Civil Liberties Union (aclu.org)

kuabudu pamoja na uhuru wa kufundisha dini.[185] Hivyo, haki hii inajumuisha uhuru wa mtu kupata elimu ya dini.

Vile vile, Mkataba huu unazitaka nchi wanachama kuheshimu uhuru wa wazazi na walezi katika kuhakikisha kuwa watoto wao wanapata elimu ya dini na maadili kwa mujibu wa imani zao.[186]

### 5.2.7 Mkataba wa UNESCO dhidi ya Ubaguzi katika Elimu wa mwaka 1960

Mkataba wa UNESCO dhidi ya Ubaguzi katika Elimu ulipitishwa na Mkutano Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) mnamo mwaka 1960 na ulianza kutumika mwaka 1962.[187]

Mkataba huu umetafsiri neno 'ubaguzi' kuwa linajumuisha kutengwa, kuzuiliwa au kufanyiwa upendeleo kwa kuzingatia rangi, jinsia, lugha, dini, siasa au maoni mengine, asili ya kitaifa au kijamii, hali ya kiuchumi au hali ya kuzaliwa kwa lengo la kusababisha kutokuwa na usawa katika upatikanaji wa elimu hasa:[188]

(i) Katika kumyima mtu yeyote au kikundi cha watu fursa ya kupata elimu ya aina yoyote au katika ngazi yoyote ya elimu.

(ii) Kumuwekea mtu au kikundi cha watu ukomo wa elimu wenye viwango vya chini.

(iii) Kuanzisha mifumo tofauti ya elimu au taasisi kwa ajili ya watu au makundi ya watu.

---

[185] Kifungu cha 18 (1) cha Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa mwaka 1966.

[186] Ibid, kifungu cha 18 (4)

[187] Convention against Discrimination in Education; adopted by the General Conference at its eleventh session, Paris, 14 December 1960 - UNESCO Digital Library

[188] Ibara ya 1 ya Mkataba wa UNESCO dhidi ya Ubaguzi katika Elimu wa mwaka 1960.

(iv) Kumuekea mtu au kikundi cha watu masharti ambayo hayaendani na utu wa mwanadamu.

Aidha, katika kupinga ubaguzi katika elimu, Mkataba huu umetafsiri elimu kwa kujumuisha aina zote za elimu, viwango vyake, upatikanaji wa elimu, kiwango cha ubora wa elimu na masharti ambayo elimu hiyo inatolewa. [189]

## 5.3 Mikatiba ya Kikanda

### 5.3.1 Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa Mwaka 1981

Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu ambao pia unajulikana kama Mkataba wa Banjul, ulipitishwa na Umoja wa Afrika kwa lengo la kutoa ulinzi wa kimataifa wa haki za msingi za binadamu na kukuza misingi ya uhuru kwa binadamu barani Afrika.[190]

Ibara ya 17 ya Mkataba huu kinatoa haki ya kupata elimu kwa kila mtu. Aidha, Mkataba huu umeweka wajibu kwa nchi wanachama kuheshimu haki (ikiwemo haki ya elimu) na uhuru uliotelewa katika Mkataba huu.[191] Vile vile, nchi wanachama zimetakiwa kutoa uelewa kwa wananchi wao kuwa upatikanaji wa uhuru na haki uliotajwa katika Mkataba huu unaenda sambamba na wajibu na majukumu ya wananchi.[192]

### 5.3.2 Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto wa Mwaka 1990.

---

[189] Ibid, kifungu cha 2

[190] Utangulizi wa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa mwaka 1981 unapatikana 36390-treaty-0011_-_african_charter_on_human_and_peoples_rights_e.pdf (au.int)

[191] Kifungu cha 25 cha Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa Mwaka 1981

[192] ibid

Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto umeweka na kufafanua haki za msingi za mtoto barani Afrika. Mkataba huu ulipitishwa na Umoja wa Afrika mnamo mwaka 1990 na kuanza kutumika 1999.[193]

Mkataba huu katika Ibara yake ya 1 inazitaka nchi wanachama kuzitambua haki, uhuru na wajibu ulioainishwa katika Mkataba huu pamoja na kuchukua hatua za lazima katika kuhakikisha haki, uhuru na wajibu uliotolewa katika Mkataba huu unasimamiwa na sheria za ndani za nchi wanachama.

Aidha, Ibara ya 11 ya Mkataba huu inatoa haki ya kupata elimu kwa kila mtoto. Hivyo, nchi wanachama wa Umoja wa Afrika zinatakiwa kuhakikisha sheria zao za ndani zinasimamia na kutoa haki hii ya mtoto ya kupata elimu.

### 5.3.3 Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa haki za Binadamu na Watu kuhusu Haki za Wanawake katika Afrika ya mwaka 2003.

Itifaki hii ilipitishwa na Umoja wa Afrika mnamo mwaka 2003 Mjini Maputo Msumbiji na kuanza kutumika mwaka 2005. Itifaki hii inatambua na kuhakikisha haki za wanawake za kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni zinatambulika kimataifa.[194]

Aidha, Ibara ya 12 ya Itifaki hii inatoa haki ya elimu na kupata mafunzo (training) kwa wanawake wote wa Kiafrika. Aidha, itifaki hii inazitaka nchi wanachama kuondoa aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake na kuhakikisha

---

[193] Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto wa Mwaka 1990 36804-treaty-african_charter_on_rights_welfare_of_the_child.pdf (au.int)

[194] Amnesty International The Protocol on the Rights of Women in Africa: Strengthening the promotion and protection of women's human rights in Africa inapatikana The Protocol on the Rights of Women in Africa: Strengthening the promotion and protection of women's human rights in Africa (amnesty.org)

fursa sawa inapatikana katika nyanja ya elimu na mafunzo. Vile vile, Ibara hii inazitaka nchi wanachama kuondoa dhana potofu zote zilizomo katika vitabu, mitaala na vyombo vya habari vinavyoendeleza ubaguzi dhidi wa wanawake katika kupata elimu. Pia, Mkataba huu umezitaka nchi wanachama kuweka mikakati ya kuwalinda wanawake hasa watoto wa kike dhidi ya aina zote za unyanyasaji wa kijinsia maskulini pamoja na kutoa adhabu kwa wanaofanya vitendo hivyo.[195]

### 5.3.4 Mkataba wa Vijana wa Kiafrika wa mwaka 2006.

Mkataba wa Vijana wa Kiafrika ulipitishwa mwaka 2006 kwa lengo la kuweka mfumo wa kimkakati wa kuwawezesha vijana katika shughuli za maendeleo katika ngazi zote zikiwemo za kitaifa, kikanda na Bara la Afrika.[196] Vile vile, Mkataba huu unashughulikia masuala muhimu yanayowahusu vijana ikiwa ni pamoja na ajira, elimu maendeleo ya ujuzi, afya, ushirikishwaji wa vijana, amani na usalama, usimamizi wa sheria, vijana wanaoishi nje ya nchi na vijana wenye ulemavu.[197]

Aidha, Ibara ya 13 ya Mkataba huu inazitaka nchi wanachama kuhakikisha kuwa vijana wa Kiafrika wanapatiwa haki ya kupata elimu iliyo bora. Pia, nchi wanachama zinatakiwa kuchukua hatua zote zinazofaa kwa lengo la kufikia upatikanaji wa haki ya elimu ikiwemo hatua ya kuhakikisha kuwa elimu ya msingi ni ya lazima kwa kila mtoto na inatolewa bila ya malipo; vile vile, nchi wanachama zinatakiwa kuhakikisha zinaondoa gharama zisizokuwa za lazima

[195] Ibid, Ibara ya 12
[196] African Youth Charter | Library | Youthpolicy.org
[197] ibid

katika upatikanaji wa elimu pamoja na kuweka mikakati ya kuinua mahudhurio na kupunguza utoro skuli.[198]

### 5.3.5 Dira ya Umoja wa nchi za Afrika Mashariki 2050

Dira ya 2050 inatambua kuwa vizazi vijavyo ni walinzi wa baadaye na kwa hivyo, hitaji la ubora na upatikanaji wa elimu zaidi ya kiwango cha msingi, viwango vya uandikishaji wa sekondari na ukamilishaji vitaongezeka zaidi ya asilimia 90 katika kipindi cha Dira ya 2050.[199]

Mfumo wa Elimu wa EAC utakuwa na mantiki ya kuanzisha uhusiano mkubwa kati ya viwango vya elimu ya juu, ufundi, sekondari, msingi na kutakuwa na mitaala yenye viwango vya kawaida ambavyo vinatambuliwa ili kuendeleza upatikanaji wa ajira na mahitaji ya sekta kwa kutumia teknolojia.[200]

### 5.3.6 Sera ya Elimu ya Umoja wa Nchi za Afrika Mashariki (EAC) 2016

Sera ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inabainisha kuwa utoaji wa elimu bora ya msingi na ya juu bado ni msingi wa maendeleo ya mtaji wa watu katika ukanda wa Afrika Mashariki.[201] Maeneo mahususi yafuatayo yalitolewa katika nyaraka mbalimbali za Sera kama ifuatavyo;

(a) Kutayarisha programu za pamoja katika elimu ya msingi, ya Sekondari na Elimu ya juu na program ya jumla ya elimu ya watu wazima na endelevu katika nchi wanachama;

[198] Ibid, Ibara ya 13
[199] Ukurasa wa 80
[200] ibid
[201] Sera ya Jumuiya ya Afrika Mashariki Ukurasa wa 10

(b) Kuhimiza na kuunga mkono ushiriki wa sekta binafsi katika maendeleo ya rasilimali watu kupitia elimu na mafunzo
(c) Kuanzisha mabadiliko ya mikakati ya elimu na mafunzo ili kuwezesha wanawake kukuza viwango vyao vya ajira za kitaalam na viwadani;
(d) Kubadilishana taarifa na uzoefu kuhusu masuala yanayofanana katika mifumo ya elimu ya nchi wanachama;
(e) Kuainisha mitaala, mitihani uthibitishaji wa taasisi ya elimu na mafunzo katika nchi wanachama kupitia hatua za pamoja za vyombo vya kitaifa vinavyohusika na utayarishaji wa mitaala;
(f) Kushirikiana katika kuweka program za elimu na mafunzo kwa watu wenye mahitaji maalumu na wasiojiweza.

## 5.4 Uzoefu wa nchi mbalimbali

### 5.4.1 Sheria ya Elimu ya Shelisheli (Seychelles) Nam. 13 ya Mwaka 2004

Nchi ya Shelisheli imetunga Sheria ya Elimu Namba 13 ya Mwaka 2004 kwa ajili ya kuweka utaratibu mzuri wa kusimamia sekta ya elimu nchini humo. Mambo muhimu yaliyomo katika Sheria hii ni kama yafuatayo:

#### (a) Usimamizi na uangalizi wa skuli za Serikali

Sheria hii ya Elimu ya Shelisheli imeipa mamlaka Wizara husika kusimamia skuli zote za Msingi na Sekondari za Serikali.[202] Vile vile, Sheria hii imeorodhesha mfumo mzima wa elimu inayotolewa na Serikali ambayo inajumuisha elimu ya awali; elimu ya msingi; elimu ya sekondari; elimu baada

[202] Sheria ya Elimu ya Shelisheli Kifungu cha 9 (1)

ya sekondari; na elimu ya juu.[203] Aidha, Waziri anaweza kuongeza elimu nyengine kuwa katika mfumo wa elimu ya Serikali kama vile elimu ya watu wazima na elimu ya masafa marefu (*online education*), elimu maalumu pamoja na elimu ya utotoni isiyo rasmi.[204]

### (b) Uwezo na wajibu wa Waziri

Sheria hii imempa uwezo Waziri wa elimu kuanzisha taasisi za elimu ambazo zinatoa elimu baada ya elimu ya sekondari pamoja uwezo wa kuanzisha taasisi nyingine za elimu ya juu katika maeneo ambayo Waziri ataona ipo haja ya uwepo wa taasisi hizo katika maeneo hayo.[205]

Aidha, Sheria hii imempa wajibu Waziri katika nyanja mbali mbali ikiwemo wajibu wa kuanzisha skuli za msingi na sekondari za Serikali katika eneo ambalo Waziri ataona linafaa kuanzishwa skuli hizo.[206]Pia, kusimamia uandiskishwaji wa wanafunzi katika skuli za Serikali pamoja na kuanzisha, kuziendeleza na kusaidia kuanzisha na kuendeleza taasisi za elimu ikiwemo vyuo vya walimu, taasisi za kiufundi pamoja na taasisi za mafunzo ya mali.[207]

### (c) Malengo na madhumuni ya mfumo wa elimu

Kwa kutambua umuhimu wa elimu, Sheria hii ya Shelisheli imeweka malengo makuu na madhumuni ya mfumo mzima wa elimu wa nchini humo na unasimamiwa na Waziri husika.[208]

---

[203] Ibid, kifungu cha 11
[204] Ibid
[205] Kifungu cha 10
[206] Ibid kifungu cha 5
[207] ibid
[208] Ibid, kifungu cha 3 (1)

Malengo na madhumuni hayo yaliyoainishwa katika sheria hii ni kuanzishwa kwa mfumo imara wa elimu na mafunzo yanayoendana na viwango vya kimataifa na misingi ya kitaifa, ambayo yatapelekea kumkuza mtu na kumjengea uwezo wa kushiriki kikamilifu kwenye maendeleo ya kijamii na kiuchumi pamoja na kujenga taasisi ambazo zitawezesha kufikiwa kwa malengo hayo.[209] Aidha, lengo kuu jengine la mfumo wa elimu wa Shelisheli ni kutekeleza sera ya elimu ya Serikali.[210]

**(d) Kuanzishwa kwa programu maalum kwa watoto wenye mahitaji maalum.**

Sheria hii imemtaka Waziri kuanzisha programu maalumu za masomo kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum ambao wamefikia umri wa kwenda skuli.[211] Aidha, Sheria hii imezitaka programu hizi za mafunzo zinazotolewa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu kutolewa bila ya vikwazo na katika mazingira rafiki.[212]

**(e) Haki na wajibu wa wanafunzi na wazee**

Sheria hii imetoa haki kwa kila mtu ya kupata elimu inayofaa kwa mujibu wa mahitaji yake.[213] Vile vile, Sheria hii imetoa wajibu kwa Katibu Mkuu kumpatia elimu kila mkaazi wa Shelisheli ambae amefikia umri wa kuanza skuli.[214]Wajibu huu unajumuisha kumuandikisha kila mtoto ambae amefikia umri wa lazima wa kuanza masomo pamoja na kumpangia mtoto yeyote katika

[209] Kifungu cha 3(2)
[210] ibid
[211] Ibid, kifungu cha 15
[212] ibid
[213] Ibid, kifungu cha 40
[214] ibid

skuli ambayo Katibu Mkuu ataona inamfaa mwanafunzi huyo kupata elimu anayostahiki.[215]

Pia, Sheria hii imetoa haki kwa wanafunzi kupata elimu ya msingi na sekondari bila ya malipo yoyote, isipokua Waziri anaweza kuridhia kuanzishwa kwa michango mbali mbali ya kusaidia skuli.[216]

Aidha, Sheria hii imetoa wajibu kwa kila mwanafunzi aliyeandikishwa katika Skuli ya Serikali au taasisi ya elimu kuzingatia kanuni za maadili na sheria nyengine zilizowekwa na Waziri pamoja na zile zilizowekwa na skuli, kuhudhuria skuli kila siku na kwa wakati pamoja na kufanya bidii katika masomo yake. [217]

Vile vile, kwa mujibu wa Sheria hii, kila mwanafunzi atawajibika kwa mwalimu, mkufunzi, au mtu yeyote ambaye ameruhusiwa kwa vitendo vyote vya mwanafunzi ambavyo atafanya ndani ya skuli na muda wa skuli wakati mwalimu au msimamizi huyo akiwa anasimamia darasa ambalo mwanafunzi huyo anasoma au kwa vitendo vyote ambavyo mwanafunzi atafanya nje ya skuli kwa shughuli ambazo skuli imeridhia.[218]

Aidha, Sheria hii imeweka wajibu kwa wazazi kuhakikisha watoto wao wenye umri wa lazima wa kusoma wanakwenda skuli kila siku.[219] Katika kuhakikisha wazazi wanatekeleza wajibu wao huu, Waziri anaweza kumteua mtendaji

[215] ibid
[216] Ibid, kifungu cha 42
[217] Ibid, kifungu cha 42
[218] Ibid, kifungu cha 44
[219] Ibid, kifungu cha 57

yeyote katika skuli kuwa afisa mahudhurio ambaye atakuwa na jukumu la kuwasimamia wazazi ambao hawatimizi jukumu lao kwa kumfuatilia mtoto mwenye umri wa lazima wa kwenda skuli pahala anapokwenda au kumchunguza iwapo mtoto huyo anafanya kazi badala ya kwenda skuli au kumsimamisha na kumuuliza mtoto yeyote ambaye anaonekana kuwa na umri wa lazima wa kwenda skuli lakini hayupo skuli.[220]

**(f) Haki na wajibu wa walimu:**

Sheri hii imetowa haki na wajibu kwa walimu na imeelezea wajibu wa mwalimu mkuu. Baadhi ya haki za walimu zilizoainishwa katika sheria hii ni haki ya kuwekewa mazingira mazuri ya kufanyia kazi zake kadri itakavyowezekana, kupatiwa vifaa vya kutosha vya kufanyia kazi yake kadri itakavyowezekana, kulindwa dhidi ya unyanyasaji, kulindwa dhidi ya kushambuliwa wakati akiwa kazini pamoja na kupatiwa fursa za masomo na kujiendeleza kielimu.[221]

Aidha, kwa mujibu wa Sheria hii walimu wana wajibu mbali mbali ikiwemo wajibu wa kufuata sheria na kanuni zilizopo pamoja na kufuata maelekezo kutoka kwa Mwalimu Mkuu au maelekezo kutoka kwa Mkurugenzi wa elimu.[222] Vile vile, mwalimu anawajibu wa kufundisha kwa bidii na uaminifu, kufanya tathmini za wanafunzi pamoja na kutunza rejista na kumbukumbu za wanafunzi kwa ajili ya ukaguzi.[223]

[220] Ibid, kifungu cha 60
[221] Ibid, kifungu cha 72
[222] Ibid, kifungu cha
[223] Ibid, kifungu cha 74 (1)

Vile vile, Sheria hii imeweka wajibu kwa mwalimu mkuu ukiwemo wajibu wa kufuata sheria na kanuni, wajibu wa kusimamia na kuwaelekeza walimu, wahadhiri wakufunzi pamoja na wafanyakazi wengine waliojitolea katika skuli hiyo n.k.[224]

### 5.4.2 Jamhuri ya Singapore

Jamhuri ya Singapore imetunga Sheria mbali mbali ambazo zinasimamia sekta nzima ya elimu nchini humo. Baadhi ya Sheria hizo ni Sheria ya Elimu ya Singapore ya Mwaka 1957 na Sheria ya Elimu ya Lazima ya Mwaka 2000.

#### 5.4.2.1 Sheria ya Elimu ya Jamhuri ya Singapore ya Mwaka 1957.

Katika kuweka usimamizi kwenye sekta ya elimu, nchi ya Singapore ilipitisha Sheria ya Elimu ya Jamhuri ya Singapore ya Mwaka 1957 ambayo inasimamia elimu na usajili wa skuli. Mambo muhimu yaliyomo katika Sheria hii ni kama ifuatavyo:

**(a) Kuanzishwa kwa Bodi ya Fedha ya Elimu.**

Sheria hii imeanzisha Bodi ya Fedha ya Elimu ya Singapore ambayo wajumbe wake ni Mkurugenzi Mkuu ambaye atakuwa Mwenyekiti, Katibu Mkuu kutoka Wizara ya fedha ambaye ni mjumbe wa kudumu, na wajumbe wengine wanne ambao sio wafanyakazi wa Serikalini na sio Wabunge ila watatoka katika taasisi na jumuiya za elimu ambao watateuliwa na Waziri anayehusika na elimu.[225]

---

[224] Ibid, kifungu cha 76 (1)

[225] Sheria ya Elimu ya Singapore ya Mwaka 1957, kifungu cha 6.

Bodi hii ina jukumu la kumshauri Waziri anayehusika na elimu juu ya usimamizi wa mali zote au fedha zilizochangiwa au kutolewa na Serikali kwa ajili ya elimu. Vile vile, Bodi hii ina jukumu la kuyapitia makadirio ya matumizi ya mwaka ya elimu ambayo yametayarishwa na Mkurugenzi Mkuu na kumshauri Waziri wa elimu juu ya makadirio hayo.[226] Aidha, Sheria hii imemtaka Waziri husika kutengeneza kanuni kwa ajili ya kuweka utaratibu mzuri wa kiutendaji wa Bodi hii ya Fedha.[227]

**(b) Kuanzishwa kwa Baraza la Ushauri la Elimu.**

Sheria hii imeanzisha Baraza la Ushauri la Elimu[228] ambalo wajumbe wake ni Mkurugenzi Mkuu, Wajumbe wote wa Bodi ya Fedha, Daktari anafanya ukaguzi kwa wanafunzi maskulini, Mkurugenzi Mkuu wa Ustawi wa Jamii, Wajumbe nane ambao watateuliwa na Jumuiya au taasisi za Elimu ikiwemo Jumuiya ya Walimu ambao watakubaliwa na Waziri, na Wajumbe wengine sita ambao watateuliwa na Waziri.[229] Vile vile, wajumbe wa Baraza hili watashika nafasi hii kwa muda wa miaka mitatu na Baraza hili litakutana angalau mara nne kwa mwaka katika mwezi wa Machi, Juni, Septemba na Disemba na pia wanaweza kukutana zaidi ya muda huo iwapo wataona inafaa. [230]

Aidha, kazi za Baraza hili ni kumshauri Waziri juu jambo lolote linalohusiana na sera ya elimu au jambo la maendeleo ya elimu. Baraza hili litafanya kazi yake ya kushauri baada ya kupata maelekezo kutoka kwa Waziri au Baraza litatoa

[226] ibid
[227] Ibid, Kifungu cha 8
[228] Ibid, kifungu cha 9 (1)
[229] Ibid, kifungu cha 9 (2)
[230] ibid

ushauri bila ya maelekezo kutoka kwa Waziri iwapo litaona suala hilo ni muhimu kushauriwa Waziri.[231]

Sambamba na hayo, Baraza la Ushauri limepewa uwezo wa kuanzisha Kamati ndogo ndogo ambazo zitafanya kazi kwa lengo maalumu. Kamati hizo zitaundwa na baadhi ya wajumbe kutoka katika Baraza la Ushauri, na wajumbe wengine kutoka nje ya Baraza kama Baraza litakavyoona inafaa baada ya kushauriana na kupata ridhaa kutoka kwa Waziri wa elimu.[232]

### (c) Kuanzishwa kwa Bodi ya Rufaa.

Sheria hii imeanzisha Bodi ya Rufaa (*Schools Appeals Board*)[233] ambayo wajumbe wake huchaguliwa na Waziri. Wajumbe hao ni Mwenyekiti ambaye atakuwa sio mfanyakazi wa Serikali, wajumbe wawili kutoka Taasisi za Elimu ya Juu, walimu wawili waliosajiliwa wasiotoka Skuli za Serikali, Wakurugenzi wawili ambao wamesajiliwa na wajumbe wengine wawili ambao watachaguliwa na Waziri.[234] Wajumbe wa Bodi hii wanafanya kazi kwa muda wa miaka mitatu.[235]

Aidha, Bodi hii ya rufaa itakuwa na jukumu la kusikiliza rufaa zinazotokana na maamuzi yaliyotolewa na Mkurugenzi Mkuu. Aidha, Bodi hii haina uwezo wa kusikiliza rufaa ya walimu wa Serikali isipokuwa rufaa ya walimu ambayo inayohusiana na kupinga kufutwa kwa usajili wake wa ualimu.[236]Vile vile,

---

[231] Ibid kifungu cha 9.
[232] Ibid, kifungu cha 12
[233] Ibid, kifungu cha 13 (1)
[234] Ibid kifungu cha 13(2).
[235] Ibid, kifungu cha 13 (4)
[236] Ibid kifungu cha 15.

katika utendaji wa kazi zake, Bodi hii imepewa uwezo wa kufanya ukaguzi, kuingia na kutazama eneo lolote la skuli.[237]

**(d) Usajili wa Skuli, Wakurugenzi na Walimu.**

Mkurugenzi Mkuu ana wajibu wa kuwa na madaftari ya usajili mbali mbali ikiwemo daftari la usajili wa kila skuli, kila mkurugenzi au msimamizi wa skuli iliyosajiliwa, daftari la usajili la kila mwalimu aliyesajiliwa pamoja na daftari la usajiili kwa walimu ambao hawakusajiliwa lakini wameruhusiwa kufundisha.[238]

**(e) Usajili wa Skuli.**

Sheria hii ya Singapore imekataza kuendesha Skuli bila ya kusajiliwa.[239] Aidha, Mkurugenzi Mkuu ana wajibu wa kusajili skuli zote za Serikali.[240] Kwa upande wa skuli binafsi, Wakurugenzi wa skuli binafsi wanatakiwa kupeleka maombi ya usajili kwa Mkurugenzi Mkuu, ambapo Mkurugenzi Mkuu anaweza kukubali maombi hayo kwa masharti au bila ya masharti. Vile vile, Mkurugenzi Mkuu anaweza kukataa maombi yaliyowasilishwa kwake juu ya usajili wa skuli binafsi na atalazimika kutoa sababu za kukataa maombi ya usajili wa skuli hiyo.[241]

Aidha, Sheria hii imeainisha vigezo mbali mbali ambavyo vitapelekea skuli kutokusajiliwa na Mkurugenzi Mkuu. Baadhi ya vigezo hivyo ni kama iwapo eneo ambalo linatarajiwa kufunguliwa skuli limeshakuwa na skuli nyingi na za

---

[237] Ibid, kifungu cha 16
[238] Ibid kifungu cha 19(1)na (2)
[239] Ibid kifungu cha 21
[240] Ibid, kifungu cha 22
[241] ibid, kifungu cha 22 (2).

kutosha au jengo ambalo linatarajiwa kutumika kama skuli linaweza kusababisha hatari au muundo wake haufai kutumika kama skuli.[242]

**(f) Kufutwa kwa usajili wa skuli.**

Sheria hii imeainisha mazingira ambayo yatapelekea Mkurugenzi Mkuu kufuta usajili wa skuli. Mazingira hayo yanajumuisha skuli kutokusimamiwa vyema, kutokuwepo kwa skuli tena, na iwapo skuli imeshindwa kusimamia masuala ya nidhamu.[243]

**(g) Kamati za Uongozi**

Sheria hii imezitaka skuli zote zisizokua za Serikali kuongozwa na Kamati za Uongozi za Skuli.[244] Kamati hizi zitakuwa na wakurugenzi wasiozidi tisa na zina jukumu la kuhakikisha kuwa skuli inafuata sheria ya elimu, miongozo pamoja na taratibu za usajili zilizowekwa na Sheria.[245] Aidha, Sheria hii imempa uwezo Mkurugenzi Mkuu kuteuwa mkurugenzi mwengine wa skuli au kuongeza idadi ya wakuregenzi wa skuli iwapo ataona skuli husika haina usimamizi mzuri.[246] Vile vile, Kamati ya Uongozi itachagua mjumbe mmoja kuwa ndiye msimamizi wa skuli ambaye atawasilisha taarifa za skuli kwa Mkurugenzi Mkuu.[247]

**(h) Wakaguzi wa Skuli**

Sheria hii imempa uwezo Waziri husika kuteuwa maafisa mbali mbali kuwa wakaguzi wa skuli katika maeneo tofauti akiwemo afisa yeyote kutoka Wizara

---

[242] ibid, kifungu cha 24
[243] ibid, kifungu cha 25
[244] Ibid, kifungu cha 26
[245] ibid
[246] Ibid
[247] Ibid, kifungu cha 28 na 29

ya Elimu kuwa mkaguzi wa skuli, afisa yeyote kutoka sekta ya afya kuwa afisa wa afya wa maskulini (*Medical Officer*) pamoja na afisa anayehusika na masuala ya afya ya jamii kuwa mkaguzi wa afya ya jamii (*public health inspector*).[248] Aidha, Sheria hii imempa wajibu Mkurugenzi Mkuu kuhakikisha kuwa ukaguzi unafanyika kwa kipindi maalum angalau mara moja kwa mwaka kwa skuli zote zilizosajiliwa.[249] Lengo la ukaguzi huo ni kuhakikisha kuwa masharti ya Sheria ya Elimu yanatekelezwa pamoja na kuhakikisha kuwa skuli zinasimamiwa ipasavyo.[250]

**(i) Adhabu**

Sheria hii imeweka makosa mbali mbali na adhabu zake ikiwemo kosa la kufungua skuli au kufanya kazi bila ya kusajiliwa, kusomesha bila ya kusajiliwa, kumzuia Mkurugenzi Mkuu kufanya kazi zake na mengineyo. Iwapo mtuhumiwa atatiwa hatiani kwa kosa lolote kati ya hayo, adhabu yake itakuwa ni faini ya dola 2,000 au kifungo kisichozidi mwaka mmoja.[251] Aidha, Sheria hii imeweka adhabu kwa ujumla kwa makosa yote yatakayofanywa iwapo adhabu hazijawekwa, basi adhabu itakayotumika ni ya faini ya dola mia tano(500$) kwa kosa la kwanza na iwapo atarudia kosa hilo, adhabu itakuwa ni faini ya dola elfu moja(1000$).[252]

#### 5.4.2.2 Sheria ya Elimu ya Lazima ya Jamhuri ya Singapore ya Mwaka 2000

[248] Ibid, kifungu cha 51
[249] Ibid, kifungu cha 52
[250] Ibid
[251] Ibid, kifungu cha 62 (1)
[252] Ibid

Nchi ya Singapore imeanzisha Sheria ya Elimu ya lazima ya mwaka 2000 ambayo inasimamia utoaji wa elimu ya msingi ambayo ni ya lazima nchini Singapore.[253] Sheria hii imetafsiri mtoto mwenye umri wa kulazimika kusoma ni mtoto yeyote mwenye umri wa zaidi ya miaka sita na hajafikia umri wa miaka 15.[254]

Aidha, Sheria hii imemtaka mtoto yeyote mwenye umri wa kulazimika kusoma na amezaliwa baada ya tarehe 1 Januari, 1996, akiwa raia wa Singapore na mkaazi wa nchi hiyo, basi atalazimika kuwa mwanafunzi na kwenda skuli kila siku.[255] Aidha, Sheria hii imetoa adhabu kwa mzazi ambaye mtoto wake yupo katika umri wa lazima wa kusoma na ikawa mtoto huyo haendi skuli.[256]

### (a) Bodi ya elimu ya lazima:

Kupitia Sheria hii, Singapore imeanzisha Bodi ya ELimu ya Lazima ambayo wajumbe wake huteuliwa na Waziri anayehusika na elimu.[257] Bodi hii ina majukumu ya kuchunguza iwapo masharti ya Sheria hii yanatekelezwa au yamekiukwa, kutoa mapendekezo kwa Mkurugenzi Mkuu kuhusu utekelezaji wa Sheria hii pamoja na kufanya mambo yote yanayoelezwa katika Sheria hii.[258]

Aidha, Bodi hii imepewa uwezo wa kusikiliza mashahidi, kumwita mtu yeyote katika kikao cha Bodi kwa lengo la kutoa ushahidi, vile vile kumtaka mtu yeyote kutoa hati yeyote ya ushahidi pamoja na kumtaka mtu yeyote kuhudhuria kikao

---

[253] Sheria ya Elimu ya Lazima ya SIngapore ya Mwaka 2000
[254] Ibid, kifungu cha 2
[255] Ibid, kifungu cha 3 (1)
[256] Ibid, kifungu cha 3 (2)
[257] Ibid, kifungu cha 5
[258] Ibid, kifungu cha 6

cha usuluhishi kinachofanywa na Bodi hii.[259] Vile vile, Sheria hii imempa uwezo Waziri wa kutoa maelekezo yoyote juu ya utekelezaji wa kazi za Bodi hii na Bodi italazimika kufuata maelekezo ya Waziri.[260]

### 5.4.3 Sheria ya Elimu ya Kenya Sura 211

Nchi ya Kenya imetunga Sheria ya Elimu Sura ya 211 kwa lengo la kusimamia na kuendeleza elimu nchini humo. Sheria hii imeweka misingi katika sekta ya elimu nchini Kenya na baadhi ya misingi hiyo ni:

#### (a) Baraza la Ushauri.

Sheria hii imempa uwezo Waziri wa elimu kuanzisha Baraza la ushauri kwa lengo la kumshauri juu ya jambo lolote linalohusu elimu nchini Kenya.[261] Baraza hili la ushauri litakuwa na wajumbe wasiopungua kumi na wasiozidi ishirini.[262]

Aidha, Sheria hii imempa uwezo Waziri wa elimu kuteua Mabaraza ya Ushauri katika maeneo mbali mbali au kuanzisha Mabaraza hayo kwa ajili ya ushauri wa eneo maalum katika sekta ya elimu.[263]

#### (b) Usimamizi wa skuli

Kwa mujibu wa Sheria hii skuli zote za msingi zilizopo chini ya Serikali za Mitaa zitasimamiwa na Serikali za Mitaa. Aidha, kwa  skuli za msingi ambazo hazipo

[259] Ibidi, kifungu cha 6 (2)
[260] Ibid, kifungu cha 6 (3)
[261] Sheria yaElimu ya  Kenya Sura ya 211, kifungu cha 4 (1)
[262] Ibid, kifungu cha 4 (2)
[263] Ibid, kifungu cha 4 (1)

chini ya Serikali za Mitaa zitasimamiwa na Bodi ya Gavana au kama Wazri atakavyoelekeza.[264]

**(c) Kamati za Skuli**.

Sheria hii imetowa uwezo kwa Serikali za mitaa kuanzisha Kamati za skuli kwa kila skuli ya msingi inayotunzwa na kusimamiwa na mamlaka ya serikali za mitaa. Kamati hizi zitakuwa na kazi ya kushauri Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuhusu masuala yanayohusu usimamizi wa skuli.[265]

Aidha, wajumbe wa kamati hizo za skuli wanateuliwa na Mamlaka za Serikali za mitaa na miongoni mwa wajumbe wa kamati hio ni wadhamini ambao wanasaidia skuli hizo.[266]

**(d) Usajili wa Skuli Binafsi**

Sheria hii imempa uwezo Waziri wa elimu kusajili skuli na kuhifadhi usajili na kutowa usajili huo kwa ajili ya kufanya ukaguzi muda wowote pale ambapo kutakuwa kuna haja ya kufanya hivyo.[267] Aidha, Waziri husika amepewa uwezo wa kufunga skuli binafsi iwapo ataona hazifuati masharti yaliyowekwa katika Sheria au iwapo mazingira hayatokua mazuri, n.k.[268]

**(e) Maombi ya kusajiliwa**.

---

[264] Ibid, kifungu cha 6
[265] Ibid, kifungu cha 9(1).
[266] Ibid, kifungu cha 9(2)
[267] Ibid, kifungu cha 13.
[268] Ibid, kifungu cha 16

Sheria hii imeweka utaratibu wa usajili wa skuli binafsi ambao ni kwa kupeleka maombi kwa Waziri ya kutaka skuli binafsi isajiliwe.[269] Aidha, katika usajili huo muombaji anatakiwa aambatanishe daraja ambalo anastahiki kusajiliwa.[270]

**(f) Taasisi ya Elimu ya Kenya**

Sheria hii imeanzisha Taasisi ya Elimu ya Kenya yenye jukumu la kuratibu taasisi zinazojishughulisha na mafunzo ya walimu, uendeshaji wa mitihani ili kuwawezesha kupata walimu wenye sifa, uendeshaji na uendelezaji wa utafiti wa elimu, kutayarisha vifaa kwa ajili ya mafunzo ya walimu pamoja na kuendeleza maendeleo ya elimu na mafunzo.[271]

Aidha, Waziri wa Elimu ndiye atakayehusika kuipangia kazi na uwezo wa taasisi hii pamoja na usimamizi wake katika utekelezaji wa kazi zake.[272]

**(g) Bodi za Elimu za Wilaya**

Sheria hii imeanzisha Bodi za Elimu za Wilaya ambazo zitakuwa katika Wilaya yoyote au eneo jengine.[273] Bodi hizi zinaanzishwa na Waziri baada ya kutangazwa katika Gazeti rasmi la Serikali.[274]

Aidha, Bodi hii itakuwa na wajumbe wasiopungua kumi na wasiozidi kumi na tano ambao watateuliwa na Waziri kwa kutumia vigezo mbali mbali.[275]

---

[269] Ibid, kifungu cha 14
[270] Ibid
[271] Ibid, kifungu cha 23 (1)
[272] Ibid, kifungu cha 23 (2)
[273] Ibid, kifungu cha 28
[274] ibid
[275] Ibid, kifungu cha 29

**(h)** U**kaguzi wa Skuli.**

Sheria hii imempa uwezo Waziri wa kumchaguwa afisa ambae atakuwa na jukumu la kufanya ukaguzi katika skuli.[276] Mkaguzi huyu amepewa uwezo wa kufanya ukaguzi muda wowote katika majengo ya skuli na kutoa ripoti kwa Waziri.[277] Aidha, ukaguzi huo unajumuisha pamoja na ukaguzi wa hesabu za skuli ili kuangalia mienendo ya kifedha katika skuli husika.[278]

### 5.4.4 Sheria ya Elimu ya Msingi ya Finland Nam. 628 ya Mwaka 1998

Sheria hii ya Elimu ya Msingi ya Finland ndio inayosimamia elimu ya msingi nchini humo. Mambo muhimu yaliyomo katika Sheria ni:

**(a) Kutambulika kwa wadau wengine wa elimu**

Sheria imetambua wadau wengine na taasisi zinazotoa elimu kwa skuli mbalimbali. Taasisi hizi zimetakiwa kutoa elimu kwa ruhusa na masharti maalum na kwa kuzingatia utamaduni wa nchi.[279] Ruhusa hiyo inaeleza maeneo ya kutolewa elimu, lugha ya kufundishia, elimu maalum iliyolengwa, na masharti mengine kwa mujibu wa sheria ya Elimu.[280]

Vile vile, Sheria imetamka kwamba Serikali inaweza kusitisha kibali na idhini iliyotolewa ikiwa elimu itakayotolewa haitakidhi masharti ya sheria hiyo au Sheria nyengine inayohusika na masuala yanayofundishwa.[281]

---

[276] Ibid, kifungu cha 18
[277] Ibid
[278] Ibid
[279] Sheria ya Elimu ya Msingi ya Finland Nam. 628 ya Mwaka 1998, Sura ya 3, Kifungu cha 7 (1)
[280] Ibid, kifungu cha 7(3)
[281]Ibid, kifungu cha 7(4)

Aidha, Taasisi inayotoa elimu imetakiwa kuzingatia mitaala iliyopo, ingawa mtaala unaweza kubadlishwa katika baadhi ya maeneo kwa kushauriana na Serikali za mitaa na taasisi za ustawi wa jamii na afya. Aidha, taasisi ya kutoa elimu inatakiwa kueleza jinsi Watoto watakavyonufaika na mtaala huo.[282]

**(b) Tathmini ya elimu**

Sheria inataka kufanywa tathmini ya elimu inayotolewa ili kusaidia maendeleo ya elimu na kuongeza uwezo wa wanafunzi.[283] Elimu hiyo inatakiwa kutathminiwa kwa kuzingatia elimu inayotolewa na athari zake, na kujumuisha tathmini ya nje ya utekelezaji wake.[284]

Kwa kuzingatia tathmini ya nje, Sheria imeanzisha Baraza la Tathmini chini ya wizara ya elimu kama taasisi inayojitegemea. Baraza hili limepewa kazi ya kusimamia tathmini ya malengo na matokeo ya upatikanaji wa elimu kitaifa kama ilivyoelezwa kwa mujibu wa masaa ya ufundishaji na mitaala mikuu ya elimu. Wizara itaweka Mpango wa tathmini na usimamizi.[285] Sheria katika ibara ya 21(4) inataka matokeo ya tathmini kuchapishwa na maendeleo yake ambayo yatawekwa katika sheria maalum.[286]

**(c) Tathmini ya wanafunzi**

Sheria imeweka utaratibu wa wanafunzi kufanyiwa tathmini kwa lengo la kuwaongoza, kuhamasisha upatikanaji wa elimu na kuangalia uwezo wa

---

[282] Ibid, kifungu cha 15(1) na (2)
[283] Ibid, kifungu cha 21(1)
[284] Ibid,kifungu cha 21(2)
[285] Ibid, kifungu cha 21(3)
[286] Ibid, kifungu cha 21(5)

wanafunzi kwa kujitathmini wenyewe. Tathmini hii inajumuisha pia usomaji, kazi za mwanafunzi na tabia.[287]

Tathmini ya masomo na maendeleo ya mwanafunzi katika masomo itaongozwa na amri au kanuni maalum zitakazotolewa na Bodi ya Taifa ya Elimu na taarifa zitawekwa katika kadi maalum kama itakavyoelezwa na Bodi ya elimu.[288]

Iwapo wazazi watataka mtoto arudie mwaka kutokana na matokeo ya jumla, wazazi watapewa fursa ya kusikilizwa kabla ya kutoa maamuzi kwa mwanafunzi huyo.[289]

**(d) Umri wa Watoto kuanza skuli**

Sheria imeweka umri wa miaka saba kwa mtoto kuanza skuli kwa lazima[290] na ruhusa ya kuongeza muda imetolewa ikiwa mtoto atakuwa na matatizo ya kisaikolojia, ambayo taarifa za Daktari zimeshauri kuwa hatakuwa na uwezo wa kusoma. Mtoto huyo atakayekuwa na maelezo ya daktari lazima aanze skuli ndani ya mwaka mmoja unaofuata.[291]

**(e) Mazingira ya kusoma**

Sheria imeweka masharti ya kuhakikisha mazingira salama kwa wanafunzi kama haki ya msingi,[292] na kila skuli itatakiwa kuwa na mpango maalum kwa

---

[287] Ibid, kifungu cha 22(1)
[288] Ibid, kifungu cha 22(2)
[289] Ibid,Kifungu cha 22(3)
[290] Ibid,Kifungu cha 25(1)
[291] Ibid,Kifungu cha 27
[292] Ibid,Kifungu cha 29 (1)

kuzingatia mitaala iliyopo, kumlinda mtoto dhidi ya udhalilishaji na unyanyasaji. Wizara ya Elimu itaweka utaratibu wa kutayarisha mpango huo.[293]

Skuli zinatakiwa kuweka mwongozo na sheria ndogo ndogo za kufuatwa katika kuhamasisha usafi na usalama wa mazingira ya skuli.[294]

**(f) Nidhamu kwa wanafunzi**

Mwanafunzi yeyote atakayeathiri ufundishaji kwa kutokufuata maelekezo au kudanganya atawekwa kizuizini kwa muda usiozidi masaa mawili au atapewa onyo la maandishi. Ikiwa kosa alilofanya ni kubwa au ataendelea na tabia mbaya baada ya kupewa onyo la maandishi, atasimamishwa skuli kwa muda usiozidi miezi mitatu.[295]

Mwanafunzi ambaye ataingilia au kuzuia ufundishaji, atatolewa nje ya darasa au atatakiwa kuondoka eneo la skuli.[296]mwanafunzi anaweza kuzuiwa kuhudhuria skuli ikiwa baada ya skuli kufanya bidii ya kumkumbusha ataendelea na tabia mbaya au za hatari ambazo zitaathiri usalama wa wanafunzi wenziwe au vifaa vya kufundishia.[297]

Sheria inataka kabla ya hatua za kupewa barua ya onyo la maandishi au kumsimamisha mwanafunzi, kosa la mwanafunzi liwe limeelezwa vizuri, mwanafunzi awe amepewa fursa ya kusikilizwa, na uchunguzi umefanywa kuhusiana na kosa hilo. Wazazi na mamlaka ya skuli ijulishwe kuhusiana na

[293] Ibid,Kifungu cha 29(2)
[294] Ibid,Kifungu cha 29(3)
[295] Ibid,Kifungu cha 36(1)
[296] Ibid,Kifungu cha 36(2)
[297] Ibid,Kifungu cha 36(3)

hatua zilizochukuliwa dhidi ya mwanafunzi aliyesimamishwa na taarifa iwe imerikodiwa.[298] Kifungu hiki kinataka kuwekwa mpango wa kumsaidia mwanafunzi aliyesimamishwa,[299] ingawa uamuzi wa kusimamishwa unatakiwa utekelezwe haraka ikiwa mwanafunzi ametumia vitisho kuhatarisha usalama wa wanafunzi wenziwe na kuna ushahidi wa vitendo vya vitisho.[300]

Sheria imemruhusu mwalimu mkuu au mwalimu husika kumuondoa mwanafunzi kwa lazima ikiwa hajaheshimu amri ya kufukuzwa au kutakiwa kuondoka skuli na hatua hii inatakiwa izingatie taratibu zilizowekwa katika matumizi ya nguvu.[301]

**(g) Mazingira ya wanafunzi wenye mahitaji maalum**

Sheria imeelekeza Wizara kuhakikisha skuli inaweka utaratibu wa kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalum, pamoja na miongozo ya kusaidia elimu kwa watu wenye mahitaji maalum.[302]

**(h) Usiri wa taarifa**

Sheria inakataza wajumbe wa Bodi za skuli, walimu walio katika mikataba chini ya kifungu cha 37, wafanyakazi wa ustawi wa jamii wa skuli husika, wataalamu wa saikolojia wa skuli, na walimu wanaojifunza; kutoa taarifa kwa watu wa nje kuhusu taarifa binafsi za wanafunzi, hali za kiuchumi au taarifa za familia zao.[303]

---

[298] Kifungu cha 36a kilichoingizwa katika marekebisho na sheria Nam. 4787 ya mwaka 2003
[299] 36a(2)
[300] Kifungu cha 36a(4)
[301] Kifungu cha 36b(1) na (3)
[302] Kifungu cha 39
[303] Kifungu cha 40(1)

Maafisa ustawi waliopo skuli wana haki ya kutoa taarifa za mwanafunzi kwa mwalimu na mamlaka zinazohusiana na elimu chini ya sheria hii kwa taarifa ambazo zina maelekezo kwa mwanafunzi.[304] Aidha, kwa idhini ya maandishi kutoka kwa mzazi au mwakilishi kisheria, maafisa hao wanaweza pia kutoa taarifa nyeti za mwanafunzi kwa ajili ya kupanga mipango ya skuli ya mwanafunzi huyo.[305]

**(i) Upatikanaji wa taarifa**

Katika utekelezaji wa majukumu yake, skuli inaweza kuomba taarifa Serikalini au katika mamlaka husika kwa ajili ya mipango ya elimu katika skuli husika. Ingawa wakati wa kuomba taarifa hizo, tathmini ya elimu na maendeleo ya elimu na takwimu muhimu ziwe zimetayarishwa na skuli husika.[306]

**(j) Malipo ya ada**

Maamuzi ya ulipaji ada na viwango vya kutozwa kwa wanafunzi yatafanywa na Wizara ya Elimu kwa kuzingatia sheria na vigezo vya ulipaji kwa Serikali Nam. 150 ya mwaka 1992.[307]

**(k) Uwekaji wa huduma za kusaidia wanafunzi**

Sheria imeweka masharti kwa skuli za msingi kuweka huduma nyengine kwa Watoto kama maktaba, eneo la kucheza na shughuli nyengine zinazohusiana na elimu ya msingi.

[304] Kifungu cha 40(2)
[305] Kifugnu cha 40(4)
[306] Kifngu cha 41(1) na (2)
[307] Kifungu cha 44

### (l) Jumuiya za wanafunzi

Sheria imeweka masharti ya kuanzishwa jumuiya za wanafunzi ambazo zitakuwa na lengo la kuendeleza ushirikiano na umoja baina ya wanafunzi, na kushirikisha wanafunzi katika masuala yanayowahusu.[308] Shughuli za jumuiya zitazingatia umri wa wanafunzi na mazingira yaliyopo skuli na skuli za karibu zinaweza kuwa na ushirikiano au jumuiya za pamoja na skuli nyengine.[309]

Iwapo skuli itashindwa kuanzisha jumuiya za wanafunzi kama ilivyoelezwa katika kifungu hiki, skuli itachukua juhudi zaidi ili wanafunzi wapatiwe fursa ya kutoa maoni yao katika masuala yanayohusu shughuli zao au jumuiya yoyote ambayo itahusisha wanafunzi kwa ujumla wao.[310]

## 5.4.5 Sheria ya Elimuya Grenada Nam. 21 ya 2002 [311]

Sheria hii imeutngwa ili kutoa huduma za elimu ndani ya nchi Grenada kwa ajili ya skuli za umma na skuli za binafsi na mambo mengine yanayohusiana na elimu.[312] Maeneo mbalimbali ya Sheria hii yanafafanuliwa hapo chini kama ifuatavyo:

### (a) Shabaha na Malengo.

Sheria imelenga kuanzisha mfumo wa elimu ulio na tofauti, uliojitosheleza na ulio bora, kukuza elimu kwa watu wa Grenada kwa kuanzisha taasisi za elimu ambazo zitakuza imani ya kiroho, utamaduni, maadili, na maendeleo ya

---

[308] Kifungu cha 41a(1)
[309] Kifungu cha 41a(2)
[310] Kifungu cha 41a(3)
[311] Sura ya 86
[312] Sheria ya Elimu ya Grenada Nam 21 ya 2002, sehemu ya Utangulizi

kiuchumi na jamii; na kuanzisha mfumo shirikishi wa elimu ulioandaliwa kwa mujibu wa Sheria.[313]

Sheria imekusudia kuhimiza kukuza elimu ya msingi na utaalam na ubunifu, kutoa nafasi ya uelewa wa sayansi na teknolojia katika jamii; kuweka misingi ya kujithamini kwa watu wote kupitia elimu endelevu na mazingira.[314]

Sheria imempa majukumu Waziri kubuni mfumo wa elimu ulio bora kadiri inavyowezekana ili kuhakikisha kwamba uwezo wa kiakili na kitaalam na maslahi ya wanafunzi yanapatikana, kuanzisha taasisi za elimu ya umma na kusaidia taasisi za elimu za kibinafsi kwa mujibu wa kanuni zilizowekwa chini ya Sheria hii.[315]

Aidha, Sheria imemtaka Waziri kuweka utaratibu wa udahili na uhamisho wa wanafunzi katika taasisi za elimu; kutathmini kazi ya taasisi za elimu kwa kuzingatia mitaala na kuweka masharti ya mtihani na upimaji wa wanafunzi.[316]

**(b) Ripoti ya Mwaka**.

Sheria imetoa wajibu kwa Waziri wa Elimu kuwasilisha ripoti ya mwaka katika ngazi za bunge kila itakapomalizika mwisho wa mwaka wa masomo.[317] Vilevile, Sheria hii pia imemtaka waziri kuwasilisha ripoti ya kila mwaka ambayo itasaidia katika kutekeleza majukumu yake na kumtathmini ikiwa hajafikia malengo yaliowekwa katika sekta ya elimu.

[313] Ibid,Kifungu cha 3(2)
[314] Ibid,Kifungu cha 3(3)
[315] Ibid,Kifungu cha 4(2)(a) –(c)
[316] Ibid,Kifungu cha 4(2)(d) –(h)
[317] Ibid,Ibid kifungu cha 6

**(c) Afisa Mkuu wa Elimu**

Sheria imetambua uwepo wa Afisa Mkuu wa Elimu,[318] ambaye atakuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa taasisi zote za elimu zinafuata masharti ya Sheria hii kwa maslahi ya umma, kuhakikisha kuwa taasisi za elimu za umma zinakuwa na vifaa vya kutosha, kusimamia masuala ya mitaala ya elimu na kuweka mpango ambao unakubalika kwa ajili ya kufanya tathmini kwa skuli na taasisi zote za elimu.[319]

**(d) Kuanzishwa kwa Baraza la Ushauri la Elimu**.

Baraza la Ushauri la Elimu limeanzishwa chini ya kifungu cha 9 na litakuwa na wajumbe wasiopunguwa kumi na nne ambao watachaguliwa na waziri kutoka katika vyuo na mabaraza mbali mbali na wengine kutoka katika chama cha walimu.[320]

Aidha, Baraza hilo litakuwa na jukumu la kumshauri Waziri wa Elimu katika mambo mbalimbali ikiwemo utayarishaji wa kanuni, mafunzo ya walimu na masuala mengine kama Waziri atakavyoelekeza.[321] Hata hivyo, Waziri hafungwi au kulazimika kufuata ushauri wa Baraza hilo.[322]

**(e) Wajibu wa wanafunzi.**

---

[318] Ibid,Kifungu cha 7(1)
[319] Ibid Kifungu cha 7(1),(2)(a),(b),(c)(d),(e) na (f)
[320] Ibid kifungui cha 9(1),(2),(3)na (4).
[321] Ibid,Kifungu cha 10
[322] Ibid,kifungu cha 12.

Sehemu ya Tatu ya Sheria inazungumzia haki na wajibu wa wanafunzi na wazazi, na kila mwanafunzi atakuwa na haki ya kupata fursa ya kusoma.[323] Kila mwanafunzi ambaye amesajiliwa katika tasisi za elimu za umma au taasisi binafsi za elimu, atawajibika kuzingatia kanuni za maadili za wanafunzi na sera nyengine za wanafunzi kama zilivyoainishwa na Wizara ya Elimu; kuhudhuria darasani kwa wakati; kushiriki katika programu za elimu ambazo mwanafunzi amepangiwa; kuwa na bidii katika kufuata mtaala uliowekwa; na kuwa na nidhamu katika mavazi, usafi na mwenendo wake kwa ujumla.[324]

Sheria imeeleza kwamba wanafunzi wanawajibika kwa mwalimu husika wakati wakiwa katika eneo la skuli na wakati wowote mwalimu anaposimamia wanafunzi au wakati wakishiriki katika shughuli za skuli zilizoidhinishwa ikiwa zinafanywa nje ya saa za skuli.[325]

Aidha, mwanafunzi atakuwa na wajibu kwa mwalimu mkuu katika kufuatilia mwenendo wake wakati wowote atakapokuwa chini ya usimamizi wa skuli na waalimu, na muda wowote unaotumika katika kusafiri kati ya skuli na sehemu anayoishi.[326]

Sheria imebainisha kwamba mwanafunzi anaposafiri kwa basi la skuli atakuwa chini ya uangalizi na udhibiti wa jumla wa dereva wa basi; na mtu yeyote ambaye wanafunzi wamewekwa chini ya usimamizi wake.[327]

---

[323] Ibid,Kifungu cha 16
[324] Ibid,Kifungu cha 17
[325] Ibid,Kifungu cha 18(1)(a)
[326] Ibid,Kifungu cha 18(1)(b)
[327] Ibid,Kifungu cha 18(2)

**(f) Haki na wajibu wa mzazi,**

Wazazi watakuwa na wajibu kwa mtoto aliye chini ya umri wa miaka 18, anayehudhuria masomo yake. Haki hizo zinajumuisha kufahamishwa maendeleo, tabia na mahudhurio ya mtoto wake; kujua na kufuatilia maelekezo kwa mtoto; kukata rufaa dhidi ya uamuzi wowote chini ya Sheria hii ambao unaathiri kwa kiasi kikubwa elimu, afya au usalama wa mtoto; na kushauriwa kuhusu uwekwaji au uanzishwaji wa programu yoyote maalum ya elimu inayomuhusu mtoto.[328]

Mzazi anaweza kushauriana na mwalimu mkuu kuhusu nidhamu ya mwanafunzi, na kutoa taarifa ya hali ya kiafya ya mtoto ikiwa inalazimika mwalimu mkuu kufahamishwa.[329] Wazazi na walimu wanaweza kuunda chama au kamati ya pamoja kwa lengo la kufuatilia maendeleo ya elimu ya mtoto kulingana na utaratibu utakaowekwa.[330]

**(g) Kamati za Skuli.**

Ikiwa katika taasisi ya elimu hakuna chama cha wazazi, mwalimu mkuu wa taasisi kwa kushirikiana na watumishi wengine, wataanzisha kamati za skuli ambazo zitajumuisha walimu, wazee wa wanafunzi na wanajamii. Kamati hizo baada ya kuundwa, zitaidhinishwa na Afisa Mkuu wa Elimu. Aidha, jukumu kubwa la kamati hizi ni kushauri uongozi wa skuli kwa mambo yoyote yanayohusiana na skuli sambamba na kufanya kazi yoyote ambayo itaagizwa na Afisa Mkuu wa Elimu.[331]

[328] Ibid,Kifungu cha 22(a) hadi (d)
[329] Ibid,Kifungu cha 22(2) na (3)
[330] Ibid, kifungu cha 24(1),(2),(3),(4),(5) na (6)
[331] Ibid, kifungu cha 25(1),(2),(3),(4),(5) na (6)

**(h) Mazingira ya kufungwa skuli**

Sheria imeainisha mazingira maalum yatakayopelekea skuli kufungwa kwa muda au moja kwa moja iwapo kutatokea majanga yatakayopelekea uharibifu au kimbunga, tetemeko la ardhi, moto, mafuriko, kuathirika majengo yanayotumiwa na skuli; kuzuka kwa ugonjwa wowote wa kuambukiza miongoni mwa wanafunzi; mahudhurio katika skuli au taasisi yoyote ya elimu ya umma yameanguka kiasi kwamba, kwa maoni ya Waziri, anahalalisha kufungwa kwa muda au moja kwa moja kwa skuliau taasisi hiyo.[332]

Waziri atalazimika kutoa taarifa na maelezo kwa walioathirika kwa kufungwa skuli hiyo pamoja na maelezo mbadala ya masomo yao.[333] Mamlaka aliyopewa Waziri na kifungu hiki ni nyongeza ya mamlaka yoyote yaliyokabidhiwa kwa Waziri na sheria nyengine yoyote inayohusiana na kufunga au kutumia taasisi za elimu au udhibiti wa masuala ya elimu katika dharura.[334]

**(i) Wajibu wa wazazi**

Wajibu wa mzazi ni kuhakikisha mtoto anapelekwa skuli mara baada ya kufikia umri wa kwenda skuli, na mtoto atasamehewa kuhudhuria skuli ikiwa skuli imefungwa kwa sababu yoyote; mwanafunzi amezuiwa kuhudhuria chini ya masharti ya Sheria au kanuni.[335]

---

[332] Ibid,Kifungu cha 35(1)
[333] Ibid,Kifungu cha 35(2)
[334] Ibid,Kifungu cha 35(3)
[335] Ibid,Kifungu cha 41(1)

Mwanafunzi hawezi kuhudhuria skuli kwa sababu ya ugonjwa hatari wa maambukizi, udhaifu, ugonjwa wa ghafla; ikiwa mwanafunzi huyo ana ulemavu wa kimwili au kiakili ambao, kwa maoni ya daktari, humfanya mwanafunzi ashindwe kufundishwa kwa njia za kawaida za kufundishia; mwanafunzi amepewa ruhusa na mwalimu mkuu ya kutokuwepo skuli kwa muda kwa sababu maalum; mwanafunzi anashiriki katika sherehe, shughuli zinazotambuliwa na madhehebu ya kidini; mwanafunzi amesimamishwa skuli; mwanafunzi anapokea elimu ya nyumbani au elimu maalum kwa mujibu wa Sheria hii.[336]

**(j) Masuala na taratibu za nidhamu**

Sheria katika sehemu ya tano imeweka utaratibu wa masuala ya nidhamu, kusimamishwa wanafunzi na kufukuzwa.[337]Mwalimu Mkuu au Mkuu wa taasisi anaweza, baada ya kushauriana na Bodi yake, kutunga sheria za kusimamia mavazi, na mwenendo wa nidhamu ya wanafunzi. Aidha, kanuni hizo lazima zisambazwe kwa wazazi wa wanafunzi; na zisianze kutumika hadi ziidhinishwe kwa maandishi na Afisa Mkuu wa Elimu.[338]

Kifungu kidogo cha 3, kinataka Sheria zinazoathiri wanafunzi lazima zitundikwe katika maeneo ya wazi ndani ya skuli au taasisi ya elimu na lazima ipitiwe upya na wanafunzi wa taasisi hiyo mwanzoni mwa kila mwaka wa skuli na zitumike kwa wanafunzi wote bila ubaguzi na lazima ziendane na Sheria hii na kanuni.

---

[336] Ibid,Kifungu cha 41
[337] Ibid,DIVISION 5 Discipline, Suspension and Expulsion of Students
[338] Ibid,Kifungu cha 51(1) na (2)

**(k) Kusimamishwa skuli kwa makosa makubwa**

Wanafunzi wanaweza kusimamishwa skuli kwa makosa makubwa na mwalimu mkuu kwa muda wa siku kumi za masomo kwa utovu wa nidhamu uliokithiri ambao unaweza kuwa hatari kwa wafanyakazi au wanafunzi wengine; ukiukaji wa kanuni yoyote ya skuli ambayo adhabu yake ni kusimamishwa; ukiukaji wa mara kwa mara wa kanuni za skuli; kukataa ovyo kwa mwanafunzi kukaguliwa, kuchunguzwa, kupewa chanjo au kutibiwa na daktari au muuguzi aliyesajiliwa anayefanya kazi kwa mujibu wa mpango wowote wa afya wa skuli; kuharibu mali yoyote ya skuli bila visingizio halali; au kumpiga mwalimu mkuu, mfanyakazi mwengine wa skuli; au mwanafunzi au mtu mwengine yeyote aliyepo kihalali skuli; kumiliki kitu chochote kilichotengenezwa au kubadilishwa kwa matumizi ya kusababisha jeraha; au kuwa na pombe au dawa za kulevya au vitu visivyo halali. Mwanafunzi ambaye amesimamishwa chini ya kifungu hiki atatangazwa.[339]

**(l) Uwasilishaji wa taarifa**

Sheria imeweka masharti ya uwasilishaji wa ripoti kwa Bodi baada ya kushauriana mwalimu mkuu, ndani ya mwezi mmoja baada ya mwisho wa mwaka wa masomo, itakayojumuisha mahudhurio ya wanafunzi,viwango vya ufaulu vya wanafunzi; matumizi ya mtaala, hali ya majengo ya skuli na matengenezo kwa ujumla, jambo lolote linaloathiri skuli na maendeleo yake; taarifa inayoelezea matumizi ya ruzuku yoyote iliyotolewa kwa skuli na Wizara au fedha zozote zilizopitishwa na Bunge, na makadirio yake ya mapato na matumizi ya skuli.[340]

---

[339] Ibid,Kifungu cha 55
[340] Ibid,Kifungu cha 65(1)

Taarifa ya Bodi ya Usimamizi ya kila skuli ya sekondari ya umma na kila skuli ya kibinafsi iliyosaidiwa lazima iwasilishwe mbele ya Bunge ndani ya miezi mitatu tangu kuanzishwa kwake kama iliyopokelewa na Waziri.[341]

**(m) Mahitaji ya kibali.**

Kwa mujibu wa Sheria hii. mtu yoyote hatoruhusiwa kuendesha skuli au taasisi ya elimu ya binafsi isipokuwa mtu huyo awe amesajiliwa na kupewa kibali cha ruhusa na waziri kwa ajili ya kuendesha skuli binafsi na atakae fanya hivyo atakuwa ametenda kosa na adhabu yake ni kulipa faini ya dola elfu moja (1000$) au kifungo cha miezi sita. Na ikiwa atakamatwa kwa mara ya pili atatozwa faini ya dola za Kimarekani mia mbili (200$) kwa kila siku kutoka siku ambayo amekamatwa kwa kosa la kwanza.[342]

### 5.4.6 Sheria ya Tanzania Nam. 25 ya mwaka 1978

Sheria hii imezingatia masuala mbalimbali ya elimu na ilianza kufanya kazi kupitia Gazeti Rasmi kwa kuzingati yafuatayo:

**(a) Jukumu la Waziri kukuza elimu ya kitaifa**

Sheria hii imempa Waziri wa Elimu mamlaka ya kukuza na kuendeleza elimu na maendeleo ya taasisi zilizojitolea kwa madhumuni hayo. Aidha, Waziri atasimamia udhibiti na mwelekeo wa sera ya kitaifa ya kutoa huduma mbalimbali za elimu.[343]

---

[341] Ibid,Kifungu cha 65(2)
[342] Ibid, kifungu cha 74(1 na 2)
[343] Kifungu cha 4(1), sheria ya Tanzania Nam. 25 ya mwaka 1978

Waziri anaweza kutafuta namna ya kuleta marekebisho katika maendeleo ya elimu kwa kuzingatia mipango iliyoandaliwa na wasimamizi wa skuli binafsi; kurekebisha na kuratibu mipango ya maendeleo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa; kuagiza au kupelekea kufanywa utafiti, au rejea kuhusiana na mambo mbalimbali ya kitaifa kwenye utoaji wa elimu.

### (b) Vyombo vilivyopo kisheria

Sheria hii imeleza utaratibu wa kuanzisha baraza la ushauri la elimu na Waziri wa Elimu anaweza kutoa amri ya kuanzisha kamati hizo za Baraza la ushauri.[344] Kazi za Baraza ni kumshauri Waziri kuhusu masuala ya utekelezaji wa sera ya taifa kuhusu elimu, uunganishaji wa vituo vya elimu nchini Tanzania, Kukuza elimu ya kitaifa na maendeleo ya skuli na jambo jengine lolote ambalo linaweza kutajwa na Wizara.

Vile vile, Sheria imeanzisha Ofisi ya Kamishna wa Elimu, na Kamishna atawajibika kwa usimamizi wa jumla na utawala wa skuli ambazo zipo chini ya usimamizi wa Serikali.[345]

Aidha**,** Sheria hii imeweka utaratibu wa kamati za elimu. Kila mamlaka ya elimu ya mitaa itaanzisha kamati ya elimu ambayo itashauri Mamlaka hiyo juu ya utendaji wake. Waziri kwa mamlaka aliyokuwa nayo anaweza kuanzisha kamati ndogo ndogo za elimu ili kusimamia shughuli za kukuza elimu.[346]

[344] Ibid,Kifungu cha 6
[345] Ibid,Kifungu cha 8
[346] Ibid,Kifungu cha 11

### (c) Mamlaka ya Serikali za Mitaa

Waziri amepewa mamlaka ya kuhamisha masuala ya Elimu kwenye Serikali za Mitaa baada ya kushauriana na Afisa Mfawidhi, na kutoa maelekezo yoyote ya mamlaka ya serikali za mitaa kuhusu utendaji na Mamlaka hiyo chini ya Sheria hii.[347] Pale ambapo Waziri anaona kwamba ni kwa maslahi ya umma, anaweza baada ya kushauriana na afisa anayefaa, kuhamisha kazi za mamlaka ya Elimu za serikali ya Mitaa kuhusiana na skuli yoyote ya mkoa.[348]

### (d) Kuanzishwa skuli

Sheria imeweka wazi kwamba hakuna skuli itakayoanzishwa bila idhini ya Kamishna wa Elimu.[349] Miongoni mwa masharti ya kuanzisha skuli ni pamoja na kupatikana kibali, na skuli ilenge kutoa mafunzo katika nyanja za kiufundi.[350] Waziri anaweza kuidhinisha au kukataa maombi yoyote, ikiwa skuli haina vigezo.[351]

Kamishna wa Elimu ametakiwa kutunza daftari la Usajili wa skuli za umma kwa kuzingatia Jina la shule; anuani yake, ikiwa ni pamoja na mkoa ambao skuli ipo, mtu au chombo cha watu kinachohusika na usimamizi wake na utawala; tarehe ya kuanzishwa kwake; na ngazi ya elimu.[352]

### (e) Uanzishwaji wa madarasa ya watu wazima

[347] Ibid,Kifungu cha 12
[348] Ibid,Kifungu cha 13
[349] Ibid,Kifungu cha 14
[350] Ibid,Kifungu cha 15
[351] Ibid,Kifungu cha 16
[352] Ibid,Kifungu cha 19 na 21

Sheria imempa mamlaka Waziri wa Elimu kuanzisha madarasa ya elimu ya watu wazima katika sehemu yoyote ambayo ataona inafaa kuwa sehemu ya skuli, na kwa kushirikiana na mamlaka ya elimu ya Serikali ya Mitaa, kufanya ukaguzi wa madarasa au madarasa ya baadhi ya skuli za umma ambayo yanaweza kutumika kama skuli.[353]

### (f) Usajili wa Skuli binafsi

Sheria inataka kila skuli binafsi iliyoanzishwa au inayokusudiwa kuanzishwa kusajiliwa chini ya Sheria kwa Kamishna wa elimu.[354] Maombi ya usajili wa skuli binafsi yatawasilishwa katika fomu maalum na yataambatanishwa na taarifa zinazohusiana na skuli inayotaka kufunguliwa na Waziri atatoa mapendekezo yake.[355]

Baada ya kupokea maombi, kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 27 na 28, Kamshina wa Elimu ataidhinisha jina la skuli na kama jina hatalikubali, basi Waziri anaweza kuidhinisha jina lolote lenye jina la Kiingereza au maneno ya Kiswahili, au neno lolote linalofanana.[356] Kamishna anaweza kufuta usajili wa skuli yoyote ya binafsi kwa misingi na taratibu ziliwekwa kisheria.[357]

Kwa mujibu wa kifungu cha 24 na 25, skuli binafsi zote zitasajiliwa na Kamishna, na iwapo skuli ya umma itatoa mafunzo ambayo hayamo katika mitaala iliyoainishwa, itatambulika kama skuli binafsi kwa ile sehemu ya

---

[353] Ibid,Kifungu cha 22
[354] Ibid, Kifungu cha 24
[355] Ibid,kifungu cha 25
[356] Ibid,Kifungu cha 26
[357] Ibid,Kifungu cha 29

ufundishaji wa mafunzo mengine. Kamishna anatakiwa kuweka orodha ya skuli binafsi na kuzitangaza katika Gazeti Rasmi la Serikali.[358]

Kamisha amepewa uwezo wa kukataa kusajili skuli binafsi ikiwa kutajitokeza sababu mbalimbali ikiwemo; ufundishaji wa skuli hauzingatii maslahi ya umma, skuli inatoa mafunzo ya ufundi tu, iwapo kuna hatari kwa watu kutumia majengo yanayopendekezwa kuwa skuli, au skuli haizingatii masharti na kanuni zilizotungwa chini ya sheria hii, au skuli hiyo ina uhusiano na taasisi ya kigeni.[359]Skuli inaweza kufutiwa usajili na Kamishna ikiwa imefanya makosa chini ya Sheria hii, skuli haipo au haifanyi kazi, au skuli imeshindwa kutoa elimu ya taifa  kama inavyotakiwa.[360]

### (g) Aina za skuli

Sheria katika kifungu cha 31 imetambua aina mbalimbali za skuli za taifa ikiwemo skuli za umma, vyuo vya maendeleo, vyuo vya elimu ya umma, na skuli za Mikoa zitajumuisha skuli za mikoa za msingi na elimu ya watu wazima na utaratibu wa usimamizi wa skuli zote umeachwa kwa Kamishna.[361]

Aidha, katika kuimarisha usimamizi huo, Kamati ya maendeleo ya Wilaya imepewa jukumu la usimamizi kwa skuli za Wilaya zilizo katika maeneo yao.[362]

### (h) Ukaguzi wa skuli

[358] Ibid,Kifungu cha 26(4)
[359] Ibid,Kifungu cha 28
[360] Ibid,Kifungu cha 29, Sheria ya Elimu ya Ghana Nam.778 ya Mwaka 2008
[361] Ibid, kifungu cha 33
[362] Ibid,kifungu cha 34

Ukaguzi wa skuli utafanywa na watendaji ambao watateuliwa na Waziri kama maafisa ukaguzi wa skuli,[363] na Kamishna ataweka utaratibu wa kuhakikisha skuli zinakaguliwa na ripoti inawasilishwa kwa Kamishna.[364]

### 5.4.7 Sheria ya Elimu ya Ghana Nam.778 ya Mwaka 2008

Nchi ya Ghana imetunga Sheria mahsusi ya Elimu ya mwaka 2008. Sheria hiyo imefafanua maeneo mbali mbali kuhusiana na usimamizi wa sekta hiyo ya elimu nchini humo. Maeneo hayo yanafafanuliwa hapa chini kama ifuatavyo:

### (a) Utangulizi (Preamble) kuakisi dhamira ya Sheria

Sheria ya Elimu ya Ghana imeanza kwa Utangulizi wa Sheria (Preamble) unaoelezea dhamira ya Sheria hiyo. Utangulizi huo umebainisha madhumuni ya Sheria hiyo ambayo ni kuweka mfumo wa sheria utakaowawezesha wananchi wa Ghana kuwa na uelewa, ujuzi, maadili, kukuza vipaji na kuwa na mwelekeo wa kuwa raia watakaosaidia uzalishaji kwa maendeleo ya nchi na ujenzi wa demokrasia.[365]

### (b) Elimu jumuishi

Sheria hii imetoa kipaumbele katika suala la kuwajumuisha watoto wenye ulemavu ili nao wapate haki ya kujifunza kama watoto wasio na ulemavu kwa kuweka masharti ya kisheria kwa madhumuni hayo.[366] Sheria hii imewataka wakuu wa taasisi za elimu kushirikiana na mabaraza ya wilaya kuhakikisha kuwa miundombinu ya skuli zinazoanzishwa inakuwa rafiki kwa watoto wenye

---

[363] Ibid,Kifungu cha 40
[364] Ibid,Kifungu cha 41
[365] Maelezo ya Utangulizi (Preamble) ya Sheria ya Elimu ya Ghana ya 2008, (Sheria Nam. 778) iliyopatikana kupitia mtandao wa Plain View Mode (lawsghana.com)
[366] Ibid,Kifungu cha 5

mahitaji maalum.[367] Kwa kutambua haja ya kuendeleza mazingira rafiki ya elimu kwa watoto wenye mahitaji maalum, Sheria imezitaka taasisi hizo kuimarisha miundombinu iliyopo na kuweka vifaa vyengine vitakavyowasaidia watoto hao wenye mahitaji maalum kadri itakavyohitajika.[368]

**(c) Uchunguzi wa kimatibabu wa watoto**

Sheria hii imeweka masharti ya kisheria kuitaka Sekta ya Elimu kwa kushirikiana na Sekta ya Afya na wizara yenye dhamana ya ustawi wa jamii kufanya uchunguzi wa kina wa afya za watoto kabla ya kujiunga, na uchunguzi wa mara kwa mara wa kitabibu kwa watoto waliopo skuli.[369] Bila ya shaka uchunguzi huu wa afya za wanafunzi katika skuli utasaidia katika ufikishaji wa elimu kwa wanafunzi kwa kutambua matatizo ya kiafya yanayowakabili wanafunzi kwa madhumuni ya kuyaondoa na kufanya lengo la utoaji wa taaluma lifikiwe.

**(d) Baraza la Taifa la Ufundishaji**

Sheria ya Elimu ya Ghana imeanzisha Baraza la Taifa la Ufundishaji[370] linaloundwa na wajumbe mbali mbali wakiwemo mwakilishi wa Waziri anayehusika na masuala ya elimu, Baraza la Taifa la Elimu ya Juu, Baraza la Elimu ya Amali, Bodi ya Taifa ya Ukaguzi wa Elimu na uwakilishi wa chuo cha elimu ya afya, uwakilishi wa vyuo vikuu vinavyotoa elimu ya ualimu na uwakilishi wa Chama cha Walimu, ambao wate wanateuliwa na Rais wa nchi hiyo.[371]

---

[367] Ibid,Kifungu cha 5(1)
[368] Ibid,Kifungu cha 5(2)
[369] Ibid,Kifungu cha 6
[370] Ibid,Kifungu cha 9
[371] Ibid,Kifungu cha 11

## SURA YA SITA

## 6.5 MATOKEO YA UTAFITI

### 6.6 Utangulizi

Sura hii inaelezea matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu baada ya kupitia fasihi, sheria za nchi, sera, uzoefu wa nchi mbali mbali na maoni ya wadau kuhusu sekta ya elimu. Aidha, Mipango ya nchi kama DIRA ya Maendeleo ya 2050 na ILANI ya CCM 2020-2025 pamoja na Mikataba ya Kimataifa yenye mnasaba na suala la elimu imezingatiwa.

### 6.7 Njia zilizotumika katika Utafiti

Njia zilizotumika kufanyia utafiti Sheria ya Elimu zimehusisha kwa asilimia kubwa utafiti wa ndani ambao umejumuisha sera, sheria mbalimbali, mikataba ya kimataifa, vitabu na maandiko yaliyozungumzia usimamizi wa sekta ya elimu.

Aidha njia nyengine ni kufanya mikutano na wadau wanaohusika katika usimamizi wa Elimu, wadau kutoka taasisi za Serikali na Zisizo za Serikali, wananchi, walimu na wanafunzi, wakaguzi wa elimu na wadau wengine katika sekta ya elimu.

### 6.8 Makundi ya Wadau (Sampuli ya utafiti) na Uchambuzi wa Takwimu

Kufikia malengo ya utafiti huu, makundi mbali mbali yalihusishwa. Makundi hayo yalijumuisha Taasisi mbalimbali za Serikali, Taasisi za binafsi

zinazohusiana na masuala ya Elimu, Wamiliki wa Skuli binafsi binafsi, Wadau kutoka taasisi za dini, Vyama vya wafanayakazi, Walimu Wakuu, wanasheria na wadau wengine wa elimu. Wadau hao ni kama wafuatao:

1. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali;
2. Idara ya Elimu Msingi na Maandalizi;
3. Idara ya Elimu ya Sekondari;
4. Kitengo cha TEHAMA Wizara ya Elimu;
5. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Wizara ya Elimu;
6. Taasisi ya Elimu Zanzibar;
7. Idara ya Mafunzo ya Ualimu;
8. Mrajis wa Elimu;
9. Kitengo cha Sheria, Wizara ya Elimu;
10. Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha;
11. Umoja wa Skuli Binafsi;
12. Wanafunzi wa Elimu ya Sekondari;
13. Wanafunzi wa Elimu ya Msimgi;
14. Watu Wenye Uzoefu katika Sekta ya Elimu;
15. Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA);
16. Ofisi ya Mufti wa Zanzibar;
17. Umoja wa Watu Wenye Ulemavu;
18. Chuo Kikuu cha Al-Sumait;
19. Chama cha Walimu Zanzibar;
20. Idara ya Ukaguzi wa Elimu;
21. Save the Children;
22. Kituo cha Kulelea Watoto Yatima;
23. Taasisi ya FAWE – Unguja;

24. Jumuiya ya ZAFAICO – Pemba;
25. Wizara ya Elimu Pemba;
26. ZATU –Pemba;
27. PACSO – Pemba;
28. AZASPO- Pemba;
29. PNYD - Kundi la Vijana – Pemba;
30. Wawakilishi wa vituo vya Yatima
31. Waandishi wa Habari;
32. Milele Zanzibar Foundation;
33. ZAFELA;
34. Kituo cha huduma za Sheria Zanzibar;
35. Kituo cha S.O.S.

Vikao vya wadau vilifanyika katika maeneo tofauti ya Zanzibar. Jumla ya wadau waliohudhuria katika vikao hivyo ni **457** sawa na **asilimia 88.9%** ya wadau walioalikwa. Katika idadi hii ya wadau makundi yaliyoshirikishwa kwa idadi kubwa ni pamoja na wanafunzi wa msingi na sekondari, walimu, wadau kutoka Wizara husika na watu wenye uzoefu mkubwa katika sekta ya elimu. Kwa uchambuzi wa kijinsia utafiti umeonesha jumla ya wanawake **125** walishiriki kutoa maoni yao na wanaume walikuwa **332.**

Wawakilishi kutoka makundi mbalimbali ya wadau ambao wameshiriki katika utafiti huu wametoa mapendekezo tofauti kuhusu Sheria ya Elimu na malengo yake. Hata hivyo, michango ya wadau walio wengi wametaka kufanyike mabadiliko makubwa katika sekta ya elimu na kubainisha kwamba changamoto zilizopo zifanyiwe kazi kisheria na kuwekewa utaratibu

madhubuti ili malengo ya kupata elimu bora yenye manufaa kwa wanafunzi na kumudu ushindani wa ajira uliopo nchini.

Aidha, wadau wamesisitiza kuimarishwa masuala ya kiutendaji ambayo yatakuwa chachu katika sekta ya elimu kwa kuzingatiwa maslahi tofauti ya watendaji na kuimarishwa usimamizi, ukaguzi, tathmini na ufuatiliaji wa maendeleo ya elimu katika muelekeo wa sekta ya elimu kwa maendeleo ya nchi kwa kipindi cha sasa na baadae.

Uchambuzi wa wadau walioshiriki katika utafiti huu kupitia vikao vya wadau ni kama unavyooneshwa katika Jadueli na Chati zifuatazo:


Jadueli Nam. 1 linaonesha Idadi ya washiriki wote na Taasisi walizotoka.

***Jadueli Nam. 1: Idadi ya washiriki wote katika vikao vya wadau.***

| Taasisi za Wadau Walioshiriki | Waliohudhuria | Walioalikwa | Asilimia |
|---|---|---|---|
| Wizara ya Elimu | 33 | 40 | 82.5 |
| Idara ya Elimu Msingi na Maandalizi | 9 | 10 | 90.0 |
| Idara ya Elimu ya Sekondari | 13 | 16 | 81.3 |
| Kitengo cha Tehama Wizara ya Elimu | 12 | 12 | 100.0 |
| Idara ya Mipango, Sera na Utafiti Wizara ya Elimu | 12 | 16 | 75.0 |
| Taasisi ya Elimu Zanzibar | 12 | 14 | 85.7 |
| Idara ya Mafunzo ya Ualimu | 16 | 20 | 80.0 |
| Mrajis katika Elimu | 8 | 8 | 100.0 |
| Kitengo cha Sheria Wizara ya Elimu | 14 | 18 | 77.8 |
| Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha | 24 | 27 | 88.9 |
| Umoja wa Skuli Binafsi | 15 | 20 | 75.0 |
| Wanafunzi wa Elimu ya Sekondari | 60 | 65 | 92.3 |
| Wanafunzi wa Elimu ya Msimgi | 57 | 65 | 87.7 |
| Watu Wenye Uzoefu katika Sekta ya Elimu | 36 | 40 | 90.0 |
| Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) | 4 | 6 | 66.7 |
| Ofisi ya Mufti wa Zanzibar | 6 | 6 | 100.0 |
| Umoja wa Watu Wenye Ulemavu | 16 | 19 | 84.2 |
| Chuo Kikuu Sumait University | 8 | 8 | 100.0 |
| Chama cha Walimu Zanzibar | 18 | 20 | 90.0 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Idara ya Ukaguzi wa Elimu | 11 | 16 | 68.8 |
| Save The Children | 4 | 4 | 100.0 |
| Kituo cha Kulelea Watoto Yatima | 8 | 8 | 100.0 |
| Taasisi ya (FAWE) – Unguja | 6 | 6 | 100.0 |
| Jumuiya ya (ZAFAICO) - Pemba | 8 | 8 | 100.0 |
| Wizara ya Elimu Pemba | 16 | 18 | 88.9 |
| ZATU –Pemba | 4 | 4 | 100.0 |
| PACSO – Pemba | 4 | 4 | 100.0 |
| AZASPO- Pemba | 4 | 4 | 100.0 |
| PNYD - Kundi la Vijana - Pemba | 4 | 4 | 100.0 |
| Kituo cha Watoto Yatima - Pemba | 4 | 4 | 100.0 |
| Waandishi wa Habari | 16 | 16 | 100.0 |
| Milele Zanzibar Foundation | 8 | 8 | 100.0 |
| ZAFELA | 8 | 8 | 100.0 |
| Kituo cha huduma za sheria | 4 | 4 | 100.0 |
| Kituo cha S.O.S | 8 | 8 | 100.0 |
| JUMLA | 457 | 514 | 88.9 |


***Chati Nam.1: Mchanganuo wa washiriki kwa Jinsia***




Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa, **asilimia (72.6%)** ya washiriki walikuwa wanaume na **asilimia (27.4%)** walikuwa wanawake. Washiriki wanawake walikuwa wachache kutokana na uteuzi wa maafisa katika baadhi ya taasisi.

Hata hivyo, mchango wao umekuwa muhimu katika maeneo ya ufuatiliaji, usimamizi, ukaguzi. Pamoja na kuimarishwa mfumo wa elimu. Matokeo hayo yanaonyesha kuwa utafiti huu umezingatia hoja ya ushiriki wa jinsia zote ili masuala ya jinsia katika sekta ya elimu yazingatiwe ipasavyo.


***Chati Nam. 2: Idadi na Asilimia ya Washiriki kwa Mujibu wa Kiwango cha Elimu***




Matokeo yanaonesha kuwa **asilimia (13.3%)** ya washiriki wana elimu ya Msingi, **asilimia (17.9%)** walikuwa na elimu ya sekondari, **asilimia (36.3%)** walikuwa na elimu baada ya Sekondari na **asilimia (32.4%)** walikuwa na elimu ya juu kuanzia shahada ya kwanza na kuendelea. Lengo kubwa la kufanya uchambuzi huu, ni kuonesha kwamba maoni katika utafiti huu yamezingatia wadau wenye elimu tofauti kwa lengo la kupata michango yao kutokana na sekta hii kuwa na changamoto katika kila eneo kuanzia ngazi za elimu ya chini hadi katika ngazi za juu.

Sehemu kubwa ya wenye elimu ya chini yaani asilimia 13.3 na 17.9 imeshirikisha wanafunzi wa msingi na Sekondari kwa lengo la kupata maoni kwa wahusika wa moja kwa moja wa ngazi hizo muhimu katika maendeleo na ukuaji wa elimu.

***Chati Nam.3: Idadi na Asilimia ya Washiriki kwa Mujibu wa Makundi ya Umri.***





Utafiti umezingatia kipengele muhimu katika uchambuzi cha eneo la umri wa wadau, ambapo kundi lenye umri kati ya **miaka 15 hadi 24** ambalo ni kundi la vijana limeshirikishwa kwa **asilimia (47.7%),** kundi la watu wenye umri kati ya **miaka 25 hadi 60** ambao ni tegemezi katika kukuza uchumi na maendeleo ya nchi limeshirikishwa kwa **asilimia (40.9%)** na kundi la mwisho ni kundi la wazee wenye umri kuanzia **miaka 60 na zaidi** ambao ni watu wenye uzoefu na wastaafu katika sekta ya elimu limeshirikishwa kwa **asilimia (11.4%)** katika utafiti huu.

Kigezo cha umri kimezingatiwa ili kuonesha uzoefu na mazingira kwa wadau wa umri tofauti na kuweza kutoa mapendekezo kwa kuzingatia wakati wa sasa na baadae.

Aidha, utafiti umebainisha na kuonesha makundi yalioshirikishwa kutoka katika taasisi mbali za Serikali na binafsi na taasisi nyengine katika masuala ya elimu pamoja wataalamu kutoka Wizara ya Elimu.

***Chati Nam.3: Asilimia kwa Mujibu wa Makundi ya Washiriki.***




Katika utafiti huu, wadau wenye utaalamu wa masuala ya elimu walishirikishwa kwa **asilimia (34.8%),** ikifuatiwa na wadau kutoka taasisi za Serikali **asilimia (28.3%)** na wadau wengi na wanafunzi walikuwa **asilimia (17.4%),** wadau kutoka taasisi za binafsi ni **asilimia (19.6%).**

## 6.9 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu umebainisha matokeo ya kisera, kisheria, kanuni na kiutendaji ambayo yatasaidia kuweka vizuri misingi ya elimu, usimamizi wa elimu,

usimamizi wa skuli, usimamizi wa walimu, wanafunzi na vyombo mbali mbali vinavyopaswa kusimamia sekta ya elimu.

### 6.5.1 Matokeo ya Kisera

#### (a) Mapitio ya Sera

Tume imebaini kwamba Sera iliyopo haikuzingatia baadhi ya mipango na malengo ya Serikali yaliyoelezwa katika DIRA 2050 na mipago ya nchi katika sekta mtambuka kama uchumi wa buluu, utalii n.k.

Miongoni mwa mambo ya msingi yaliyoelezwa ni kupitia upya mfumo wa elimu ili vijana waweze kujiajiri, mkakati wa usimamiaji wa makuzi na malezi ya watoto waliofikia umri wa kuanza skuli, ushirikishwaji wa wananchi katika maendeleo ya elimu, kuimarisha program za mafunzo ya amali zinazoendana na uwepo wa ajira, mageuzi katika mitaala ya elimu, kuinua kiwango cha ufundishaji, mikakati ya kusambaza vifaa vya kufundishia na kuimarisha matumizi ya Tehama.

Aidha, utafiti umebaini kwamba Sera ya elimu haijaelekeza vijana tokea hatua za awali kujielekeza katika sekta za maendeleo kama utalii, viwanda na uchumi wa buluu, au kujiajiri mwenyewe kwa kutumia fursa zilizopo.

#### (b) Mapitio ya mfumo wa elimu

Tume imebaini kwamba mfumo wa elimu uliopo hautoi maarifa ya kielimu kwa wanafunzi na stadi zinazowawezesha wanafunzi kufikiri zaidi na kuwa wabunifu ili kupambana na soko la ajira. Aidha, imebainika eneo la miundombinu ikiwemo maabara, maktaba na vifaa vya Tehama havijawekewa

mikakati maalumu ya kisera pamoja na ujumuishwaji na matumizi ya elimu ya dini katika kukuza sekta ya elimu nchni.

Vile vile, imebainika mfumo wa elimu haujaweka wazi upatikanaji wa walimu wenye utaalam, usimamizi wa walimu, tathmini ya walimu wanaofundisha katika skuli mbali mbali za Serikali na binafsi.

### 6.5.2 **Matokeo ya Kisheria**

#### (a) Mapitio ya Sheria ya Elimu

Utafiti huu umebaini kwamba, Sheria iliyopo haisaidi kubadilisha mfumo wa elimu uliopo na taratibu za usimamizi wa sekta nzima ya elimu. Aidha, kuna baadhi ya maeneo yaliyoelezwa katika sheria tayari yameshawekewa Sheria yake na hivyo hayawezi kufanyakazi kwa sasa. Maeneo yenyewe yanahusisha Sehemu ya sita, Sehemu ya Saba na baadhi ya vifungu viinavyozungumzia ukaguzi wa elimu, mafunzo ya amali, elimu ya juu ambapo usimamizi wake umeshawekewa utaratibu na sheria nyengine za Zanzibar na Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Utafiti umebaini kwamba, Muundo na baadhi ya Vyombo vilivyoanzishwa katika Sheria kama Bodi ya Elimu, Kamati za Wilaya na Mikoa haviendani na muundo wa Serikali uliopo na hivyo kupelekea mgongano wa kimajukumu. Aidha, baadhi ya vyombo vilivyoanzishwa vinahitaji kuundwa tena kwa kuwekewa misingi na kazi zake kama Kamati za Elimu, Bodi za skuli, usajili wa skuli n.k.

**(b) Kutokubainishwa kwa baadhi ya shughuli muhimu za Wizara katika Sheria**

Utafiti umebaini kwamba kuna shughuli muhimu zinazosimamiwa na Wizara kama masuala ya utafiti, usimamizi wa mitaala, usimamizi wa elimu ya Sekondari na Msingi, masuala ya ICT, tathmini na ufuatiliaji, elimu mjumuisho na usimamizi wa taasisi ya elimu ambayo majukumu yake hayakutambulishwa na kubainishwa kwa kina katika Sheria iliyopo na hivyo, kuhitajika utambuzi na usimamizi wa kisheria.

Muundo wa Ofisi ya Msajili wa Elimu haujaweka wazi masuala ya usimamizi, uwasilishaji wa taarifa mbali mbali zinazotoa picha ya hali halisi ilivyo katika sekta ya elimu Zanzibar, leseni na usajili wa walimu pamoja na taratibu na masharti yanayolingana.

**(c) Utaratibu wa kuripoti na kutoa taarifa**

Utafiti umebaini kuwa mfumo wa kisheria uliyopo sasa haujaweka mazingira ya kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa shughuli za elimu kupitia vyombo mbali mbali vilivyopewa kazi ya usimamizi katika ngazi zote. Aidha, imebainika ripoti za kusaidia udhibiti wa ubora wa elimu, mafanikio ya taasisi na skuli, ukaguzi na masuala ya mitihani hazijawekewa utaratibu maalum wa kuripotiwa na tathmini ya usimamizi wa maelekezo mbali mbali yanayotolewa katika kuimarisha sekta ya elimu.

**(d) Muundo wa Taasisi na mgawanyo wa majukumu**

Utafiti umebaini kuwa Sheria haijaweka mgawanyo ulio wazi baina ya majukumu ya Serikali, Waziri husika, Tawala za Mikoa, na Bodi ya ushauri.

Mgawanyo wa majukumu utaisaidia Serikali katika mipango ya maendeleo na wananchi watafahamu ngazi zilizopo Kitaifa na Kimikoa katika usimamizi wa mfumo wa elimu.
Aidha, Sheria iliyopo imebainisha majukumu ya Waziri ingawa kuna baadhi ya majukumu ni ya kiutendaji zaidi ambayo yanapaswa kuwa chini ya Wakurugenzi na Maafisa Elimu wa Wilaya na Mkoa.

Utafiti umebaini kuwa, mbali ya kuanzishwa kwa Kamati za Skuli chini ya kifungu cha 24 na 25 vya Sheria, muundo uliopo unahitajika kufanyiwa marekebisho ili kushirikisha zaidi Shehia, jamii na wazee wa wanafunzi, kuziweka vizuri zaidi kazi za Kamati za skuli ili zilenge kuendeleza skuli na kukuza taaluma. Aidha, Sheria haijatambua muundo unaotambulika wa skuli binafsi, na majukumu yao katika Skuli za Serikali na Binafsi.

**(e) Muundo wa Bodi ya Elimu**

Utafiti umebaini kuwa Sheria imeanzisha Bodi ya Ushauri ingawa baadhi ya majukumu iliyopewa Bodi hii ni ya kiusimamizi zaidi kuliko ya kiushauri. Aidha, imebainika kwamba kuna baadhi ya majukumu ambayo yanatakiwa kusimamiwa na Bodi hayakuainishwa katika Sheria hii.
Utafiti pia umebaini kwamba Muundo wa Bodi, uanzishwaji wake, wajumbe wa Bodi na sifa zake, kazi na majukumu ya Bodi na muda wa kutumikia Bodi na maeneo mengine yanahaja ya kuwekewa msingi kisheria ili kuimarisha usimamizi katika sekta ya elimu nchini.

**(f) Majukumu ya wadau wengine katika usimamizi wa sekta ya elimu**

Utafiti umebaini kwamba Sheria haijabainisha majukumu ya wazi kwa wadau muhimu kama Asasi zinazosimamia masuala ya elimu au zilizoundwa kwa madhumuni hayo, na wazee ambapo majukumu yao hayakuelezwa kwa kina katika kifungu cha 20 na 22 cha Sheria iliyopo sheria haijaweka sifa, uzoefu na majukumu ya walimu wakuu, majukumu ya jamii, Kamati za skuli, taasisi na wadau wengine wa elimu ambao ushiriki wao ni muhimu katika kusaidia mipango ya maendeleo ya elimu.

**(g) Usimamizi na udhibiti wa Skuli**

Utafiti umebaini kuwa muundo wa usimamizi wa skuli haujabainishwa wazi katika Sheria kwa skuli za Serikali na skuli binafsi. Usimamizi unahitaji kuonesha ufuatiliaji wa ufundishaji, nidhamu na mwenendo wa skuli mbali mbali, udhibiti wa kuhakikisha skuli zinafundisha kwa mujibu wa mitaala iliyopo na adhabu kwa vitendo vyovyote kwa upande wa walimu na wanafunzi vinavyokiuka Sheria ya Elimu au Sheria nyengine ya nchi.

**(h) Usajili wa Skuli za Serikali na Skuli binafsi**

Utafiti umebaini kuwa Sheria iliyopo imetaja usajili wa skuli katika vifungu vya 10, 11,13,14 na 15. Hata hivyo taratibu zilizopo katika Sheria hazikuweka kwa uwazi masuala ya usajili kwa skuli za Serikali na binafsi, masharti na vigezo vya usajili, kutokuzingatiwa misingi ya kutokuwa na ubaguzi wakati wa kuanzishwa kwa skuli, masharti ya uwepo wa walimu wenye sifa, uwezo wa kifedha wa kusimamia na kuiendeleza skuli na vigezo vya miundombinu ikiwemo majengo,na vifaa vya kufundishia n.k.

Aidha, imebainika kuwa ipo haja ya kuwepo kwa Daftari la Usajili la skuli zote za Serikali na binafsi ili kuzitambua skuli zilizopo, hadhi zake, maeneo zilipo, vifaa vilivyopo, eneo la ardhi, idadi ya walimu na idadi ya wanafunzi.

**(i) Usajili na leseni za walimu**

Utafiti umebaini kuwa mbali ya kuwekwa mazingira ya kukataa kumsajili mwalimu na kufuta usajili wa mwalimu chini ya vifungu vya 40 na 41 vya Sheria ya Elimu, Sheria hiyo haijaweka wazi masharti ya usajili kwa baadhi ya maeneo. Miongoni mwa maeneo ambayo hayajawekwa wazi ni taratibu za usajili wa walimu, utaratibu wa maombi kwa walimu, utaratibu wa kufuta usajili wa walimu na utaratibu wa kufuta walimu ambao hawana sifa.

Aidha, Sheria haijabainisha majukumu ya Msajili wa Elimu pamoja na kutokuwepo kwa masharti ya kuanzishwa kwa daftari la usajili na muundo wake. Vile vile, kifungu kinachozungumzia leseni ya walimu kinapaswa kibadilishwe ili masharti yake yasikwaze ufundishaji na ukuzaji wa sekta ya elimu.

**(j) Utaratibu wa malalamiko**

Utafiti umebaini kuwa Sheria haikubainisha utaratibu wa kuwasilisha na kuyashughulikia malalamiko ya walimu kuhusiana na haki na fursa za walimu na vyombo vya kushughulikia malalamiko hayo na hatua zinazoweza kuchukuliwa.

Aidha, imebainika kuwa utaratibu wa wanafunzi, wazee na jamii kulalamikia walimu katika masuala mbali mbali kama vile ufundishaji, tabia au maadili ya

mwalimu haujawekwa kisheria. Hivyo, kukosekana kwa taratibu hizi kunanyima haki, fursa na kukwaza maendeleo ya elimu, Zanzibar.

**(k) Maadili ya walimu**

Utafiti umebaini kwamba Sheria haijaanzisha kanuni za maadili ya walimu ambazo zitakuza nidhamu za walimu na kulinda maslahi ya wanafunnzi katika skuli mbali mbali. Kada ya walimu ni muhimu katika jamii na matendo ya walimu yanaathari kubwa kwa maendeleo ya wanafunzi na jamii kwa ujumla. Mbali ya kuwepo kwa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 2 ya 2011, kuna haja ya kuweka makossa, maalum na mazingira kwa walimu wanaokiuka maadili.

**(l) Makosa na adhabu**

Utafiti umebaini kwamba Sheria iliyopo imeacha baadhi ya makosa katika maeneo ya usajili na udhibiti wa walimu, ufundishaji, maadili pamoja na kuweka adhabu ndogo za kiwango cha TZS. 5,000 mpaka TZS 15,000 ambazo ni za chini sana ikilinganishwa na ukubwa wa makosa yanayofanywa.

Aidha, utafiti huu umebaini kutokuwepo kwa utaratibu wa kumaliza baadhi ya makosa madogo madogo ambao utaruhusu kulipwa faini kwa makosa hayo na kupunguza utitiri wa kupeleka mashauri mengi ya kiutawala katika vyombo vya kisheria. Imebainika kuwa Sheria haikuweka utaratibu wa kumaliza makosa madogo kwa muda mfupi ili kutokuathiri shughuli na maendeleo ya wanafunzi.

**(m) Mafunzo kwa walimu**

Utafiti umebaini kwamba Sheria haijaweka masharti ya kuwaendeleza walimu katika mafunzo ya muda mfupi kwa kuzingatia, mabadiliko ya sayansi na teknolojia, mabadiliko ya mitaala na mafunzo mengine ya kuwajengea uwezo walimu na kuwafanya wawasaidie wanafunzi kulingana na mazingira. Aidha, imebainika baadhi ya walimu hushiriki katika mafunzo ambayo hawajaanza nayo awali katika kufundisha na wengine kubadilisha masomo wanayofundisha na wengine hujiendeleza katika maeneo waliyobobea katika ufundishaji wanapofikia katika elimu ya juu.
Utafiti umebaini kwamba kuna walimu ambao hawana stadi za kufundisha lakini wanafundisha katika skuli mbalimbali.

**(n) Mfuko wa Maendeleo ya Elimu**

Utafiti umebaini kwamba Mfuko wa Maendeleo ya Elimu ulioanzishwa chini ya kifungu cha 56 cha Sheria unahitaji kuwekewa misingi zaidi kiutendaji pamoja na kubainisha kwa uwazi vyanzo na upatikanaji wa fedha za mfuko wa elimu na matumizi yake ili uweze kuinua sekta ya elimu na kusaidia kutatua changamoto zinazoikumba sekta ya elimu.

Aidha, Sheria imetaka kutungwa kanuni zitakazofafanua taratibu za muundo, kazi na udhibiti kwa mfuko lakini utafiti ubaini kuwa kanuni hizo hazijatungwa na hivyo kufanya utaratibu wa uanzishwaji na uendeshaji wa mfuko huo kutokufikia malengo kama ilivyokusudiwa.

**(o) Kamati za Wilaya na Mikoa**

Utafiti huu umebaini kuwa, kifungu cha 26 na 28 vya Sheria ya Elimu vimeanzisha Kamati za Wilaya na Mikoa ambazo muundo wake unapelekea

muingiliano wa majukumu ngazi ya Wilaya na Mkoa na unanyima fursa kwa Mikoa kuwa na jukumu la juu la usimamizi.

Aidha, majukumu yaliyoainishwa katika kifungu cha 27 na 29 hayalengi kuinua na kukuza elimu katika Wilaya na Mikoa na kufikia katika malengo ya DIRA ya 2050 na ILANI ya CCM 2020.

**(p) Ukaguzi wa masuala ya kiafya kwa wanafunzi**

Utafiti umebaini kuwa kifungu cha 57 cha Sheria ya Elimu kimetaja suala la ukaguzi wa kiafya lakini hakikiweka muda maalumu wa kufanyika uchunguzi huo. Aidha imebainika kwamba ipo haja ya kuwekewa utaratibu kisheria masuala ya uchunguzi wa kiafya kwa mazingira ya skuli pamoja uchunguzi wa wanafunzi kwa maradhi/ viungo vitakavyoainishwa na suala hilo kuwa ni la lazima kwa wakati utakaowekwa.

**(q) Kufanya tathmini kila baada ya muda**

Utafiti umebaini kuwa ipo haja ya kuwekwa utaratibu wa kisheria wa kufanyika kwa tathmini kila baada ya muda na kutolewa ripoti itakayoainisha mafanikio na changamoto zitakazojitokeza katika uendeshaji na utekelezaji wa shughuli za kielimu hapa nchini. Aidha, kuwepo kwa hatua hiyo kutapelekea ripoti hiyo ya tathmini kupima mwenendo wa elimu ikilinganishwa na viashiria vilivyowekwa kufikiwa, kuangalia elimu inayotolewa kama inakidhi haja ya mtazamo wan chi katika kupata elimu bora itakayowawezesha vijana wanaomaliza kujitegemea na kuwa na utaalamu wa ushindani katika soko la ajira.

### (r) Watu wenye ulemavu na maendeleo ya sayansi na teknolojia

Utafiti huu umebaini kwamba uhitaji wa elimu kwa watu wenye ulemavu unakumbana na changamoto nyingi zinazosababishwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia ambayo kila baada ya muda kuna mabadiliko katika maeneo hayo ya utandawazi. Kwa mustakbal huo utafiti umeona ipo haja ya kuwa na utaratibu maalum wa kisheria kwa watu wa aina hii katika upatikanaji wa elimu juu yao. Utaratibu utakaotayarishwa uwe na vipengele vitakavyowasaidia kupata haki ya elimu kwa aina ya kiupendeleo na isiwe sawa na watu wengine ambao hawana ulemavu.

## 6.6 Matokeo ya Kiutendaji

### (a) Matumizi ya sayansi na teknolojia

Utafiti umebaini kwamba Wizara ya Elimu inayo Idara maalumu ya TEHAMA inayosimamia masuala ya teknolojia kwa ajili ya kuimarisha huduma za elimu zitumie mifumo mbali mbali. Mbali ya kuwepo kwa Idara hii bado matumizi ya teknonolojia kwa skuli za msingi na Sekondari hayajawa ya kuridhisha na baadhi ya skuli hazina vifaa vya kutosha vya kuwezesha kusoma kupitia mifumo ya sayansi na teknolojia. Matumizi haya hayajaimarishwa pia katika skuli binafsi ambazo zinatoza ada kwa lengo la kutoa huduma nzuri kwa wanafunzi wanaowafundisha.

### (b) Mazingira jumuishi

Utafiti umebaini kwamba Sera ya Elimu na Sera ya Watu wenye Ulemavu hazijafanyiwa kazi vya kutosha katika kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Aidha, imebainika kuwa skuli nyingi hazina mazingira ya kujumuisha watoto wenye ulemavu kama walemavu wa viungo na baadhi hawana vifaa maalum vya kuwasaidia wanafunzi wenye ulemavu wa kusikia, kuona na kuzungumza.

**(c) Udhibiti mdogo wa vituo vya elimu ya ziada (Tuition centre)**

Utafiti umebaini kwamba kuna vituo vingi vya elimu ya ziada (tuition) ambavyo vimekosa usimamizi na udhibiti wa moja kwa moja kutoka wizara ya elimu. Aidha, utafiti umebaini kwamba kuna baadhi ya Skuli zinawataka watoto kutumia muda wa ziada kuhudhuria masomo mbali mbali bila ya kuzingatia muda halisi wa masomo.

Kutokudhibitiwa kwa masomo ya ziada kunawafanya watoto wakose muda wa kupumzika, wakutane na mazingira hatarishi wakati wanapokwenda na kurudi kwenye masomo ya ziada, kutokupata muda wa kuhudhuria masomo ya dini na kwa upande wa walimu kushindwa kutumia muda mzuri wakiwa kazini katika kufundisha na kuwasaidia wanafunzi hao.

**(d) Utungwaji wa kanuni**

Utafiti umebaini kwamba Sheria iliopo imetaja kuanzishwa kwa kanuni mbali mbali zitakazosaidia kuimarisha sekta ya elimu lakini kanuni hizo bado hazijatungwa hadi sasa. Hatua hii inakwamisha utekelezaji wa baadhi ya vifungu vya Sheria.

## SURA YA SABA

## 7.0 MAPENDEKEZO YA TUME NA HITIMISHO

### 7.1 Utangulizi

Sura hii inatoa mapendekezo ya utafiti wa mapitio ya Sheria ya Elimu Nam. 6 ya mwaka 1982. Baada ya kuzingatia Sera, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020-2025, maoni ya wadau wa sekta ya elimu pamoja na uzoefu wa nchi mbalimbali, Tume inatoa mapendekezo katika maeneo ya Sera, Sheria na utendaji.

### 7.2 Mapendekezo ya Sera

Tume inapendekeza Sera iliyopo ifanyiwe mapitio kwa kujumuisha mikakati na matarajio yaliyowekwa katika DIRA ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050 na mwelekeo wa elimu. Aidha, kutokana na mabadiliko mbali mbali ya sayansi na teknolojia, pamoja na uzoefu wa nchi mbali mbali na mazingatio ya Mikataba ya Kimataifa. Inapendekezwa Sera ijumuishe maeneo yafuatayo:

(a) Msingi wa elimu kwa watoto wadogo wanaofikia umri wa kuanza Skuli katika ngazi ya maandalizi na msingi;

(b) Mitaala ya elimu na utaratibu wa kufanyiwa mapitio mitaala hiyo;

(c) Miongozo kuhusiana na Lugha ya kufundishia;

(d) Mazingatio ya Elimu mjumuisho;

(e) Viwango vya ufaulu wa mitihani;

(f) Usajili wa walimu na mafunzo ya walimu;

(g) Matumizi ya teknolojia katika ufundishaji;

(h) Usimamizi wa sekta ya elimu;

(i) Mfuko wa Elimu na utaratibu wake;

(j) Mfumo wa tathmini ya elimu na walimu ili kuwa na kiwango bora cha ufundishaji;

(k) Maendeleo ya elimu kwa ujumla;

(l) Suala la utafiti wa elimu;

(m) Msingi na Usimamizi vyuo vya amali na vyuo vyengine vya kukuza elimu;

(n) Mwelekeo wa Dira ya elimu ya Zanzibar.

## 7.3 Mapendekezo ya Kisheria

### 1. Kufutwa Sheria iliyopo

Mbali ya mapendekzo ya kisera yaliyobainishwa hapo juu, Tume inatoa mapendekezo mbali mbali ya kisheria yatakayosaidia kuimarisha sekta ya elimu nchini. Miongoni mwa mapendekezo hayo, Tume inapendekeza kufutwa Sheria ya Elimu Nam. 6 ya Mwaka 1982 na kutungwa sheria mpya kutokana na sababu zifuatazo:

(a) Kutokuzingatiwa kwa mikakati na matarajio ya DIRA ya Maendeleo ya 2050, Mipango ya mwelekeo wa Elimu Afrika na Afrika Mashariki pamoja na mipango iliyoelezwa katika ILANI ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020.

(b) Kuwepo kwa maeneo na vifungu ndani ya Sheria ya Elimu ambavyo vimeshatungiwa Sheria zake kama vile eneo la ukaguzi na masuala ya elimu ya amali.

(c) Uwepo wa maeneo ambayo kwa sasa yanasimamiwa na Sheria za Muungano kama eneo la Elimu ya Juu.

(d) Kutokuwepo kwa mgawanyo ulio wazi wa vyombo vya usimamizi wa elimu, muundo na majukumu yake.

(e) Kutokuwepo kwa uendelevu wa usimamiaji wa shughuli za elimu katika Sheria pamoja na kutokuwekwa wazi misingi ya Mfuko wa Elimu.

(f) Kutokuzingatiwa kwa misingi ya utawala bora kwa kuacha eneo la uwajibikaji na uwazi katika usimamizi wa mfumo mzima wa elimu.

(g) Kutokuainishwa nafasi ya Wizara katika usimamizi wa vyuo mbali mbali na miongozo yake.

(h) Kutokubainishwa utaratibu wa nidhamu za wanafunzi, mahusiano ya walimu na wazee, pamoja na uwasilishaji wa malalamiko.

2. **Maeneo ya kuzingatiwa:**

Tume inapendekeza Sheria mpya inayopendekezwa kutungwa izingatie yafuatayo:

**a) Kuweka wazi malengo ya kuwepo kwa Sheria ya Elimu**

Inapendekezwa Sheria iweke wazi malengo ya kuwepo kwa Sheria ya Elimu ambayo yatajumuisha uwekaji wa mfumo wa sheria utakaowezesha wananchi kuwa na uelewa, ujuzi, maadili, malengo ya ukuzaji vipaji, ubunifu na mwelekeo wa kusaidia uzalishaji kwa maendeleo ya nchi. Mapendekezo haya yanatokana na udhaifu wa mfumo wa elimu uliopo sasa kama ilivyobainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Zanzibar. Hivyo inapendekezwa kuwa na Vifungu mahsusi katika Sheria hiyo mpya ya Elimu viwekwe kujumuisha malengo ya Sheria ya Elimu kama yalivyoelezwa hapo juu.

**b) Kuimarisha misingi katika masuala ya elimu**

Inapendekezwa kuwa Sheria mpya inayopendekezwa kutungwa ikiimarishe kifungu cha 53 kinachozungumzia misingi ya elimu kwa kuongeza misingi muhimu ambayo haukujuilishwa katika Sheria Nam. 6 ya 1982 ikiwemo:

(i) Uzingatiaji wa ubora wa viwango vya elimu kuanzia ngazi ya elimu ya maandalizi, msingi, sekondari hadi chuo kikuu kwa kuwa na mafunzo ya kina ya walimu na miundombinu bora zaidi ya elimu;

(ii) Ushirikishwaji mkubwa zaidi wa wananchi katika masuala ya elimu kupitia kamati za skuli na jumuiya mbali mbali za kiraia, sekta binafsi na washirika wa maendeleo;

(iii) Uwajibikaji wa wazi wa walimu, walimu wakuu na viongozi wengine wa sekta ya elimu kupitia upimaji na tathmini ya utendaji pamoja na uwasilishaji wa ripoti za utendaji;

(iv) Maadili kwa wanafunzi, walimu na wasimamizi wote wa sekta ya elimu nchini.

**c) Kutambua vyombo vya usimamizi wa masuala ya elimu na kazi zake.**

Tume inapendekeza Sheria mpya ya Elimu itakayotungwa izingatie vyombo vya usimamizi wa sekta ya elimu na mgawanyo wa majukumu yake na masharti yanayohusu vyombo hivi vya usimamizi wa elimu. Miongoni mwa kasoro ziliopo katika Sheria ya Elimu ya mwaka 1982 ni pamoja na kutobainishwa kwa kina, kazi za vyombo hivyo vya usimamizi wa elimu zikiwemo kamati za skuli, mamlaka yake, muda wa wajumbe kudumu katika nafasi zao na maeneo mengine, pamoja na kuwepo kwa uwezekano wa kuingiliana kwa majukumu baina ya vyombo hivyo hasa Bodi na Kamati za Skuli, Bodi za Wilaya na Mikoa katika vifungu vya 27-31. Aidha, majukumu ya

Bodi katika vifungu vya 5-9 vya Sheria iliyopo, kifungu cha 24 cha Kamati za Skuli na uanzishwaji wake n.k.

Hivyo, Tume inapendekeza Sheria mpya inayopendekezwa iwe na vifungu vitakavyoweka maelezo ya kina ya uanzishwaji wa vyombo hivyo vya usimamizi wa elimu, kazi zake za msingi, mamlaka yake, sifa za wajumbe kwenye vyombo hivyo kwa kuzingatia utaalamu na uzoefu katika sekta ya elimu, kusita kwa wajumbe wa vyombo hivyo na kadhalika.

**d) Utaratibu wa udhibiti wa Skuli za Serikali**

Sheria ya Elimu imeweka utaratibu wa usimamizi wa Skuli za Serikali katika vifungu vya 17-21 ingawa haijaanisha yafuatayo:

(i) Sifa za skuli za Serikali na uanzishwaji wake;
(ii) Uhusiano wa skuli na Wizara na Idara zake;
(iii) Uwajibikaji wa walimu wakuu na Kamati za Skuli;
(iv) Uandikishwaji wa wanafunzi;
(v) Matumizi ya skuli za Serikali na rasilimali za skuli;
(vi) Uhifadhi wa maeneo ya skuli na utaratibu wake;
(vii) Uwajibikaji katika ukusanyaji wa ada mbali mbali n.k.

**e) Jukumu la Mamlaka za Serikali za Mitaa.**

Sheria ya Elimu imetambua mamlaka za Serikali za mitaa na Kamati za Wilaya na Mikoa. Inapendekezwa kuwa Sheria inayopendekezwa kutungwa iweke muundo mzuri kwa Mikoa na Wilaya kushiriki katika maendeleo ya elimu kwa kubainisha majukumu ya msingi ya Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya kwa

skuli zilizo katika maeneo yao. Majukumu hayo inapendekezwa yajumuishe maeneo yafuatayo:

i. Kutathmini maendeleo ya skuli zilizo katika mikoa yao,
ii. Kusaidia shughuli za ulinzi wa skuli na utunzaji wa mazingira,
iii. Kuratibu upatikanaji wa vifaa vya misaada kutoka kwa wadau mbalimbali vinavyoingizwa katika skuli zilizo katika mikoa kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu,
iv. Kutathmini matumizi ya maeneo ya skuli kwa shughuli mbalimbali na kuelekeza njia bora ya matumizi ya maeneo hayo, kusaidia upatikanaji wa huduma kama maji na umeme kutoka mamlaka zinazohusika na kusaidia shughuli za skuli, kusaidia uratibu wa mitihani ya taifa kwa kuhakikisha ulinzi na taratibu za Serikali zimefuatwa na skuli, kuhakikisha wazazi walio katika Mikoa au Wilaya zao wanapeleka watoto skuli kuhakikisha malengo ya sheria yanafikiwa, kuhakikisha uanzishwaji wa maeneo maalum ya kujisomea kama maktaba za Wilaya na Mikoa.
v. Kusaidia kupatikana kwa hati miliki za maeneo ya Skuli ziliopo katika maeneo yao.
vi. Kuhamasisha uchangiaji wa sekta ya elimu katika maeneo yao kupitia kwa wawekezaji waliopo katika maeneo yao na wanachi wa maeneo hayo kwa ujumla. Uchangiaji huo unaweza kujikita katika upatikanaji wa vifaa vya maabara, na maktaba, matengenezo ya majengo ya skuli, upatikanaji wa viti na meza na maeneo mengine.

Aidha inapendekezwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zisaidie katika uanzishwaji wa Mipango ya maendeleo ya skuli na kuibua vipaji vya wanafunzi walio katika Mikoa na Wilaya zao.

**f) Masuala ya nidhamu na adhabu kwa wanafunzi**

Sheria ya Elimu, imeweka mamlaka ya Nidhamu kwa vyombo mbali mbali ikiwemo Kamati za Skuli zilizoanzishwa chini ya kifungu cha 24. Utaratibu huo haujatoa Mamlaka na kueleza upeo wa makossa ya kufikishwa katika Kamati, nay ale ya Kusimamiwa na Wlimu na Walimu Wakuu.

Tume inapendekeza Sheria ibainishe wazi usimamizi wa masuala ya kinidhamu kwa wanafunzi, pamoja na kupendekeza hatua za kuchukuliwa kwa makosa mbalimbali yanayofanywa na wanafunzi kama itakavyowekwa katika Kanuni.

Aidha, inapendekezwa Sheria ieleze uwezo na makosa yanayopelekea kusimamishwa kwa muda wanafunzi na taratibu zake, kufukuzwa au kupewa adhabu kubwa kulingana na makosa yanayofanyika skuli.

Inapendekezwa Sheria itoe mamlaka kwa Mwalimu Mkuu na Kamati za skuli kushauriana kuhusu nidhamu ya wanafunzi na pale itakapokuwa kosa ni kubwa zaidi, Wizara ishirikishwe katika maamuzi hayo.

**g) Suala la mitaala**

Tume inapendekeza kuwekwa vifungu maalum vitakavyozungumzia mitaala ya wanafunzi na jinsi ya kubadilishwa mitaala hiyo. Sheria iainishe sera ya kutumika katika mitaala, tathmini ya mitaala kila baada ya muda, misingi ya

kufundishwa, taratibu za masomo ya dini, kushauri vifaa vya kutumika katika maskuli ili kuendana na mitaala hiyo, utayarishwaji wa mitihani kwa kuzingatia mitaala iliyopo, na kuhakikisha mitaala inazingatia maadili, inaimarisha stadi za ubunifu na inaimarisha maendeleo ya wanafunzi kielimu.

**h) Kutambua Idara na taasisi za usimamizi wa elimu ndani ya Wizara**

Kutokana na kuwepo kwa Idara nyingi zilizoundwa kiutawala kusaidia majukumu ya Wizara ya Elimu, Zanzibar, Tume inapendekeza Sheria inayopendekezwa kutungwa itambue Idara au majukumu yanayofanywa na Idara hizo na mchango wa Idara husika katika kusimamia elimu ili kuwa na mwendelezo mzuri na usimamizi wa majukumu yanayofanywa na Wizara. Inapendekezwa Idara za usimamizi ikiwemo Idara za usimamizi wa Skuli za msingi na Sekondari, Idara zinazosimamia Maendeleo ya Skuli na Walimu na idara ya TEHAMA zitambuliwe kisheria na zisaidie kuunda mfumo sahihi wa usimamizi wa sekta ya elimu Zanzibar.

**i) Kupima viwango vya ubora wa elimu**

Tume inapendekeza sheria iweke jukumu kwa Wizara kuweka utaratibu wa kupima viwango vya elimu vya wanafunzi na viwango kwa walimu wanaofundisha. Mbali ya majukumu ya mwalimu mkuu, Sheria itambue chombo cha kusimamia tathmini za wanafunzi na kuchunguza ufaulu wa wanafunzi na mambo yanayopelekea wanafunzi kutokufanya vizuri katika baadhi ya masomo.

Inapendekezwa chombo hicho kitathmini:

i. Ufahamu wa wanafunzi katika masomo yao;
ii. Hali ya ufaulu wa wanafunzi;

iii. Njia zinazotumika kuwapima wanafunzi;
iv. Masomo wanayofeli wanafunzi na sababu zake;
v. Sababu zinazofanya wanafunzi kufeli mitihani;
vi. Skuli ambazo viwango vyake vitakuwa chini ya ufaulu kwa miaka mingi;
vii. Kupendekeza hatua za kuchukuliwa na Wizara na Serikali katika kuhakikisha kunakuwa na ufaulu mkubwa wa wanafunzi;
viii. Uwezo wa wahitimu na namna wanavyoweza kuingia katika soko la ajira na kumudu ushindani uliopo.

**j) Uanzishwaji wa Jukwaa la Elimu**

Tume inapendekeza kuanzishwa kwa jukwaa la elimu litakalotoa fursa kwa wadau kutoa maoni yao chini ya miongozo ya Wizara na Bodi ya Elimu itakayoundwa chini ya Sheria. Hatua hii itasaidia kukutanisha wataalamu na wazoefu wa sekta ya elimu, viongozi wa dini, wazee na taasisi binafsi, na washirika wa maendeleo wenye nia na malengo ya kuendeleza sekta ya elimu Zanzibar.

**k) Suala la uzingatiaji wa teknolojia katika elimu**

Kutokana na mabadliko yaliyopo na misingi ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050, Tume inapendekeza sheria iweke vifungu vitakavyolazimisha skuli kuendeleza masomo na matumizi ya vifaa vya sayansi na teknolojia, na kuweka wajibu kwa Wizara na Bodi ya Elimu kusimamia maendeleo ya teknolojia ili kuwawezesha wanafunzi kujifunza vizuri zaidi.

**l) Uchunguzi wa afya za wanafunzi na mazingira**

Sheria ya elimu katika kifungu cha 57, imeweka utatatibu wa uchunguzi wa afya za wanafunzi, pamoja kuwekwa taarifa za maendeleo ya afya na maendeleo ya

mwanafunzi. Hata hivyo, kifungu hakijabainisha nani mwenye jukumu la kuweka taarifa na utaratibu huo.

Tume inapendekeza kuwekwa kifungu kinachohamasisha kufanywa uchunguzi wa kiafya kwa wanafunzi kila baada ya muda ili wanafunzi wenye maradhi ya mbalimbali waweze kufahamika na kuwekewa utaratibu kwa kushauriana na mamlaka husika. Aidha, hatua hii itahakikisha maendeleo ya wanafunzi, kushauri hatua za kuchukuliwa na wazazi na vyombo husika kama Wizara ya Afya na taasisi za mazingira ili kudumisha afya, usafi na kuweka mazingira bora ya skuli.

**m) Mfuko wa elimu**

Inapendekezwa kuimarishwa kwa Mfuko wa Elimu kwa kuwekewa vyanzo na upatikanaji wa fedha za Mfuko pamoja na kuwekwa kwa taratibu maalum katika Kanuni, ambazo zitasimamia Mfuko huo ili uweze kusaidia kuinua sekta ya elimu nchini.

**n) Haki na Majukumu ya wazazi na wanafunzi, Walimu Wakuu, Kamati za Skuli na Jamii kwa ujumla.**

Kifungu cha 22 cha Sheria, kimeainisha majukumu ya wazazi na walezi ambayo yamejielekeza katika uandikishaji zaidi. Inapendekezwa Sheria iainishe haki na majukumu ya wadau muhimu ambao watasaidia kuinua sekta ya elimu ikiwemo:

(i) Majukumu ya wazazi wa wanafunzi katika kusimamia elimu za watoto wao pamoja na kufuatilia kwa karibu tabia na nyendo za watoto wao.

(ii) Kuonesha majukumu ya Walimu Wakuu pamoja na kuwekwa utaratibu maalumu wa upatikanaji wao, sifa wanazotakiwa kuwa nazo , uzoefu na maadili.

(iii) Kuongezwa na kuwekwa wazi majukumu ya Kamati za Skuli katika kuhakikisha ubora wa elimu katika Skuli zao, kupanga mikakati ya ubunifu katika Skuli hizo na kufuatilia njia za kuimarisha miundombinu ya kujifunzia kama maabara, maktaba, madarasa nakadhalika.

(iv) Majukumu ya wanafunzi wakiwa maskulini pamoja na taratibu za adhabu iwapo watashindwa kutekeleza majukumu yao.

(v) Upatikanaji wa wajumbe wa Kamati za Skuli pamoja na kuweka utaratibu wa Wizara ya Elimu kuwa na nafasi ya ushiriki na kuzisimamia Kamati za Skuli binafsi.

(vi) Wajibu wa jamii kwa ujumla katika kusimamia sekta ya elimu.

Vile vile, inapendekezwa Sheria hii ioneshe haki muhimu za wazazi, wanafunzi, walimu, walimu wakuu na jamii kwa ujumla.

**o) Usajili wa skuli**

Sehemu ya Tatu ya Sheria iliyopo katika vifungu vya 10,11, 13 14 na 15 vinahitaji kujumuisha msingi ya uwejibikaji na uwazi ili kuratibu vizuri eneo hili. Inapendekezwa Sheria iweke wazi masuala ya usajili kwa kuweka mambo yafuatato:

(i) Utaratibu wa usajili wa skuli za Serikali na binafsi ikiwemo masharti kwa skuli hizo ili ziendelee kuwa na usajili,

(ii) Kuanzishwa kwa rejista ambayo itaweka kumbukumbu za skuli zote zilizosajiliwa, idadi ya walimu, idadi ya wanafunzi, ufaulu wa skuli pamoja na hadhi zao;

(iii) Uwezo wa msajili wa skuli;

(iv) Masharti na vigezo zinavyopelekea skuli kusajiliwa au kukataliwa kusajiliwa kama vile uwezo wa walimu, uwezo wa kifedha kwa skuli, mazingira ya eneo linalotarajiwa kufunguliwa skuli, muundo wa jengo la skuli, n.k;

(v) Kufutiwa usajili na vigezo vinavyopelekea kufutiwa usajili na utaratibu wa rufaa ikiwa skuli haikuridhika na uamuzi wa kufutiwa usajili au kukataliwa usajili.

**p) Mfumo wa uendeshaji na muundo wa skuli za binafsi na Serikali**

Sheria iliyopo haijaweka masharti ya misingi ya skuli binafsi, ambazo kwasasa kumekuwa na wimbi kubwa la skuli hizo nchini. Inapendekezwa Sheria iweke wazi mfumo wa uendeshaji na muundo wa skuli za Serikali na binafsi. Mfumo wa uendeshaji uoneshe usimamizi, ufuatiliaji wa ufundishaji, nidhamu na mwenendo wa skuli, na udhibiti wa kuhakikisha skuli zinafundisha kwa mujibu wa mitaala iliopo na hakuna vitendo vyovyote kwa upande wa walimu na wanafunzi vinavyokiuka Sheria ya Elimu au Sheria nyengine ya nchi.

Aidha, inapendekezwa Sheria iweke masharti na utaratibu wa uanzishwaji wa skuli binafsi, usimamizi wake, usajili, kufutwa kwa skuli binafsi, utaratibu wa rufaa kutokana na uamuzi wa kuzifuta skuli hizo pamoja na kuonesha uwezo wa Serikali katika kusimamia skuli binafsi.

**q) Usimamizi na usajili wa walimu**

Sheria iliyopo imetambua usajili wa walimu katika vifungu vya 35-43 katika, sehemu ya 5, vifungu ambavyo havibainishi utaratibu wa usajili wala havitambui Mamlaka ya Usajili.

Inapendekezwa Sheria iweke utaratibu mzuri wa usimamizi wa walimu pamoja na usajili wao kwa kuwekwa masharti ya usajili kwa walimu, utaratibu wa maombi ya usajili kwa walimu, utaratibu wa kufuta usajili wa walimu pamoja na utaratibu wa kufuta walimu ambao hawana sifa na taratibu za rufaa kwa walimu wasioridhika na uamuzi wa kufutiwa usajili. Vile vile, Sheria iweke wazi kazi za Ofisi ya mrajis wa elimu, daftari la usajili, malalamiko ya walimu pmaoja na nidhamu kwa walimu.

Inapendekezwa kurekebishwa kifungu kinachozungumzia leseni ya walimu cha 42 na kuweka masharti mengine ambayo hayatakazwi ufundishaji na ukuzaji wa sekta ya elimu.

**r) Mamlaka na uwezo wa Waziri**

Sheria katika sehemu ya pili, vifungu vya 3 na 4 imeweka majukumu na uwezo wa Waziri ingawa baadhi ya mamlaka yanaweza kufanyiwa na vyombo au wasaidizi walio chini yake, hivyo kwa lengo la kumpa jukumu la usimamizi zaidi wa Sera na Mipango ya nchi.

Inapendekezwa Sheria iweke wazi kwa kuainisha Mamlaka, majukumu na uwezo wa Waziri katika kusimamia sekta ya elimu.

**s) Suala la wanafunzi wenye ulemavu**

Inapendekezwa Sheria iweke wazi utaratibu maalum wa upatikanaji wa elimu kwa wanafunzi wenye ulemavu bila ya kuwabagua wanafunzi hao. Sheria hii

iweke wazi upatikanaji wa haki ya elimu kulingana na aina ya ulemavu walionao wanafunzi hao. Aidha, inapendekezwa Sheria iweke sharti kwa Skuli kuhakikisha uwepo wa miundombinu itakayosaidia wanafunzi wenye ulemavu kufikia maeneo ya kujifunzia kwa urahisi pamoja na upatikanaji wa vifaa vya usaidizi kwa wanafunzi hao.

**t) Muundo wa Bodi ya Ushauri**

Sheria katika vifungu vya 5-6 vimeeleza uanzishwaji wa Bodi ya ushauri na majukumu yake. Hata hivyo baadhi ya majukumu ni ya kiutndaji zaidi kwa lengo la kukiimarisha chombo hiki kwa kukibadilisha kuwa Bodi ya Elimu na kukipa uwezo na mamlaka ya kuisaidia Wizara na Serikali katika suala la elimu.

Hivyo, Tume inapendekeza Sheria mpya iweke wazi Muundo wa Bodi, uanzishwaji wake, upatikanaji wa wajumbe wa Bodi pamoja na sifa zao, kazi na majukumu ya Bodi na muda wa kutumikia Bodi na maeneo mengine ambayo ni muhimu katika uanzishwaji na uendeshaji wa Bodi hiyo.

**u) Utaratibu wa usimamizi wa wanafunzi**

Suala la usajili wa wanafunzi na ujumuishwaji wa taarifa zao ni la msingi ili kupata taarifa (data base) za wanafunzi waliopo. Inapendekezwa Sheria iweke wazi utaratibu wa uwekaji wa taarifa za wanafunzi, usajili wa wanafunzi, uhamisho wa wanafunzi, umri wa mwanafunzi kuanza skuli na muda wa kukamilisha elimu ya maandalizi, msingi, sekondari na ngazi ya cheti na diploma.

**v) Usimamizi wa majengo na vifaa vya Skuli**

Inapendekezwa Sheria iainishe shughuli zinazopaswa kufanywa katika majengo ya skuli pamoja na kuweka utaratibu maalum wa usimamizi wa shughuli hizo ikiwemo muda wa kutumika kwa majengo hayo. Mapendekezo haya yanatokana na haja ya kutunzwa kwa majengo na vifaa hivyo ili vitumike na wanafunzi kwa muda mrefu.

**w) Uanzishwaji na usimamizi wa vyuo vya ufundi**

Sheria ya Elimu, katika sehemu ya Saba imeeleza katika vifungu vya 47-49 kuhusu usimamizi wa elimu ya juu, ambayo kwa sasa ni suala la Muungano. Hata hivyo, vipo vyuo ambavyo kitaratibu vinapaswa kusimamiwa na kuratibiwa na Wizara ya Elimu kwa maslahi ya nchi na sekta ya elimu Zanzibar, ambayo havitoi elimu ya juu.

Inapendekezwa Sheria ianzishe utaratibu wa usimamizi wa Vyuo vya ufundi na taaluma, ikiwemo uanzishwaji wa vyuo vya ufundi ambavyo havihusiani na elimu ya juu, usajili, vibali, maombi ya usajili, idadi ya wanafunzi, daftari la usajili, kufutwa kwa vyuo, pamoja na sifa za walimu.

**x) Makosa, adhabu na utaratibu wa rufaa**

Sheria ya Elimu imeweka makosa mbali mbali ya kisheria, ambayo baadhi yake hayawezi kusimamiwa katika wakati uliopo, adhabu zake ndogo na kuna baadhi ya masharti ya Sheria hayajawekewa adhabu.

Inapendekezwa Sheria iongeze makosa na adhabu katika maeneo mbali mbali ikiwemo makosa katika usajili na udhibiti wa walimu, ufundishaji. Vile vile,

Sheria iongeze viwango vya adhabu kwa makosa yanayofanywa chini ya Sheria hii kwa kuwa viwango vya adhabu viliopo sasa katika Sheria vipo chini sana.

Vile vile, inapendekezwa Sheria hii iainishe makosa madogo madogo ambayo yataruhusu utaratibu wa ulipaji faini kwa makosa hayo kwa lengo la kuyamaliza makosa madogo madogo kwa haraka ili kuepuka kuathiri shughuli na maendeleo ya wanafunzi.

### 7.4 Hitimisho

Sheria ya Elimu Nam. 6 ya mwaka 1982 ni sheria mama inayosimamia sekta ya elimu nchini na ni ya muda mrefu. Sheria hii imefanyiwa marekebisho katika mwaka 1993 na mwaka 2020. Aidha, mbali ya kuwepo kwa mabadiliko ya mifumo ya kielimu, uchumi, kijamii, kisayansi na teknolojia, mabadiliko ya Sera za nchi, Dira ya Maendeleo ya 2050 na malengo ya millenia, bado sheria hii haijafanyiwa marekebisho au mapitio makubwa ambayo yangepelekea kwenda sambamba na mabadiliko hayo.

Kutokana na umuhimu wa kuibadilisha sekta hii ya elimu, ili isaidie zaidi jamii na iendane na mipango ya nchi iliyopo, Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar iimeifanyia mapitio Sheria ya Elimu iliyopo na imefanya utafiti katika usimamizi na uendeshaji wa sekta ya elimu. Utafiti huu umezingatia na kujumuisha Sera na sheria mbalimbali, Mikataba ya Kimataifa, uzoefu wa nchi mbalimbali na sheria wanazozisimamia, maoni ya wadau na nyaraka mbalimbali zinazoeleza usimamizi katika sekta ya elimu.

Utafiti huu umependekeza kufanyiwa marekebisho Sera ya Elimu na kujumisha mikakati na matarajio yaliyowekwa katika mipango mikuu ya nchi ya mwelekeo wa elimu nchini ambayo inajumuisha mambo mbali mbali ikiwemo mitaala ya elimu na utaratibu wa kufanyiwa mapitio mitaala hiyo, miongozo kuhusiana na lugha ya kufundishia, mazingatio ya elimu mjumuisho, matumizi ya teknolojia katika ufundishaji, usimamizi wa sekta ya elimu pamoja na usajili wa walimu na mafunzo ya walimu.

Aidha, utafiti huu umependekeza kufutwa kwa Sheria ya Elimu iliopo na kutungwa kwa sheria mpya ambayo itazingatia mambo ya msingi ikiwemo kuweka wazi malengo ya kuwepo kwa Sheria ya Elimu, itaimarisha misingi katika masuala ya elimu, kuweka na kutambua vyombo vya usimamizi wa masuala ya elimu na kazi zake, kuweka utaratibu wa udhibiti wa Skuli za Serikali, binafsi, nidhamu kwa wanafunzi, haki na majukumu ya wazazi na wanafunzi, walimu wakuu, Kamati za Skuli na jamii kwa ujumla. Vile vile, Sheria hio itazingatia uanzishwaji na usimamizi wa vyuo vya ufundi pamoja na usimamizi katika suala la wanafunzi wenye ulemavu.

**REJEA**

**Mikataba ya Kimataifa**


Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu (1948)

Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW) wa mwaka 1979.

Sera ya Elimu ya Umoja a Nchi za Afrika Mashariki (EAC) 2016

Committee on Economic, Social and Cultural Rights, *General Comment 13, the Right to Education,* Twenty FirstSession, 1999,

Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni wa Mwaka 1966 (UN General Assembly, *International Covenant on Economic, Social and Cultural Rights*, 16 December 1966, United Nations, Treaty Series, vol. 993 )

Mkataba wa Haki za Mtoto wa mwaka 1989

Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW) wa mwaka 1979.

Mkataba wa Haki za Watu wenye Ulemavu wa mwaka 2006.

Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa mwaka 1966.

Mkataba wa UNESCO dhidi ya Ubaguzi katika Elimu wa mwaka 1960

Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa Mwaka 1981

Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto wa Mwaka 1990.

Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa haki za Binadamu na Watu kuhusu Haki za Wanawake katika Afrika ya mwaka 2003.

Mkataba wa Vijana wa Kiafrika wa mwaka 2006.

Dira ya Umoja wa nchi za Afrika Mashariki 2050

Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni wa mwaka 1966 unapatikana UN General Assembly, *International Covenant on Economic, Social and Cultural Rights*, 16 December 1966, United Nations, Treaty Series, vol. 993

Manual for Human Rights Education with Young people, Council of Europe inapatikana Compass: Manual for Human Rights Education with Young People - Manual for Human Rights Education with Young people (coe.int)

**Sheria za nchi mbalimbali**

Sheria ya Elimu ya Shelisheli (Seychelles) Nam. 13 Ya Mwaka 2004

Sheria ya Elimu ya Singapore ya Mwaka 1957

Sheria ya Elimu ya Lazima ya Mwaka 2000 Singapore

Sheria ya Elimu ya Kenya Sura 211.

Sheria ya elimu ya Msingi ya Finland Nam. 628 ya mwaka 1998
Sheria ya Elimu Nam. 21 ya 2002 ya Grenada, Sura ya 86
Sheria ya Tanzania Nam. 25 ya mwaka 1978
Sheria ya Elimu ya Ghana Nam.778 ya Mwaka 2008

**Mipango Mikuu na Sera**

ILANI ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025
Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050
Sera ya Elimu ya mwaka 2006
Sera ya Afya na Usalama Kazini Zanzibar ya Mwaka 2016
Sera ya Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2018
Sera ya Uhakiki wa Chakula na Lishe Zanzibar ya Mwaka 2008

**Sheria za Zanzibar**

Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984
Sheria ya Elimu, Sura ya 9 ya mwaka 1959 (The Education Decree, 9/1959).
Sheria ya Mfuko wa Elimu ya Juu Zanzibar ya Nam.6 ya mwaka 2001
Sheria ya Elimu Nam. 6 ya 1982
Sheria ya Kuwalinda Wari na Watoto wa Mzazi Mmoja Nam. 4 ya mwaka 2005
Sheria ya Mtoto Nam. 4 ya mwaka 2005
Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu Zanzibar Nam. 3 ya mwaka 2011.
Sheria ya Baraza la Mitihani Zanzibar Nam. 6 ya Mwaka 2012.
Sheria ya Bodi ya Huduma za Maktaba Zanzibar Nam. 7 ya Mwaka 1993
Sheria ya Taasisi ya Elimu Nam. 14 ya mwaka 2016
Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyuo vya Amali Nambari 8 ya mwaka 2006
Sheria ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu Nam. 10 ya mwaka 2018
Sheria ya Tume ya Kurekebisha sheria Zanzibar Nam. 16 ya mwaka 1986
Sheria ya Elimu Nam. 6 ya mwaka 1982
Sheria ya Marekebisho Nam. 4 ya mwaka 2020

**Vitabu na Makala**

Abagi, O. and Odipo, G (2000). Implementing the Report of the Commission of Inquiry into the Education System Dar es salaam Data star

Abdalla. S.M. (2014) Education statistical Abstract Ministry of Education and vocational training Zanzibar

Abdulghani Al-Shuaibi (2014) The Importance of Education, Salalah College of Technology,

Anangisye, W. A., & Fussy, D. (2014). Tanzania: Revisiting eastern and central African education systems. In C. Wolhuter (Ed.), Education in East and Central Africa, (pp. 373—398). London: Bloomsbury

Asterhan, S. N. Clarke & L. B. Resnick (Eds.) Socializing intelligence through academic talk and dialogue (pp. 63-76). Washington, DC: American Educational Research Association.

Bryk, A. S., Gomez, L. M., Grunow, A., & LeMahieu, P. G. (2015). *Learning to improve. How America's schools can get better in getting better*. Harvard Education Press.

Bogonko, S. N. (2000). Reflections on education in East Africa. Nairobi Kenya: Oxford University Press

Berjaoui, R. R. & Karami-Akkary, R. (2019): Distributed leadership as a path to organisational commitment: the case of a Lebanese school. Leadership and Policy in Schools, 19(4), 610-624.

Bigge, M.L. & Shermis, S.S. (1992). Learning Theories for Teachers. (5th ed.). New York: Harper Collins Publishers.

Boezaart, T. (2012): A Constitutional Perspective on the Rights of Children with Disabilities in an Educational Context. South African Journal of Public Law, 27, 465-472.

Boyd, W. L., & Crowson, R. L. (2002). The quest for a new hierarchy in education: From loose coupling back to tight? *Journal of Educational Administration*, *40*(6), 521–533

Carneiro, R. (2007): The big picture: understanding learning and meta-learning challenges. European Journal of Education.

Choudhuri, Indranath. 2005. Promoting Value Education through Children's Literature. Journal of Value Education, 5, 29-36.

Cohen, L., Manion, L., & Morrison, K. (2018). *Research methods in education* (8th ed.). Routledge.

Everard, K.B. Geoffrey, M. & Wilson, J. (2004). *Effective school management.* Fourth Edition. London: Paul Chapman Publishing

Dewey, John (2016). Democracy and Education. New YorkThe Free Press Education

Education and Manpower Bureau (2003): Enhancing school development and accountability through school self-evaluation and external school review. EMB Circular No. 23/2003.

Falvey, M. A. (2004). Toward realizing the influence of "Toward realization of the least restrictive educational environments for severely handicapped students.". Research and Practice for Persons with Severe Disabilities

Fisher, R. 1990. Teaching children to think. Nelson Thornes, Cheltenham.

Giangreco, M. F., Broer, S. M., & Edelman, S. W. (2001). Teacher engagement with students with disabilities: Differences between paraprofessional service delivery models. Research and Practice for Persons with Severe Disabilities, 26(2), 75–86.

Hija, I. M. (2010) Zanzibar. International Encyclopedia of Education (Third Edition), 896-903

Imaguezor, M. V. (1997). Analysis of Cases of Violation of Students Rights in Secondary Schools in Edo State. M.Ed Thesis, University of Benin, Nigeria.

International Disability and Development Consortium. (2013). *Teachers for all: Inclusive education for children with disabilities.*

Joanna Giota & Ingemar Emanuelsson (2018) Individualized teaching practices in the Swedish comprehensive school from 1980 to 2014 in relation to education reforms and curricula goals, Nordic Journal of Studies in Educational Policy

John, B. & Earl, M. (2003). Key *issues in secondary education: Introductory readings.* New York: Continuum

Kumar, S. & Ahmad, S. (2008): Meaning, aims and process of education. In: School of Open Learning. Newark: Science and Education Publishing

Kuleana (1999). The State of Education in Tanzania: Crisis and Opportunity. Mwanza, Kuleana in Tanzania: Debate and Action. Dar es Salaam, University of Dar es Salaam Convocation

Letseka, M. M. (2013): Understanding of African Philosophy through Philosophy for Children (P4C). Mediterranean Journal of Social Sciences, 4(14), 745-753

Labon, D. (1999). Inclusion education at work: Students with disabilities in mainstream schools. Washington, DC: Organisation for Economic Co-operation and Development

Giangreco, M. F., Broer, S. M., & Edelman, S. W. (2001). Teacher engagement with students with disabilities: Differences between paraprofessional service delivery models. Research and Practice for Persons with Severe Disabilities, 26(2), 75–86.

Lofchie, M. F. (2015). Zanzibar: Background to revolution. United States of America: Princeton University Press.

Martin, A. J., Nejad, H., Colmar, S. & Liem, G. A. D. (2012): Adaptability: Conceptual and empirical perspectives on responses to change, novelty and uncertainty. Journal of Psychologists and Counsellors in Schools, 22(1), 58-81.

Mapuri, O. R. (1996). Zanzibar, the 1964 revolution: Achievements and prospects. Dar es Salaam: Tema.

MEoC(2001).Education sector development programme: Primary Education Development Plan, 2002– 2006.Dar es Salaam: United Republic of Tanzania Mkuki Press

Moberg, G. (2000). *Development of teacher perceptions of inclusive education in Finland*. Paper presented at the 11th International Association for Scientific Study of Intellectual Deficiency, World Congress, Seattle, WA.

Mulford, B., Kendall, D., Ewington, J., Edmunds, B., Kendall, L. & Silins, H. (2008): Successful principalship of high-performance schools in high-poverty communities. Journal of Educational Administration, 46(4), 461-480.

Ninni Wahlstorm, Daniel Sundgerg (ed) (2018) Transnational Curriculum Standards and Classroom Practices The New Meaning of Teaching, 1st Edition, Routledge.

Nakpodia, E.D. (2009). Perceptions of Principals' Responsibilities in in-loco-parentis in Nigerian Secondary Schools. *Journal of Education Administration and Policy Studies*.

Nyerere, J.K (1967). Education for Self -Reliance. Arusha United Republic of Tanzania

Obraori Nmabunwa Peters Adiela & Chinuru Achinewhu Safeguarding the Future and Right to Education of Children with Disabilities in Nigeria, in New Challenges to Education: Lessons from Around the World BCES Conference Books, 2021, Volume 19. Sofia: Bulgarian Comparative Education Society ISSN 2534-8426

Opper, I. (2019): Teachers Matter: Understanding Teachers' Impact on Student Learning. Santa Monica, CA: Rand Corporation.

Prodhan, M. (2016): The educational system in Bangladesh and scope for improvement. Journal of International Social Issues.

Randall, L. & Coakley, L. (2007): Applying adaptive leadership to successful change initiatives in academia. Leadership & Organization Development Journal, 28(4), 325- 335

Revolutionary Government of Zanzibar Ministry of Education and Vocational Training, Zanzibar Education Development Programme (ZEDP) 2008/09 – 2015/16 DRAFT 3 February 6, 2007

R.P.L Loimeier, Between Social Skills and Marketable Skills, Chapter Five. The Politics of Education in the Colonial Period I: Schools

Russell, T. & Munby, H. (1992). Teachers and Teaching from Classroom to Reflection. London: Falmer Press.

Scottish Office (2002): How good is our school? Self-evaluation using performance indicators. Edinburgh: the Scottish Office of Education and Industry Department.
Serdyukov, P. (2017): Innovation in education: what works, what doesn't, and what to do about it? Journal of Research in Innovative Teaching & Learning, 10(1), 4-33.

Sokal, L., Trudel, L. E. & Babb, J. (2020): Canadian teachers' attitudes toward change, efficacy, and burnout during the COVID-19 pandemic. International Journal of Educational Research Open, 1,

Spilt, J. L., Koomen, H. M. & Thijs, J. T. (2011): Teacher wellbeing: The importance of teacher-student relationships. Educational Psychology Review, 23(4), 457-477.

Sun, J., Anderson, R., Lin, T. & Morris, J. (2015): Social and cognitive development during collaborative reasoning. In C. S.

UNESCO (2015): Rethinking Education: Towards a global common good? Paris: UNESCO. Witherspoon,

UNICEF (2007): Promoting the Rights of Children with Disabilities. Innocenti Digest No 13. Florence, Italy: UNICEF Innocenti Research Centre.

World Bank (1996). Tanzania: The Challenge of Reforms: Growth, Incomes and Welfare.Volume 1, World Bank

W. Hendry Some Aspects of Education in Zanzibar, Journal of the Royal African Society, Vol. 27, No. 108 (Jumai 1928), pp. 342-352  published By: Oxford University Press

Zehlia Babaci- (2015) "Zanzibar's Curriculum Reform: Implications for Children's Educational Rights," part of comparative and International Education book series, Q*uarterly Review of Comparative Education*